# Nipashe

Alhamisi Novemba 3, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581118

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13


SUPA JACKPOT
TZS.1,046,433,814
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




## Mpina akomaa TRAB na TRAT, Bunge lataka hatua serikalini

UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizindua mradi wa visima 10 vya maji vyenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 70 kwa siku, Kigamboni mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

MGAWO WA MAJI

# Waziri Mkuu aingilia kati

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### KIKOSI KAZI CHAIBUA NENO UCHAGUZI WA RAIS

KIKOSI kazi cha kamati maalum iliyoundwa kuchambua maoni mahsusi...

## Aagiza wafugaji waondoke Liwale

UKURASA 3

RIPOTI MAALUM



UKURASA 4

Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mjini Wingwi wakivuka daraja linalounganisha vijiji vya Chupwe na Sebudawa, Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maji ya bahari yavamia makazi


NBC Twiga Bond
Wekeza kwenye ndoto zako na hatifungani inayokupa
10% faida kila mwaka
*Vigezo na Masharti kuzingatiwa
Tangazo hili na Waraka wa Matarajio wa hatifungani ya NBC Twiga imeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)
NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe.



Mwenyekiti wa kikundi cha Gerezani Youth, Sheikh Firoz Bituri (kulia), akikabidhi zawadi kwa Imamu wa Msikiti wa Kichangani Magomeni, Sheikh Alhad Walid Kawambwa, katika mkesha wa Maulid jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa aingilia mgawo wa maji

**Na Frank Monyo**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameiagiza Wizara ya Maji kwa kushirikiana na sekta binafsi ihakikishe inakamilisha taratibu za utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Mto Rufiji utakaosambaza maji katika maeneo ya Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam.

Vilevile, ameielekeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) iendelee kutenga fedha kwa ajili ya uchimbaji wa visima zaidi kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa maji, akionya: "Tusipokuwa makini, tutaingia katika janga la ukame."

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana baada ya kukutana na Waziri wa Maji, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Pwani na viongozi wa DAWASA kwa ajili ya kujadili hali ya upatikanaji wa maji katika mkoa huo ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan.

Juzi Rais Samia wakati wa Kongamano la Kitaifa la Nishati Safi ya Kupikia, alimwagiza Waziri Mkuu kuhakikisha anasimamia uunganishwaji wa maji kutoka Kigamboni kuja maeneo mengine ya Jiji la Dar es Salaam pamoja na kuangalia maunganisho ya maji ili kukabiliana na uhaba wa maji katika jiji hilo.

Waziri Mkuu alisema serikali itahakikisha maeneo yote yanapata huduma za maji na kazi ya uchimbaji visima na kutafuta vyanzo vingine vya maji inaendelea ili kufikia matamanio ya Rais Samia ya kufikisha huduma ya maji karibu na makazi ya wananchi.

Akizungumza baada ya kukagua na kuwasha pampu ya maji katika mradi wa visima vya maji Kigamboni, Waziri Mkuu alisema visima hivyo ambavyo vina uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 70 kwa siku, vitasaidia katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa maji katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Waziri Mkuu alisema mahitaji ya maji katika Mkoa wa Dar es Salaam ni lita milioni 544 kwa siku na uzalishaji maji kwa siku ni lita milioni 520 katika kipindi ambacho kiwango cha maji katika Mto Ruvu kinakuwa katika hali ya kawaida, hivyo kuwa na upungufu wa lita zaidi ya milioni 20.

"Katika kipindi hiki ambacho kiwango cha maji katika Mto Ruvu kimepungua, uzalishaji wa maji nao umepungua na kufikia lita milioni 300 kwa siku, hivyo kusababisha upungufu wa lita milioni 244. Kwa sasa tukiingiza lita milioni 70 kutoka katika mradi huu wa visima vya Kigamboni, tutakuwa na upungufu wa lita milioni 174, hivyo tutapunguza changamoto ya upatikanaji wa maji katika baadhi ya maeneo," alifafanua.

Waziri Mkuu pia alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali ilitoa Sh. bilioni 25 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa uchimbaji visima 10 katika eneo la Kigamboni. Kati yake, visima saba vimewezesha upatikanaji wa lita milioni 70. Aliwaagiza watendaji DAWASA waendelee na uchimbaji wa visima vingine.

Awali, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso alisema katika kuhakikisha maji ya uhakika yanaendelea kupatikana katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwamo Dar es Salaam, wizara inaendelea kufanya tathmini ya kutumia maji ya ardhini. Alisema kama wameweza kupata lita milioni 70 Kigamboni, hivyo anatarajia watapata maji mengi zaidi kupitia miradi ya uchimbaji wa visima.

Akizungumzia kuhusu mradi wa kutoa maji kutoka Mto Rufiji, waziri huyo alisema wizara inaendelea na ufuatiliaji wa mradi huo ambao unatarajiwa kuzalisha maji lita milioni 750 kwa siku na hivyo kuondoa tatizo la uhaba wa majisafi na salama katika maeneo ya Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

Kumekuwa na kilio cha uhaba wa maji katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na ukame uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa vyanzo vya maji.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455 Mtaa wa Mtumba,
Fax: +255 26 2323233 S.L.P. 2888,
Barua Pepe: ps@mow.go.tz 40470DODOMA,
Tovuti: www.mwtc.go.tz 03.11.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumamosi tarehe 05-11-2022 hadi 08-11-2022 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea JNHPP SITE, gari hizo zina namba za usajili:
**T 681 DUB / T 777 AQR T 454 DYG / T 394 DVS T 645 DFA / T 390 DHQ T 559 BKC / T 321 DDH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 20**
**Upana - mita 7.40**
**Kimo - mita 5.10**

3. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM hadi JNHPP SITE kupitia KILWA ROAD, KIBITI, MLOKA.**
Gari zitasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 06:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka Dar es Salaam Port mpaka Bungu.
Kutoka Bungu kwenda **JNHPP Site** gari zitasafiri muda wa mchana ***( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

117131202

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**


# Mpina akomaa na TRAT na TRAB

**Na Waandishi Wetu,**
DODOMA

MBUNGE wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina ameibua tena bungeni sakata la Sh. trilioni 360 za malimbikizo ya kodi za makinikia na kutaka serikali iliambie Bunge ukweli.

Akichangia jana bungeni taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Mpina alisema maelezo yaliyotolewa kuhusu fedha hizo kwamba zimeshasamehewa zote huku ikidaiwa hazijasamehewa, yanapaswa kuwekwa sawa ili Bunge lipate hatima ya fedha hizo.

Alisema kodi hizo zilikuwa zimeshikiliwa na mamlaka za rufani za kikodi za TRAB na TRAT.

"Serikali ilituambia hapa Januari 2020 serikali ilifuta madai haya, lakini taarifa ya CAG (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2019/20, inatambua serikali inadai Sh. trilioni 360 na ilipofikia taarifa ya CAG ya mwaka 2020/21 anasema inaonyesha kuwa kesi za makinikia zenye thamani ya Sh. trilioni 5.595 zimeamriwa na TRAB na TRAT na ilipoamriwa serikali iliagizwa kufanya majadiliano na kampuni zilizopaswa kulipa kodi hizo," alisema.

Mpina alisema amefuatilia ripoti za viongozi ikiwamo vikao vyote vya Hayati Rais Dk. John Magufuli na Rais Samia Suluhu Hassan kama waliwahi kuzungumza kusamehe kodi hizo za Sh. trilioni 360.

"Hawajawahi kuzungumza fedha hizi zimefutwa, mahakama iliagiza kampuni za madini na serikali wajadiliane namna ya kulipa Sh. trilioni 5.595, sasa aliyeagiza kodi hizo zisamehewe ni nani? CAG alete taarifa juu ya jambo hili ili Watanzania wajue hitimisho na fedha zao. "Nchi hii maskini haiwezi kuingia makubaliano ya kusamehe kodi kubwa hizo, halafu tukaendelea kutoza kodi ndogo ndogo kwa wananchi, tunaacha wafanyabiashara wakubwa kama hawa wanasamehewa na nani? Na tulishaeleza hizi kodi zilipatikanaje.

"Serikali itoe kauli kuhusu hili na CAG akachukue nyaraka zote kama Dk. Magufuli alisamehe hili deni au Rais Samia. Tuletewe hapa ili tufanye uamuzi kama Bunge," alisema.

Kauli hiyo ilimwinua kwenye kiti Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, George Simbachawene, akimtaka Mpina kueleza vizuri kinachotokea kwenye rufani za kikodi kukiwa na mgogoro na kodi.

Simbachawene alisema kuna wanaodaiwa walishafunga kampuni na mazingira ya aina hiyo yalichangia wawekezaji kuondoka.

**PAC NA MADUDU**

Awali Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilibainisha 'madudu' ya upotevu wa fedha katika mashirika mbalimbali ya umma kwa mwaka 2020/21, ikiwamo Mamlaka ya Mapato (TRA) iliyoshindwa kukusanya mapato kwa asilimia 14 sawa na Sh. trilioni 2.8.

Kamati hiyo pia imebaini Shirika la Umeme (TANESCO), Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) na Shirika la Madini (STAMICO) kwa mwaka huo yalikuwa na uwiano usio mzuri wa madeni kulinganisha na mtaji wa jumla.

Taasisi zingine zilizobainika kufanya vibaya ni pamoja na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya PSSSF na NSSF, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HELSB), benki za TIB, TCB, Mfuko wa Jeshi la Polisi wa Tuzo na Tozo na Jeshi la Uhamiaji.

Akiwasilisha bungeni jana jijini Dodoma taarifa ya PAC, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisema TRA ilifanya vibaya katika ukusanyaji wa mapato kulinganisha na makadirio waliyojiwekea kwa mwaka wa fedha unaoisha Juni 30, 2021 na kwamba kulikuwa na nakisi ya ukusanyaji wa mapato ya Sh. trilioni 2.8 na imechangiwa na matatizo mbalimbali likiwamo ongezeko kidogo la makusanyo ya kodi.

Hasunga alisema kamati imetoa mapendekezo katika maeneo mahsusi ikiwamo kuishauri TRA kuboresha mifumo yake ya ukusanyaji wa kodi na serikali kuboresha shughuli za vyombo vinavyohusika na kushughulikia rufani za kodi (TRAT na TRAB).

Kamati hiyo pia imependekeza Msajili wa Hazina kuangalia namna bora ya kuongeza mtaji katika Mashirika ya kimkakati ya TANESCO, TPDC na STAMICO. Kuhusu ukaguzi maalum Idara ya Uhamiaji (Viza na stika bandia), Hasunga alisema ulibaini wageni 33,558 waliwasili nchini kupitia KIA, lakini taarifa zao ambazo ni pamoja na fomu za kuingia nchini, stakabadhi za mapokezi ya fedha (ERV) na uwekaji fedha benki hazikupatikana kwa ajili ya uhakiki.

Kwa sababu hiyo, ukaguzi haukuweza kuthibitisha kiasi cha mapato ambacho serikali ilipaswa kupata kutoka kwa wageni hao na kupendekeza watumishi wa idara ya uhamiaji 32 wachukuliwe hatua.

Hasunga pia alisema kamati imebaini mifuko ya PSSSF na NSSF haijapata faida katika miradi iliyowekeza mabilioni ya shilingi kutokana na kutokuwa na mikakati madhubuti ya masoko na mauzo.

■**Imeandaliwa na Augusta Njoji na Richard Makore**



Rais mstaafu wa Bunge la Pan Afrika, Gertrude Mongela (kushoto), akizungumza kwenye kongamano la kitaifa kuhusu nishati safi ya kupikia lililoandaliwa na Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Waziri wa Fedha mstaafu, Zakia Meghji (wa pili kushoto), Waziri mstaafu na Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa UN-HABITAT, Prof. Anna Tibaijuka (wa tatu kushoto) na mwongoza mjadala, Doris Rwebangira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri atoa siku 14 polisi kuwaondoa wafugaji Liwale

**Na Mwandishi Wetu,** LIWALE

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni amelipa siku 14 Jeshi la Polisi mkoani Lindi kuwaondoa wafugaji katika maeneo ambayo hayajatengwa na serikali wilayani Liwale kwa ajili ya shughuli za ufugaji.

Masauni aliyefuatana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi katika ziara hiyo, alitoa agizo hilo jana kutokana na migogoro kati ya wafugaji na wakulima iliyosababisha vifo vya watu 12 mkoani Lindi.

Akizungumza na mamia ya wananchi wa Kijiji cha Linegene, Kata ya Mirui, Waziri Masauni alisema kitendo cha wafugaji kufanya shughuli za ufugaji katika maeneo ambayo hayaruhusiwi kufanya kazi hizo, ndiyo sababu ya kutokea mauaji hayo ambayo yanasababishwa na mifugo kuingizwa katika mashamba ya wakulima na hivyo kuchangia migogoro isiyoisha.

"Ninatoa siku 14 kwa Jeshi la Polisi, wahakikishe wafugaji wote waliopo katika maeneo ambayo hayaruhusiwi kwa ajili ya ufugaji waondolewe haraka iwezekanavyo," aliagiza.

Waziri Masauni aliwataka polisi kuwakamata wafugaji ambao wanatembea na visu, mapanga, panga, nondo, mikuki na mishale maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo ambapo silaha hizo zinasababisha watu kujeruhiwa pamoja na mauaji.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki aliwataka wafugaji waliopo wilayani humo kuondoka haraka iwezekanavyo katika maeneo yote ambayo hayaruhusiwi kwa ajili ya mifugo.

"Mimi ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi lakini sipendi kuona wafugaji wanaleta taharuki katika nchi hii, wanavunja sheria, wanapaswa kufanya ufugaji unaotambulika. Kwanini tufanye kiuhalifu? Haiwezekani, lazima tuishi kama watu na siyo kuishi kama wanyama. Yeyote anayelisha shamba la mtu, huyo akamatwe ashughulikiwe vizuri, apigwe faini, afungwe, acheni mambo ya kitoto kama hayo," alionya.

Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi Nchini, Awadhi Haji alisema jeshi hilo haliwezi kuchezewa, hivyo litachukua nafasi yake kwa kuwakamata wanaofanya uhalifu wilayani humo.

"Ninarudia tena, tutafanya operesheni ya nyumba kwa nyumba na pia tutawakamata wafugaji wanaotembea na silaha, wananchi endeleeni kutupa ushirikiano katika kupambana na hawa wahalifu," alisema.

Mkazi wa Kata ya Mirui, Joseph Abdalla alidai wafugaji katika kijiji hicho wameingiza ng'ombe katika shmaba lake na kumsababishia hasara kubwa, na alipohoji, walimjibu hawana sehemu ya kulisha mifugo hiyo.

Mawaziri hao wanaendelea na ziara katika mkoa huo ili kudhibiti migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo inaendelea kuleta madhara ya watu kujeruhiwa na hata vifo.

# Kikosi kazi chaibua neno uchaguzi wa Rais

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIKOSI kazi cha kamati maalum iliyoundwa kuchambua maoni mahsusi ya demokrasia Zanzibar, kimewasilisha ripoti kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ambayo pamoja na mambo mengine kimependekeza matokeo ya urais Zanzibar yahojiwe mahakamani.

Kimesema utaratibu huo utakuza demokrasia na kuongeza uwazi katika usimamizi wa uchaguzi.

Akiwasilisha ripoti hiyo jana, Ikulu, Zanzibar, mbele ya Dk. Mwinyi, Mwenyekiti wa Kikosi Kazi hicho, Dk. Ali Uki, pia kuna mapendekezo ya utaratibu wa kura ya mapema kuendelea isipokuwa uadilifu uzingatiwe katika uchaguzi na masuala yote yanayoleta hofu wakati wa uchaguzi yafanyiwe kazi.

Dk. Uki alisema utaratibu huo wa kupiga kura ya mapema uendelee, isipokuwa vyama vya siasa viache kuhamasisha wanachama kuvunja sheria wakati wa kampeni na kupiga kura.

Pia alisema wamekubaliana kwa pamoja kuwapo kwa tume ya maridhiano ya kisiasa kwa ajili ya kuleta usuluhishi na kuhakikisha maridhiano yanatekelezwa na kusimamiwa kwa nguvu zote na kuwekewa misingi ya kisheria.

Aidha, Dk. Uki alisema inapendekezwa muundo wa serikali ya umoja wa kitaifa unashuka hadi chini katika ngazi za uongozi wa chini wakiwamo masheha. Kwa mujibu wa Dk. Uki, mapendekezo ya uteuzi wa masheha yazingatie sifa na kuepuka mwelekeo wa kisiasa.

Kuhusu muundo wa tume ya uchaguzi, alisema inapendekezwa nafasi ya mwenyekiti na wajumbe wake zitangazwe na kuombwa kuwapo timu ya kupokea maombi kwa ajili ya uteuzi.

Katika daftari la kudumu la wapigakura, alisema ufahamike utaratibu wake kikamilifu ikiwamo wananchi kupata vyeti vya kuzaliwa na vitambulisho vya Mzanzibari mkazi ambavyo ni muhimu katika upigaji kura.

Mambo mengine yaliyopendekezwa ni pamoja na mgawanyo wa nafasi za ajira katika taasisi za Muungano kutazamwa upya. Kwa sasa Zanzibar inapata mgawo wa asilimia 21 katika ajira taasisi za Muungano wakati Tanzania Bara mgawo wake ni asilimia 79.

Pia kamati hiyo imependekeza kuenziwa kwa tunu za kitaifa ikiwamo Mapinduzi ya Januari 12, mwaka 1964, kuwa ndiyo yaliyowakomboa wananchi wa Zanzibar na kuwa huru katika nchi yao.

Alisema pia kikosi kazi kimependekeza masuala ya uzalendo, ukweli, kustahimiliana na kuvumiliana yawe mambo ya msingi ya kuzingatiwa katika kujenga misingi ya taifa lenye uadilifu kwa wananchi wake.

Dk. Uki alisema suala la elimu ya uraia linatakiwa kufundishwa na kuendelezwa na kupewa kipaumbele kwa vijana ikiwamo shuleni ili kufahamu taifa wapi linatoka.

Makamu Mwenyekiti wa Kikosi Kazi, Balozi Amina Salum Ali, alisema wamejifunza katika kipindi cha siku 15 uvumilivu wa kisiasa katika kuendesha mambo mbalimbali yenye mustakabali wa taifa na kuwa wamoja.

Alisema suala la uzalendo ni muhimu ambalo linatakiwa kuzingatiwa na kuwa sehemu ya kipaumbele cha wananchi wa Zanzibar katika kuwaunganisha na kuondokana na siasa za chuki zenye kujenga uhasama.

Dk. Mwinyi baada ya kupokea ripoti hiyo, aliahidi katika uongozi wake kutekeleza na kusimamia maridhiano ya kisiasa ambayo ndiyo yatakayoihakikishia Zanzibar kuwapo kwa amani ya kudumu na wananchi kufanya shughuli zao na kukuza uchumi.

Alisema katika ripoti hiyo yako mambo yanahitaji kutekelezwa muda mfupi na mengine kuchukuwa muda mrefu na mengine yanahitaji marekebisho ya katiba.

Alisema kwa yale mambo yanayohusu mabadiliko ya katiba yatapelekwa kwa wataalamu serikalini na kuyapitia kwa ajili ya kufanyiwa kazi.


The Guardian Limited

VACANCY

Freelancer Sales Executive

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our advertising sales team in **Dar es Salaam, Mwanza and Kilimanjaro.**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration or Sales & Marketing
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th November, 2022.**

67131002

## MABADILIKO TABIANCHI

# Maji ya bahari yavamia makazi

## ■Safari za shule zakwama, kijiji chaumiza kichwa

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa** PEMBA

UKIINGIA katika Shehia ya Mjini Wingwi, Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba, mara moja utashuhudia kwa vitendo athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo sasa ni kilio cha ulimwengu.

Athari zipo dhahiri zaidi katika vijiji viwili vya Chupwe na Sebudawa, ambako wanafunzi wake wanalazimika kuvuka daraja lililojengwa kwa miti ili kuifikia shule ya msingi wanakosoma.

Shida kuu iliyosababisha wazazi kuibuka na ubunifu huo wa daraja la miti ni kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari ambayo yamevamia makazi ya asili ya watu na shughuli za kijamii.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mjini Wingwi, Juma Khamis Kombo, anarejea historia ya kituo hicho cha elimu kwamba katika miaka ya 1990, wanafunzi walikuwa na mahudhurio mazuri lakini milenia ilipobadilika, yaani miaka ya 2000, utoro ulikithiri miongoni mwa wanafunzi baada ya kina cha maji kuongezeka kwenye eneo hilo la kivuko.

"Kina cha maji ya bahari kiliongezeka hapa tulipojenga daraja na kufunga njia inayokuwa inatumiwa na watoto kuja shuleni na kurudi majumbani, hivyo utoro ukaongezeka. "Kwa wastani watoto 500 walishindwa kuhudhuria shuleni kwa siku na wale wachache waliofanikiwa walikumbana na vikwazo vingi kama kuanguka na madaftari yao kuingia kwenye maji.

"Maji yaliongezeka sana, magogo ya mnazi yaliyokuwa yamewekwa kama kivuko na wanavijiji, yalifunikwa na maji na kuoza, hivyo ilikuwa shida kwa wanafunzi kuvuka," anasimulia.

Mwalimu Mkuu Kombo anabainisha kuwa shule hiyo kwa sasa ina wanafunzi 1,272 na kwamba zaidi ya nusu yao wanaishi katika vijiji vya Chupwe na Sebudawa.

"Tulipobaini utoro umezidi, tuliitisha kikao cha wazazi ili kutatua shida hiyo, wanavijiji waliamua kwa pamoja kujenga daraja la miti ili kuwezesha watoto kupata haki ya elimu," Mwalimu Kombo anafafanua.

Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Miradi ya Jamii kisiwani huko, Masoud Kombo anasema daraja hilo limesaidia kupunguza utoro miongoni mwa wanafunzi ingawa siyo la kudumu.

"Baada ya daraja hili kujengwa, tumefanikiwa kuwarejesha shuleni watoto 118 ambao walikuwa wamekatisha masomo kwa sababu ya kukosekana kivuko.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mjini Wingwi wakiwa kwenye daraja linalounganisha vijiji vya Chupwe na Sebudawa kisiwani Pemba mwanzoni mwa juma lililopita. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

"Hata hivyo, tunaiomba serikali itujengee daraja la kudumu kwa sababu daraja lililoko sasa ni la miti. Kina cha maji kinaendelea kuongezeka, hivyo miti inaweza kuoza.

"Hofu yetu kama daraja hili litakatika, utoro wa wanafunzi unaweza kujirejea tena, hivyo suluhisho ni kujengwa daraja la kudumu hapa," anashauri.

Kaimu Sheha wa Mjini Wingwi, Hussein Makame Hamad anasema daraja la miti lililojengwa, limekuwa mkombozi kwa wanafunzi wa vijiji vya Chupwe na Sebudawa.

"Daraja hili ingawa siyo la kudumu limerejesha furaha iliyopotea kwa wazazi na watoto, mahudhurio darasani yameongezeka," anapongeza jitihada za wanakijiji.

Anabainisha kuwa Sh. milioni 7.3, ambazo ni mchango wa wanakijiji na wahisani, zimetumika katika ujenzi wa daraja hilo la miti lenye urefu wa mita 60.

Mpaji Hassan, mwanakijiji wa Chupwe, anasema ili kukabiliana na ongezeko la maji ya bahari na athari zingine za kimazingira, wameotesha mikoko zaidi ya 3,000 kuzunguka eneo la daraja.

"Kwa sababu daraja hili siyo la kudumu, tunawaomba wahisani kuchangia ili tujenge daraja la kudumu ambalo litahakikisha wanafunzi wetu kusoma katika mazingira rafiki," mama huyo anawasilisha kilio chao.

Time Shaibu, mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Mjini Wingwi, anakiwa kuwa miongoni mwa wanafunzi walioathiriwa na mabadiliko ya tabianchi lakini sasa ana uhakika wa kufika shuleni kila siku za masomo kutokana na ujenzi wa daraja.

"Sasa ninahudhuria masomo bila kukosa. Kabla ya daraja kujengwa, nilikaa nyumbani zaidi ya miezi mitano wakati huo nikiwa darasa la nne, njia tuliyokuwa tunaitumia ilikuwa haipitiki, lakini sasa hali ni tofauti, tunakuja shuleni kila siku za masomo," mwanafunzi huyo wa kike anasema.

Ali Salim Mata, Ofisa Mdhamini Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba, anapongeza hatua zilizochukuliwa na wanakijiji kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha watoto wao wanarejea shuleni.

"Serikali pekee haiwezi kuzuia athari za mabadiliko ya tabianchi na maeneo yaliyoathirika ni mengi. Wanavijiji wa Chupwe na Sebudawa waliamua kujenga daraja na kupanda mikoko ili kuzuia athari za kuongezeka maji ya bahari, hili ni jambo la kuigwa," anapongeza.

Mata aliwahimiza wanavijiji wengine ambao maeneo yao yamevamiwa na maji ya bahari, kuiga mfano huo kwa kupanda mikoko kwenye maeneo yao.

Anataja hatua zaidi zilizochukuliwa na ofisi yake zinajumuisha serikali kwa kushirikiana na wanavijiji wamejenga matuta kuzuia maji kuvamia maeneo ya kilimo, akitolea mfano Kijiji cha Ndagoni kilichoko Chake Chake, Pemba.

Ni hatua zinazoungwa mkono na kupata ufafanuzi zaidi kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti Mazingira Zanzibar (ZEMA), Sheha Juma Mjaja anayebainisha kuwa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, mbali na kujenga matuta kuzuia maji ya bahari kuvamia maeneo ya kilimo na makazi ya watu, pia wanaijengea uwezo jamii ili iwe mlinzi wa miradi ya kukabiliana na athari hizo.

"Tunawapa elimu namna ya kuhifadhi na kulinda mazingira, jamii imekuwa na mwamko wa kulinda mazingira. Mkakati wetu ni kumshirikisha kila mtu ili kufahamu wajibu wao katika kulinda na kuhifadhi mazingira," anafafanua.

Mkurugenzi huyo anasema mkakati huo pia unawashirikisha wanawake kwa sababu ndiyo waathirika wakubwa wa mabadiliko ya tabianchi.

Mjaja anarejea takwimu za Umoja wa Mataifa (UN) za mwaka jana zinazoonesha takribani watu milioni 600 ulimwenguni wanaishi katika maeneo hatarishi ya bahari ambayo hayazidi mita 10 kutoka usawa wa bahari, miongoni mwao wakiwa ni wakazi wa Zanzibar.

"Ni wazi kuwa Zanzibar haijaweza kukabiliana ipasavyo na mabadiliko ya tabianchi na kuna haja ya kuchukua hatua za haraka ambazo zinaleta faida kubwa za kiuchumi katika kushughulikia kasoro za kukabiliana na hali iliyopo," anasisitiza.

Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa Zanzibar ina maeneo 148 yaliyoathirika kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Kati yake, 23 yako Unguja na 125 yako Pemba 125, shida kuu ikiwa kuongezeka kina cha maji ya bahari ambayo yamevamia makazi ya asili ya watu na shughuli za kijamii.

Kwa mujibu wa utafiti wa athari za mabadiliko ya tabianchi kwa uchumi wa Zanzibar wa mwaka 2012 uliofanywa na serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID), gharama za ziada zinazohusiana na athari za tabianchi dhidi ya afya Zanzibar, zinaweza kupanda hadi dola milioni 900 ifikapo mwaka 2030, ambao ni ukomo wa upimaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Omar Dadi Shajak, anasema serikali imeandaa mikakati ya kupata fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Mabadiliko ya tabianchi yanaathiri Zanzibar kutokana na kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari na mmomonyoko wa udongo maeneo ya pwani.

"Katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali imetenga Sh. bilioni 3.4 kwa ajili ya ujenzi wa kuta za kuzuia maji ya bahari na Sh. bilioni 1.1 kwa ajili ya upandaji mikoko.

Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) na ni miongoni mwa nchi zilizowasilisha mchango wake wa kukabiliana na athari hizo katika Sekretarieti ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi Julai 30, mwaka jana.

# Kiwewe maji kuvamia makazi ya watu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Kijiji cha Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja wako katika hatari ya kupoteza nyumba zao kutokana na maji ya bahari yanayojaa na kufika katika makazi yao.

Hali hiyo iliyozua taharuki kubwa, imejitokeza katika siku za karibuni huku sababu kubwa ikielezwa kuwa ni mabadiliko ya tabianchi.

Maji hayo yamevamia soko la samaki ambalo liko karibu na makazi ya wananchi huku wananchi wa kijiji hicho wakieleza kuwa kama hatua za haraka hazitachukuliwa, nyumba zao zitaathirika.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wananchi hao wameelezea hofu yao kuwa huenda wakawa katika matatizo ya kukosa makazi hata kupoteza maisha baadhi yao.

Asha Makame, mmoja wa wananchi wa kijiji hicho, alisema wamepata hofu kutokana na kasi ya maji ya bahari kupanda hali ambayo haijawahi kujitokeza katika miaka ya nyuma.

"Hali inatuogopesha kutokana na maji ya bahari kupanda na kutishia amani," alisema.

Alisema miaka saba ya nyuma bahari haikuwa karibu na makazi yao lakini kwa sasa hali imebadilika na kuwafanya kuishi kwa wasiwasi.

Katibu wa Kamati ya Wavuvi wa kijiji hicho, Khamis Hafidh Ali, alisema bahari imeshakula mita ishirini za eneo la nchi kavu yaliko makazi yao na kuomba serikali kutumia wataalamu kufanya utafiti na kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo lililojitokeza ili lisiendelee kuleta madhara.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Omar Dadi Shajaki, alisema Zanzibar ni kisiwa, hivyo imekuwa ya kwanza kuathirika hasa kutokana na hali inavyojitokeza duniani na matokeo yake maji kupanda katika nchi kavu.

Alisema serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, imetenga Sh. bilioni nne kwa ajili ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Shajaki alisema Zanzibar ina maeneo 143 ambayo yameathirika na mabadiliko ya tabianchi na yanahitaji uharaka wa kufanyiwa kazi ili kudhibiti maji ya bahari kuvamia makazi ya wananchi.

# January: Kampeni nishati safi haina lengo kuua ajira

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba (Pichani) amewaeleza Watanzania kampeni ya matumizi ya nishati safi ya kupikia hailengi kuondoa ajira kwa wauzaji wa nishati zisizo salama, bali itawapa fursa zaidi.

January aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipojibu hoja za washiriki wa mjadala wa kitaifa wa nishati safi ya kupikia uliofanyika kwa siku mbili na kuwakutanisha wadau mbalimbali wa nishati hizo wakiwamo wawakilishi wa nchi mbalimbali.

Alisema amesikiliza michango mbalimbali katika mdahalo huo, baadhi wakitoa hoja inayoaishiria kuwa kuanzishwa kwa kampeni hiyo kunalenga kuondoa ajira za wanaofanya biashara ya mkaa na kuni.

Alisema matumizi ya nishati safi ya kupikia haliwezi kwenda vizuri bila kuwapo sera, sheria, kanuni, mifumo na udhibiti wake na ndio matarajio ya serikali.

Waziri huyo alisisitiza kuwa serikali haina nia ya kuondoa ajira na kwamba watapata ajira nadhifu zaidi kuliko kukata au kuchoma mkaa.

"Kuna fursa nyingi za ajira katika nishati safi ya kupikia kuliko kukata miti na misitu ambayo ni rasilimali ya Taifa katika maendeleo," alisema.

January alisema katika kulipatia ufumbuzi suala hilo ndiyo sababu ya kuwapo kwa mjadala huo wa kitaifa na zipo nchi zilizofanikiwa, akizitaja India na Rwanda.

Alibainisha kuwa ili mtu apate tani moja ya mkaa, lazima akate miti tani saba, akisisitiza kuwa ni matarajio ya serikali kwamba mjadala huo utakuja na ufumbuzi wa namna ya kuandaa sera, mikakati, kanuni na mifumo ya namna bora ya kutumia nishati safi ya kupikia kama Rais Samia.



Akichangia mada ya namna wanawake wenye ushawishi wanaweza kuhamasisha msukumo wa kisiasa wa kuweka nishati safi ya kupikia, Getrude Mongela alisema kwa kuwa nchi imeshafanya mengi, suala la kuondoka katika nishati isiyo salama litafanikiwa.

Waziri mstaafu, Prof. Anna Tibaijuka alisema kuwa kwa sababu wameamua kupika kwa nishati safi, kunahitajika utashi huku Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Envirocare, Loyce Lema alisema elimu ya sera inahitajika kwa wananchi hususan wanawake ambao ndio wanatafuta maji, kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia na kutunza mazingira.

Katika mjadala huo, washiriki walibainish elimu ya sera inahitajika kwa Watanzania kuelekea matumizi ya nishati safi ya kupikia hususani kwa wanawake ili kujiepusha na magonjwa yanayosabishwa na nishati zisizo salama.

Juzi Rais Samia wakati akifungua mjadala huo wa kitaifa, aliagiza kuundwa kwa kikosi kazi kitakachojadili na kupitia sera za serikali na kuja na afua zitakazowezesha Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia.



# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Uamuzi kuwapeleka madereva wodi za majeruhi funzo kubwa

**AJALI** za barabarani zimekuwa zikiripotiwa mara kwa mara katika vyombo vya habari kwenye maeneo mbalimbali nchini. Kwa sasa hakuna mkoa ambao haujakumbwa na tatizo hilo kwa kuwa kila wakati matukio hayo yanaripotiwa katika vyombo vya habari.

Kwa ujumla, ajali hizo zimekuwa zikisababisha baadhi ya watu kupoteza maisha na wengine kujeruhiwa au kupata ulemavu wa kudumu. Baadhi ya sababu ambazo zimekuwa zikitajwa kuwa chanzo cha ajali hizo ni mwendokasi unaosababishwa na madereva, kukosekana kwa umakini wakati wa uendeshaji wa vyombo vya moto, hitilafu au kasoro katika magari na matumzi ya vileo kwa baadhi yao madereva. Kutokana na ongezeko la ajali hizo, serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali zikiwamo kuagiza madereva wanaosababisha ajali kuchukuliwa hatua za kisheria, kufutiwa leseni na kufumua uongozi wa kikosi cha usalama barabarani ambacho ndicho chenye dhamana ya kuhakikisha ajali zinadhibitiwa.

Hivi karibuni, kwa mfano, Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, alifanya mabadiliko ya makamanda wa jeshi hilo makao makuu na mikoa ambayo pia yalikigusa kikosi hicho. Aliyekuwa Mkuu wa Kikosi hicho, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mtafungwa, aliondolewa na kwenda kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza na aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Ramadhani Ng'anzi, kupewa wadhifa huo.

Mabadiliko hayo ndani ya trafiki, yameongeza chachu zaidi katika utendaji wa kikosi hicho kutokana na baadhi ya wakuu katika mikoa, kuonekana wakichukua hatua mbalimbali katika kupambana na madereva wanaosababisha ajali ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu. Mmoja wa wakuu hao ni yule wa mkoa wa Iringa, Mrakibu (SP) Mossi Ndozero, ambaye wiki iliyopita, kikosi chake kiliwapeleka madereva wa mabasi makubwa waliokamatwa kwa makosa mbalimbali ya usalama barabarani katika wodi za majeruhi wa ajali kuona wanavyoteseka kutokana na uzembe unaofanywa na baadhi yao. Madereva waliopelekwa katika wodi hizo ni wale waliokamatwa na wengine kufutiwa leseni kwa makosa mbalimbali ikiwamo kuendesha kwa mwendokasi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ndozero alisema waliamua kufanya hivyo ili madereva hao wajionee namna majeruhi wanavyoteseka kutokana na ajali za barabarani. Alisema madereva hao walipelekwa katika wodi za wanaume na wanawake za majeruhi hao ikiwa sehemu ya mafunzo kwa kundi hilo.

Kwa jumla, uamuzi wa kuwapeleka madereva hao ulikuwa mzuri kwa sababu wengi wao, pindi ajali zinapotokea wamekuwa wakikimbia na kuwatelekeza abiria na magari, hivyo kushindwa kutambua ni namna gani waathirika wanateseka.


Ni uamuzi wa kuungwa mkono pia mfano wa kuigwa kwa sababu madereva hao wamejionea kwa macho yao ni jinsi gani ajali zinavyosababisha matatizo mbalimbali vikiwamo vifo na majeraha. Pia wamejionea madhila wanayoyapata watu ikiwamo kupoteza muda wa kuzalisha kwa sababu ya matibabu au kuuguza ndugu zao.

Uamuzi huo pia unaonekana ni mzuri kwa sababu utakuwa umewapa mwanga madereva hao kwamba wana dhamana kubwa ya kulinda uhai wa watu, hususani abiria wanaopanda kwenye vyombo vya moto wanavyoviendesha.

Licha ya uamuzi huo, baadhi ya watu walisema madereva hao wangepelekwa kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti ili waonyeshwe watu waliopoteza maisha kutokana na ajali. Lakini itoshe tu kusema kupelekwa katika wodi hizo ni funzo kubwa kwao ili kutambua maumivu wanayoyapa waathirika wa ajali za barabarani zinazochangiwa kwa kiasi kikubwa na madereva hao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






# Muungwana Lazima Nilonge

## Simulizi hii iwe funzo kwa watoto wengine

Na Halfani Chusi

**SIKU** ya mtoto wa Afrika, iliyoandaliwa na Taasisi ya Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), kupitia kampeni ya 'Safari salama bila rushwa ya ngono'

Ilikuwa ya kipekee kutokana na simulizi ya Mtoto Elizabeth Sagati, ambaye alisimulia mapito aliyopitia katika masomo yake mpaka kumaliza shahada ya uzamili akisomea uandishi wa habari na mawasiliano kwa umma

Taasisi hiyo inayodhaminiwa na Women Fund Tanzania (WFT), iliandaa kongamano lililowakutanisha watoto zaidi ya 781, wazazi na walezi 143 ambao walifunzwa namna ya kutumia teknolojia kupinga ukatili na rushwa ya ngono.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali akiwamo Ofisa kutoka Idara ya maendeleo ya jamii Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, John Deogratius.

Katika kongamano hilo kitu kilichovuta taswira na kukonga mioyo ya watu ni simulizi ya Elizabeth Sagati, kama ilivyokaririwa na mwandishi wa makala haya akitamka:

"Mimi ni Mmasai, nimepitia magumu sana katika maisha yangu, kwa sasa mimi ni mwanafunzi katika chuo cha Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia, lakini hapo nyuma nilisoma uandishi wa habari na mawasiliano kwa umma, mpaka kufika leo hii ni kwa neema ya Mungu kwa sababu nimepitia magumu mengi."

Katika familia yake, anasema ni mtoto wa pili kuzaliwa upande wa mama, lakini kwa baba wako wengi, akiwa amesoma darasa la kwanza mpaka la saba na baada ya kumaliza, baba yake akataka kumuozesha akiwa na miaka 12, lakini mama hakukubali.

Kwa hiyo mama huyo akampa ujumbe huo, lakini yeye alikataa kushirikiana naye, yeye akisema hataki kuolewa anahitaji kusoma ili atimize ndoto zake, huku mama akimsihi bora akubali tu kwani angemfarakanisha na baba yake, wakashindwa kuelewana.

Mtoto anasema akasimamia hoja, heri iwe hivyo, lakini abaki anasoma.

Anasema, wakakimbizana na baba yake, hivyo mpaka akafanikiwa kwenda shule, kitu ambacho anashukuru zaidi walikuja wafadhili kutoka Finland, wanaojihusisha na kuwasomesha watoto wa kimasai katika mazingira magumu.

Katika hao naye akawa mmoja wapo, wakamchukua akaanza kusoma wakati anasoma kidato cha kwanza hakurudi likizo nyumbani, kwa sababu kulikuwa na hofu akirudi wangemlazimisha aolewe. Kwa hiyo, lile shirika likamtafutia makazi mjini Morogoro, shule ikifunga akawa anaenda kupumzika hapo, bila ya kwenda nyumbani maana ikafika ajenda ni lazima aolewe.

Eliza akaendelea kusimulia kuwa nilipomaliza kidato cha pili, kwa kuwa likizo ilikuwa ndefu nikasema ngoja niende nyumbani nikasalimie wazazi ndugu jamaa na marafiki, nilivyofika tu nyumbani wakanikamata wakanipeleka wakaenda kunificha huko wanakokujua wenyewe ili nisirudi shule niolewe wakaniwekea mdada wa kazi akawa ananihudumia.

Yule dada kwa sababu alishapewa mikakati asinipe simu lakini niliendelea kumlaghai baadaye akanipa nikampigia matroni wa shuleni nilikokuwa nasoma nikamueleza hali halisi ya kilichonikuta baada ya kwenda nyumbani kusalimia.

Akachukua timu ya Askari, wakaja mpaka nyumbani kipindi hicho wenzangu shule wanaendelea kusoma nikarudishwa shule na baba yangu akapewa onyo asirudie tena.

Nilipofika shule waliniambia wameshafanya usajili kwahiyo siwezi kuendelea na masomo labda nikae mpaka mwakani ndio nikajiunge tena ndio nitapata usajili na namba ya kufanyia mtihani kidato cha nne.

Kwa hiyo nyumbani nimekaa mwaka mmoja angekuwa ni mtoto mwingine angeshakata tamaa ya maisha na asingeendelea na masomo tena"

Aliendelea kuwa wakati huo tayari baba na mama yake walishatengana kupitia hilo baba alimwambia mama kwa sababu umekaidi amri yangu kakae huko peke yako na watoto wako

Baada ya kukaa huo mwaka mzima lile shirika likaniendeleza tena kielimu mpaka nikamaliza kidato cha nne, baada ya hapo nikaenda chuo cha uandishi wa habari Morogoro, nikasoma uandishi wa habari na mawasiliano kwa umma sasa nimemaliza na naendelea na masomo mengine.

## Hati za kimila 900 zakabidhiwa Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

HATI miliki za kimila 901 zilizoandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia mradi wa kurejesha ardhi iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kame nchini, zimekabidhiwa kwa wananchi wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida.

Kutolewa kwa hati hizo kunatarajia kumaliza tatizo la migogoro ya ardhi na kudhulumiana mashamba hususani kwa wanawake ambao idadi kubwa walikuwa wakikumbwa na kadhia hiyo.

Mratibu wa mradi wa kurejesha ardhi iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula nchini, Joseph Kihaule, alisema wananchi waliokabidhiwa hati hizo, hawatalipia kodi ya mwaka kama ilivyo kwa wananchi wa mijini.

Meneja wa Tume ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, Suzan Mapunda, alisema lengo la kutoa hati hizo ni kutaka vijiji viwe na mpangilio mzuri, kuondoa migogoro ya ardhi na kuongeza uzalishaji.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mkalama, James Nkwega, alisema wataweka mikakati ili upimaji ardhi na uandaaji wa hati miliki za kilima uwe endelevu kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi wilayani hapo.

Mmoja wa wananchi waliokabidhiwa hati hizo, Regina Rwenge, alisema kutolewa kwa hati hizo kutawafanya kuwa imara katika familia zao kwa kuwa wanawake walikuwa wakidhulumiwa haki zao za kumiliki ardhi.

Mwananchi mwingine, Fanuel Kaali alisema kupata hati hizo ni mkombozi mkubwa kwao kwa kuwa zitawasaidia hata kwenda kukopa fedha benki kwa ajili ya kuanzisha miradi ya maendeleo na hivyo kuinua uchumi wao.

## Uzalishaji wa maji Mbeya washuka

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKAZI wa Jiji la Mbeya wameanza kupatiwa huduma ya maji kwa mgawo kutokana na uzalishaji wa maji kutoka chanzo cha Mlima Mbeya kushuka kutoka lita 9,000 hadi lita 3,000 kwa siku.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya UWSSA) imesema hali hiyo imesababishwa na uharibifu wa mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) Mkoa wa Mbeya katika Kijiji cha Ihombe wilayani Mbeya, Ofisa Uhusiano wa mamlaka hiyo, John Nkana alisema uzalishaji wa maji katika chanzo hicho umeshuka kwa zaidi ya asilimia 75 na kusababisha baadhi ya maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Mbeya kukosa maji.

Aliyataja maeneo yaliyoathirika kwa kukosa au kupata maji kwa mgawo yanajumuisha vijiji vya Idugumbi, Ihombe na Mamlaka ya Mji Mgogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya pamoja na maeneo ya Iwambi, Itende na Iziwa katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Nkana alisem upungufu huo wa maji kwa kiwango kikubwa unasababishwa na shughuli za kibinamu zinazoendelea kufanyika kwenye vyanzo vya maji, hususan kilimo cha umwagiliaji kunachofanyika bila kuzingatia sheria.

Ofisa Mhifadhi Mkuu wa TFS Wilaya ya Mbeya, Eunice Mbilinyi alisema kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria za uhifadhi miongoni mwa wananchi wanaoingia bila kibali ndani ya hifadhi ya safu za Mlima Mbeya na kufanya shughuli za kibinadamu.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akikabidhiwa taarifa fupi ya usafishaji wa Mto Msimbazi na Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Kuratibu Usafishaji wa Mito na Mabonde Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Elizabeth Mshote, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Jafo akabidhiwa ripoti ya usafishaji Mto Msimbazi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo amepokea taarifa fupi ya usafishaji wa Mto Msimbazi kutokana na maelekezo aliyotoa hivi karibuni kwa Kikosi cha Kuratibu Usafishaji Mito na Mabonde Mkoa wa Dar es Salaam.

Taarifa hiyo iliwasilishwa kwa Waziri Jafo ofisini kwake jijini Dodoma jana na Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Kuratibu Usafishaji wa Mito na Mabonde Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Elizabeth Mshote. Hivi karibuni alifanya ziara ya kikazi ya kukagua mto huo katika Kata ya Mogo, Mtaa wa Kipawa baada ya kupokea malalamiko kuhusiana na athari za kimazingira zinazotokana na usafishaji wa mto huo.

Hata hivyo, wakati wa ziara hiyo, baada ya kusikiliza maoni ya wananchi alipata maoni yanayokinzana ambapo wengine walidai shughuli za usafishaji mto huo zimeleta athari kwa mazingira na wengine wakidai zimeleta manufaa makubwa kwa jamii inayozunguka eneo hilo. Itakumbukwa kuwa Februari 2021, Waziri Jafo, alikutana na wadau wanaojishughulisha na uchimbaji mchanga katika mkoa huo kujadili kero za kimazingira zinazotokana na uchimbaji mchanga kiholela katika mito na mabonde ili kuweka utaratibu mzuri.

Kikao hicho kiliwezesha kuandaliwa mwongozo wa usafishaji mito utakaotumika katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa lengo la kuondoa mchanga, taka ngumu na tope ili kupunguza au kuondoa madhara ya mafuriko ambao ulitolewa kwa mujibu wa kifungu cha 57 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

## KABWELA

**Fadhili Mohamed**






Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Khalfan Haule (kushoto), akipokea baadhi ya mifuko ya saruji 200 kutoka kwa Meneja wa Benki ya Azania tawi la Lamadi, Muhidin Mjuvi, iliyotolewa msaada na benki hiyo, kuchangia ujenzi wa madarasa matatu katika Shule ya Msingi Chanyauru B, wilayani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi ataja athari za mabadiliko ya tabianchi katika biashara, uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema wakati serikali zote mbili ya Tanzania na Zanzibar zinachukua hatua madhubuti za kukuza biashara na uwekezaji, inatambua kwamba maendeleo ya sekta hizo yana athari katika mabadiliko ya tabianchi.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa 26 wa sera na utafiti kuhusu biashara na mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Hoteli ya Golden Tulip, visiwani hapo ulioandaliwa na Taasisi ya Utafiti na Sera Tanzania (REPOA) na kufadhiliwa na Benki ya CRDB.

Dk. Mwinyi alisema mabadiliko ya hali ya hewa yanabadilisha na kupunguza mavuno ya mazao ya kilimo na uwezo wa uzalishaji wa uchumi wa taifa lolote.

"Tayari tunashuhudia hapa Tanzania; ambapo hali mbaya ya hewa inapunguza pato la kilimo, kiasi cha samaki wanaovuliwa, uzalishaji wa mwani na pia kumekuwa na vifo vya mara kwa mara vya mifugo kutokana na ukame," alisema.

Dk. Mwinyi alisema kwa upande mwingine, biashara ya kimataifa huathiri utoaji wa gesi chafuzi kwa njia tofauti na huzalisha hewa chafu kupitia uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma zinazouzwa.

Alisema biashara pia huongeza uzalishaji wa gesi chafu kupitia unyonyaji wa maliasili kama vile madini, mafuta, mbao na bidhaa za viwandani ambazo zinatumia nishati nyingi katika uzalishaji wake.

"Kwa kuzingatia uhusiano huu kati ya maendeleo ya biashara na athari zake katika mabadiliko ya hali ya hewa, tunahitaji kuchukua hatua kwa pamoja ili kuweza kubadilisha jinsi tunavyofanya biashara ndani na kati ya nchi zetu," alisema Dk. Mwinyi.

Pia alisema ni vyema kupunguza uzalishaji wa hewa chafu kwa ujumla, kwa kuchunguza mbinu za sera ambazo zinawezesha kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema ni imani yake kwamba kuna uwezekano wa kuongeza biashara na uwekezaji wakati huo huo kupunguza utoaji wa gesi.

Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari, alisema lengo la warsha hiyo ni kujadili masuala ya maendeleo ya nchi hasa ya mfungamano kati ya biashara, mabadiliko ya tabianchi na uchumi ambao ni endelevu.

Alisema, athari za mabadiliko ya tabia ya nchi yamezikumba nchi nyingi za Afrika zikiwamo Tanzania Bara na Zanzibar.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema mkutano huo utatoa mafunzo ya kweli ya kujua madhara ya mabadiliko ya tabianchi na kutumia fursa zilizoko katika eneo hilo.

Alisema huu ni muda wa kukabiliana na mabadiliko hayo kwa sababu bila ya kuutumia muda huo kuna uwezekano wa kupata changamoto zaidi baadaye.

## Mbunge abainisha vikwazo uwekezaji

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MBUNGE wa Njombe Mjini (CCM), Deodatus Mwanyika, amesema sheria kutotabirika na urasimu ndiyo sumu ya uwekezaji wa ndani na nje ya nchi na kushauri serikali kuja na kitu kitakachokidhi haja zao.

Hata hivyo, amepongeza uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza shughuli za uwekezaji nchini.

Akichangia bungeni Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 2022, mbunge huyo alisema: "Suala la kutotabirika kwa kiasi kikubwa tunaishukuru serikali tunatambua, ndiyo maana tuna blueprint, utekelezaji wake umeanza, tozo nyingi zimeondolewa katika tozo 300 zimebaki 114 zinashughulikiwa.

"Tumeona hata ukipewa cheti cha uwekezaji, bado unahangaika na taasisi na wakala za serikali zingine, tunashukuru wizara wamekubali maoni ya kamati, sasa cheti kitatoka ndani ya siku saba badala ya 14, ni maendeleo mazuri."

Alisema kuna umuhimu Kituo cha Uwekezaji (TIC) kuwa mamlaka kamili ili kusaidia kufanya uamuzi wenye tija.

"Pia busara itumike, tunahitaji sekta binafsi kwenye vyombo vingine vya uamuzi kwa ajili ya maslahi kwa taifa," mbunge huyo alishauri.

# Taasisi yajitosa kusaidia wasichana waishio katika mazingira hatarishi

**Na Beatrice Shayo**

TAASISI ya Mwanamke na Uongozi (MnU) imeanza kuwasaidia wasichana watano ambao wanaishi katika mazingira hatarishi wakiwamo waliopata ujauzito na kutelekezwa.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa MnU, Shamira Mshangama, wakati wa uzinduzi wa taasisi hiyo ambayo imewahusisha wanawake 50 ambao wanafanya kazi katika sekta mbalimbali.

Alisema wamezindua App iitwayo 'Anza na Ulicho Nacho' ambayo watakuwa wanaitumia katika kutoa elimu kwa ajili ya kuwainua wanawake kiuchumi.

Mshangama alisema lengo kuu ni kuwa na jamii ambayo imehamasika na kujua umuhimu wa kutoa sehemu ya mali au kipato chao kuboresha maisha ya wengine wenye uhitaji.

"Kwa kuhakikisha lengo kuu linafikiwa tumeona tuanze sisi kwanza kwa kuboresha maisha ya wasichana watano waliopata mimba katika umri mdogo na kutekelezwa na wazazi wenzao hali iliyosababisha kuwalea watoto wao katika umaskini," alisema.

Mshangama alisema taasisi hiyo ilianza mwaka 2017 na imewafikia zaidi ya wanawake 100,000 wa Tanzania katika miradi mbalimbali wanayofanya kwa kushirikiana na serikali, kampuni binafsi, taasisi za kijamii na wadau wa maendeleo kwa lengo la kubadilisha maisha yao na kutatua changamoto za kimaisha zinazowakabili.

Aidha, alisema wanawake ni wachangaji wazuri katika vikundi mbalimbali na hata katika sherehe hivyo wameona ni vizuri kuwasaidia wasichana hao ambao wanapitia matatizo.

"Bado kuna wanawake wengine wanaoishi katika mazingira magumu ya kimaisha bila kupata msaada wako ambao hata pesa ya kula mlo mmoja wa siku, wapo ambao hawana nguo kwa ajili ya watoto wao," alisema.

Alisema hali ya kuwa na tabaka kwa wanawake wahitaji na wanawake wahisani ndio iliyosababisha MnU kuona haja ya kuunda mtandao huo ambao wanaenda kuwa daraja kata ya wanawake hao.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya kutengeneza na uuzaji wa vipodozi vya asili ya Brembo, Asnat Masudi, alisema wanawake wengi wanapitia changamoto nyingi ni muhimu kushirikiana nao ili kufikia malengo yao.

Alisema wanaamini wanawake wakishirikiana kwa pamoja watafanikiwa katika kuwasaidia wasichana hao ambao wanapitia mazingira magumu.

HABARI KITAIFA

# Waomba hatua za dharura kudhibiti tembo Same

**Na Maulid Mmbaga**

WANANCHI wilayani Same wameililia serikali kuchukua hatua za haraka kutatua tatizo la tembo wanaoonekana kuzagaa katika makazi yao na kuhatarisha usalama wao.

Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha ukame katika hifadhi za wanyama na kufanya tembo kutembea maeneo mbalimbali kutafuta malisho na maji kupitia shoroba ambazo sasa zimekuwa makazi ya watu.

Akizungumza na Nipashe jana, Saida Simba mkazi wa Kitongoji cha Makei, wilayani Same, alisema wanyama hao wamesababisha hofu kwa watoto wanaotembea wakati wa kwenda shule na wakati mwingine wanashindwa kuhudhuria masomo kutokana na kuhofia wanyama hao.

Alisema tembo hao wameibua hofu kubwa pia kwa wanawake wanaotembea zaidi ya kilomita nane kwenda kutafuta maji na wakati mwingine wakilazimika kuchelewa kurejea nyumbani wakisubiri tembo waondoke katika eneo wanakotakiwa kupita.

"Tatizo la hawa wanyama katika eneo hili limekuwa kubwa na la muda mrefu, wakati mwingine watoto wanarudi nyumbani wanakuambia wamewaona tembo wakiwa wanakwenda shule hii inahatarisha usalama wao," alisema na kuongeza:

"Jana pia kuna wanawake walikuwa wanatoka sokoni walishindwa kwenda nyumbani kwasababu tembo walikuwa barabarani, walilazimika kutumia njia nyingine ambayo inamzunguko mkubwa, hadi saa 02:00 usiku walikuwa hawajafika nyumbani, ukizingatia mazingira ya huku kutembea usiku sio salama hasa kwa sisi wanawake," alisema Saida.

Charles Athumani kiongozi wa eneo hilo, alisema wanyama hao wamekuwa wakiwasumbua kwa zaidi ya mwaka sasa, tatizo hilo walishalipeleka ngazi ya wilaya lakini bado halijapatiwa ufumbuzi.

"Tembo hawa wanasababisha matatizo kwa wananchi, lakini sisi tukiwagusa ni tatizo hii haiko sawa, inaonekana kama mnyama ana thamani kuliko binadamu," alisema Athumani.

Naye Mwenyekiti wa Kitongoji cha Masandare, wilayani hapo, Bakari Ramadhani, alisema mwaka uliopita wanyama hao waliharibu mazao ya watu, lakini fidia wanayolipwa haiendani na thamani ya kilichoharibiwa.

"Hapa kwetu pamoja na ukame uliopo lakini hata mvua ikinyesha tatizo kubwa linalotusumbua ni tembo, hata ukifika hapa jioni sio ajabu ukiona wanyama hao wako hapo nje, wamekuwa wasumbufu ukimuona huwezi kutoka nje inabidi ukae ndani hadi waondoke.

"Tulipeleka malalamiko katika uongozi wa wilaya na tukateuwa vijana ili wapatiwe mafunzo ya namna ya kuwafukuza hawa tembo, lakini mara ya mwisho tulivyoenda tuliambiwa kwamba hawana fedha za kuendesha suala hilo," alisema Ramadhani.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo, alisema halmashauri wamefanya jitihada mbalimbali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA) ikiwamo kuandaa kikosi kazi na kukipatia elimu watakayokwenda kuitoa kwa wananchi, ambayo itawapa mbinu ya kuwafukuza wanyama hao pindi watakapowaona katika makazi yao.

"Uchache wa mvua katika eneo letu umesababisha uhaba wa maji katika hifadhi, jambo linalosababisha tembo wengi kutoka kwenye mapori yao na kwenda kutafuta maji, hali inayowapeleka hadi katika makazi ya watu," alisema Mpogolo. Aidha, alieleza kwamba TANAPA wamechukua hatua ya kuchimba mabwawa pamoja na visima vya maji hifadhini ikiwa ni moja ya jitihada za kuongeza maji ili kuzuia wanyama hao wasitoke nje ya eneo la hifadhi.

"Uwapo wa tembo wengi katika maeneo ya watu limekuwa ni tatizo kwasababu wanaathiri watu. Shirika linalojihusisha na wanyamapori (WWF) wamekuwa wakitoa msaada na tunashirikiana nao kutoa elimu kwa jamii namna ya kuwafukuza wanyama hao," alisema Mpogolo.

"Tulizungumza na wenzetu TANAPA tukawasisitiza kwamba wachimbe mabwawa makubwa ambayo yatakuwa na uwezo wa kuhifadhi maji kwa muda mrefu ili kutatua tatizo hilo," alisema Mpogolo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (wa tatu kulia), pamoja na viongozi wengine waandamizi wa benki hiyo wakijipongeza, baada ya kuzindua hati fungani (bondi) inayofahamika "NBC Twiga Bond" ya miaka mitano yenye thamani ya Sh. bilioni 30, jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya kupanua uwezeshaji (mikopo) wa bei nafuu kwa wafanyabiashara wadogo, kati na sekta ndogo za kilimo nchini. Kulia ni Mwakilishi wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Brighton Kinemo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tz kushiriki mkutano kimataifa mabadiliko ya tabianchi Misri

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA inatarajia kushiriki mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi nchini Misri, pamoja na mambo mengine itaweka msimamo katika mambo nane ikiwamo upunguzaji wa uzalishaji wa gesijoto duniani.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu msimamo wa Tanzania kwenye majadiliano yatakayokwenda kufanyika katika mkutano huo.

Jafo alisema katika mkutano huo Tanzania inakwenda kuweka msimamo katika suala la malengo ya dunia katika uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

Alitaja maeneo mengine ni hatua wezeshi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, hasara na uharibifu unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, upunguzaji wa gesijoto.

Maeneo mengine ni masoko ya kaboni na mbinu zisizo na masoko, mfumo wa uwazi katika hatua na misaada inayotolewa pamoja na madhara ya hatua za kisera za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Jafo alisema mkutano huo unatarajiwa kuhudhuriwa na wajumbe wapatao 35,000 kutoka nchi mbalimbali wakiwamo wakuu wa nchi, mawaziri na wataalamu waliobobea katika mabadiliko ya tabianchi, taasisi za kifedha, vyombo vya habari, wanasiasa, makundi maalum, wafanyabiashara na wanaharakati wa mazingira.

"Mwaka jana Tanzania ilishiriki katika mkutano huu ambao ulikuwa ni wa 26 nchini Uingereza, ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alitoa hotuba na kushiriki mikutano iliyofikia maamuzi muhimu ya mustakabali wa dunia na nchi yetu."

Jafo alisema kwa mwaka huu Tanzania imedhamiria kushiriki kitofauti kwamba kutaandaliwa banda la maonyesho ambalo litakuwa na shughuli ya kuitangaza Tanzania mafanikio yaliyopatikana katika sekta mbalimbali.

## Wananchi watahadharishwa kuwekeza fedha taasisi zisizoaminika

**Na Beatrice Moses**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewatahadharisha wananchi kuwa makini kwa kuepuka kuwekeza fedha zao kwenye taasisi au vikundi vya fedha visivyoaminika.

Waziri Ndejembi aliwahamasisha wananchi kujiunga na kutumia mifuko rasmi ya uwekezaji ya serikali ili kuepuka kukumbana na matukio ya kutapeliwa.

Alisema hayo jana Dar es Salaam wakati alipokuwa akizindua mauzo ya vipande vya mfuko wa uwekezaji wa pamoja 'Faida Fund' uliopo chini ya Kampuni ya Watumishi Housing Investment (WHI).

"Hivi karibuni tumeshuhudia wawekezaji wengi wenye nia nzuri wakitapeliwa fedha zao na baadhi ya watu wasio waaminifu, ninafurahi kuona kwamba Mfuko wa Faida una mfumo inayomhahakikishia mwekezaji usalama na uhakika kwa fedha anayoweka itampa faida," alisema.

Alisema malalamiko ya utapeli kupitia mitandao inatokana na wengi kufanya uwekezaji usio salama kupitia upatu mfumo ambao haueleweki na usio rasmi, na kuwa rahisi kutapeliwa.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa WHI, Dk. Fred Msemwa, alisema kuanzishwa kwa Faida Fund ni kuziba uwazi kwenye baadhi ya mifuko iliyopo ambao umesababisha watu wa kipato cha kati na chini kukwama kujiunga.

"Faida Fund ni mfuko wenye lengo la kukuza mtaji wa wawekezaji kupitia uwekezaji wa pamoja, wakulima, mamalishe, bodaboda, wafanyabiashara, watumishi wa umma na wa sekta binafsi Watanzania ndani na nje ya nchi ndiyo walengwa," alisema.

Kadhalika, alisema Faida Fund inatoa fursa kwa makundi yasiyo rasmi katika uwekezaji kujiunga kupitia katika hati fungani za serikali ambao awali ulikua ukitumika na watu wenye vipato vya kati na juu.

Mfumo wa uwekezaji wa Faida Fund umebuniwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (EGA), ambao unatajwa kusaidia kuwa na gharama ndogo za uendeshaji na kufungua fursa ya kupata faida itakayowezesha kupatikana kwa gawio zuri kwa wawekezaji husika.

# ‘Serikali haikutoa fidia, ilitoa kifuta machozi’

BUNGE limeelezwa kuwa serikali ilitoa mkono wa pole na sio fidia kwa wananchi 12,647 walioathirika na milipuko ya mabomu iliyotokea Aprili 29, mwaka 2009 katika kambi ya JWTZ Mbagala na Sh. bilioni 17.4 zilitumika.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alieleza hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Mbagala (CCM), Abdallah Chaurembo.

Mbunge huyo alihoji kauli ya serikali kuhusu mapunjo ya fidia kwa wananchi hao.

Simbachawene alisema malipo hayo yalitolewa kwa awamu sita kuanzia mwaka 2009 hadi 2020.

Vile vile, alisema serikali ilitoa kifuta machozi pamoja na kugharamia huduma za mazishi kwa familia 29 zilizopoteza wapendwa wao kutokana na milipuko hiyo.

“Zoezi la kutoa mkono wa pole kwa waathirika lilisitishwa rasmi na serikali mnamo mwezi Machi 2020 baada ya walengwa wote waliokusudiwa kujitokeza na kulipwa,” alisema.

Katika swali lake la nyongeza, Mbunge huyo alihoji serikali haioni haja ya kutoa ufafanuzi kwa wananchi hao ya tofauti kati ya fidia na kifuta machozi.

“Kutokana na malalamiko kuwa mengi ya wananchi hao, waziri utakuwa tayari kwenda kusikiliza malalamiko yao na kupatia majibu,” alisema.

Waziri Simbachawene alisema yupo tayari kuwasikiliza wananchi hao na alipata fursa ya kukutana na baadhi yao kwa niaba yake walikutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, waliwasilisha barua.

“Maafa yanasababishwa na majanga na majanga huwa si jambo lililopangwa au kutarajiwa, yanapotokea maafa huwezi kuweka utaratibu wa kulipa fidia, hutolewa kifuta machozi kwa walioathirika na serikali ilifanya hivyo kulipa kifuta machozi ambapo kiasi cha Sh. bilioni 17.4 zilitumika ni fedha nyingi na serikali ilishughulikia mazishi,” alisema.



Watoto wenye usonji kutoka mikoa mbalimbali nchini wakiwa na wazazi wao, wakitambulishwa Bungeni, jijini Dodoma jana, walipofika kujifunza shughuli za Bunge kwa kuwezeshwa na Shirika la Living Together Autistic Foundation (Li TAFO). **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yaeleza sababu upungufu uzalishaji umeme

SERIKALI imesema kuna upungufu wa vyanzo vya uzalishaji wa umeme hususani kwenye maji ambapo megawati 190 hazipatikani kama ilivyotarajiwa.

Kutokana na hali hiyo, imesababisha baadhi ya maeneo kukatika umeme au kupewa kwa mgawo huku akitaja mipango ya serikali ambapo kabla ya mwezi Desemba kuisha mradi wa Kinyerezi I extension utakaotoa megawati 185 uwe umekamilika ili kuondoa tatizo hilo.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, aliyasema hayo jana bungeni baada ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kutaka atoe ufafanuzi wa serikali kwa ujumla kwenye maeneo ambayo yamepelekewa umeme na kutokea tatizo la kukatika mara kwa mara.

Byabato alisema pia serikali imetenga Sh. bilioni 500 kwa ajili ya kuimarisha Gridi ya Taifa na Sh. bilioni 300 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu mingine ili umeme usikatike mara kwa mara.

“Tuna uhakika tunapoelekea kumaliza mwaka huu majibu ya haraka yatapatikana na tunapomaliza mwaka wa fedha 2022/23 majibu makubwa ya muda mrefu yatapatikana ili kuondokana na tatizo la kukatika kwa umeme,” alisema. Hata hivyo, baada ya ufafanuzi huo, Spika Tulia alitaka watazame maeneo ya kipaumbele kama afya, elimu na biashara umeme uwepo ili kuwapunguzia gharama ya matumizi ya majenereta.

“Mameneja wa mikoa waangalie maeneo fulani ya kutoa kipaumbele na yanahitaji umeme kwa wakati hasa ya biashara,” alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Ndanda (CCM), Cecil Mwambe, alihoji mkakati wa serikali kuhakikisha kuwa inamaliza kero ya kukatika kwa umeme mara kwa mara kwenye Mikoa ya Kusini hasa Wilaya ya Masasi na vijiji vyake.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Byabato, alisema hali ya upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Mtwara imeendelea kuimarika na kuwa ya kuridhisha ikilinganishwa na kipindi cha nyuma na serikali ina mkakati wa dhati wa kumaliza kero hiyo kwa mikoa ya Kusini na Tanzania nzima.

“Ili kuondoa changamoto hii serikali imetenga Sh. milioni 600 kwa ajili ya kurekebisha miundombinu katika laini za Newala, Nyangao, Masasi na Mahuta. Aidha, Sh. bilioni 2.2 zimetengwa kwa ajili ya kujenga njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 kutoka Nanganga hadi Masasi,” alisema.

Katika mpango wa kudumu wa kuimarisha Gridi ya Taifa, alisema serikali imetenga Sh. bilioni 250 kujenga Gridi ya Taifa kutoka Songea - Tunduru hadi Masasi na kwa mwaka 2022/2023 imetenga Sh. bilioni 66.7 kuanza ujenzi wa njia hiyo.

## Mbunge aeleza hofu watoto chini miaka 5 kuugua kisukari

MBUNGE wa Mtoni (CCM), Idrissa Juma Abdulhafar, amesema kumekuwapo na ongezeko la watoto chini ya miaka mitano kuugua kisukari na saratani na kuitaka serikali kuwa na mkakati wa kuhudumia kwa asilimia 100 matibabu ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa watoto wote chini ya miaka 18.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alihoji pia serikali ina mpango gani wa kupambana na visababishi vya maradhi yasiyoambukiza.

Naibu Waziri wa Afya, Dk.Godwin Mollel, alisema suala la kuhudumia watoto chini ya miaka mitano kwa mujibu wa utaratibu wanapaswa kupata matibabu bure.

“Kumekuwa na changamoto wanahitaji huduma, lakini baadhi ya dawa zinakosekana, kweli kuna mzigo mkubwa wa gharama ndio maana tunaleta muswada wa bima ya afya kwa wote wenye lengo la kupelekea matatizo hayo yasuluhishwe,” alisema.

Kadhalika, alisema katika mwaka wa fedha 2022/2023 serikali imetenga Sh. milioni 725 kwa ajili ya kutekeleza Mpango Mkakati wa Tatu wa Kitaifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza, 2021 - 2026.

Alisema mpango umeainisha mikakati mahsusi ya udhibiti wa visababishi vya magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo, kuimarisha uratibu na ushirikishwaji wa sekta mtambuka, miundombinu ya utoaji wa huduma, kuwajengea uwezo watumishi katika kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza, kuimarisha na kusimamia shughuli za utafiti pamoja na kuhamasisha wananchi kuhusu njia za kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.

Pia alisema njia hizo ni pamoja na kufanya mazoezi, pamoja na kuzingatia kanuni bora za lishe.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Maryam Azan Mwinyi, alihoji serikali inasaidiaje wananchi kwenye gharama za magonjwa hayo.

Naibu Waziri Mollel, alisema kwa mwaka mmoja serikali inatumia Sh.bilioni 670 ambapo kati ya fedha hizo zingine zinaelekezwa kusaidia watu wenye magonjwa hayo.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA



# Mongela akiagiza Chuo ATC kufundisha ubunifu

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, ameuagiza uongozi wa Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), kujikita zaidi na utoaji wa mafunzo kwa njia ya vitendo, ubunifu, uvumbuzi na ugunduzi.

Mongela alitoa agizo hilo jana jijini hapo, wakati akiweka jiwe la msingi katika hospitali ya mafunzo ya kufundishia na tiba inayoendelea kujengwa na ATC.

Alisema chuo hicho, kimetoa mchango kwa nchi kwa kuwa kimezalisha wataalamu ambao ndio watendaji kazi na endapo watazingatia mambo hayo, watajitangaza na kupata soko ndani na nje ya nchi kwa mafunzo wanayofundisha wanafunzi.

Alisema kimekuwa kinaaminika kwa kuwa ufundishaji wake ni wa vitendo zaidi kuliko nadharia na kuutaka uongozi kuongeza kasi na kuzingatia mambo hayo.

"Rai yangu chuo hiki, kijikite zaidi kufundisha watu kwa vitendo, ugunduzi, uvumbuzi ufanyike na utoaji wa masuluhisho ya matatizo yanayowakabili wananchi kwa kusaidia kwa kuwa dunia ya sasa imejikita huko," alisema Mongela.

Alisema kwa sasa Tanzania ina uhitaji wa watu wabobezi kwenye masuala ya teknolojia ya kidigitali na kielektroniki kwa kuwa nyakati hizi ni za mapinduzi ya viwanda na kuna mahitaji ya wataalamu hao.

"Sisi tunaamini ATC mko kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuibeba nchi yetu, katika sekta ya utaalamu wa ufundi kwa vitendo kwa kuwa teknolojia inakwenda kasi mno," alisema.

Mkuu wa Chuo cha Ufundi cha Arusha, Musa Chacha, alisema katika utoaji wa mafunzo na kuboresha elimu, chuo hicho kwa kutumia mapato yake ya ndani walitenga Sh. bilioni 1.38 ili kutekeleza mradi huo.

Alisema ujenzi wa mradi umetumia mafundi jamii 'Force Acount' kupitia kitengo cha ndani cha ushauri na kamati tatu ziliundwa kwa ajili ya usimamizi.

Kadhalika, alisema mradi umefikia hatua nzuri kukamilika na hadi sasa Sh. bilioni 1.06 zimeshatumika na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Novemba, mwaka huu.

Vilevile, alisema hospitali hiyo, inatarajia kutoa huduma kwa wagonjwa 100 hadi 300 kwa siku na itahudumia wanafunzi, wafanyakazi wa chuoni hapo na wananchi kwa ujumla.

Alisema kwa kuanza itatoa huduma za uchunguzi wa afya ya mama na mtoto, magonjwa ya macho, mfumo wa pua, masikio, meno na magonjwa ya ndani yakiwamo ya upasuaji, utoaji wa dawa na vifaa tiba.




Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Mafunzo na Tiba ya Chuo cha Ufundi cha Arusha (ATC), Faraji Magania (kulia), baada ya kuweka jiwe la msingi la mradi huo, jijini Arusha jana. Wa pili kulia ni Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Musa Chacha. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Songe yakusanya mapato mil. 9.4/- kwa miezi sita

**Na Dege Masoli, KILINDI**

SERIKALI ya Kijiji cha Songe, Kata ya Songe, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga, kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Aprili hadi Septemba mwaka huu, imekusanya zaidi ya Sh. milioni 9.4.

Akisoma taarifa ya mapato na matumizi katika mkutano wa hadhara, Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Joyce Ikungu, alisema fedha hizo, zimetokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani.

Alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 4.029 zimetumika kutekeleza miradi ya kijamii ikiwamo ya shule mpya shikizi.

"Kwa sasa hivi fedha za kijiji zilizobaki benki kwenye akaunti ni Sh. milioni 5.425 baada ya kutoa kiasi kingine kwa ajili ya kwenda kufanya ujenzi kwenye mradi wa shule shikizi," alisema.

Mwenyekiti wa serikali ya kijiji hicho, Ibrahim Goda, alitaja baadhi ya miradi iliyofanikisha kukusanya kiasi hicho cha fedha kuwa ni pamoja na faini walizotozwa waharibifu wa mazingira.

"Tumesimamia vyema utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji na kila aliyefanya uharibifu katika maeneo hayo, tumekuwa wakali na kuwatoza faini na imesaidia kuendeleza miradi yetu ya maendeleo," alieleza Goda.

Diwani wa Kata ya Songe, Mohamed Makengwa, alisisitiza suala la uharibifu wa mazingira ikiwamo kupiga marufuku kulima maeneo ya milima, hifadhi na vyanzo, kwamba licha ya kupigwa faini wanaweza kutumikia kifungo.

# Askofu ataka Watanzania kufunga kuomba mvua

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Gombo la Chuo, Daniel Methew, amewataka Watanzania kufunga na kumwomba Mungu ili kuwanusuru na adha ya kukosekana kwa mvua inayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi na kusababisha ukame.

Kiongozi huyo wa kanisa hilo katika mji mdogo wa Ngaramtoni, wilayani Arumeru, alisema hayo jana wakati alipokuwa akisimikwa kuwa askofu wa kanisa hilo, kuzindua kanisa na kitabu chake.

Alisema kutokana na hali ya ukame kwa kipindi hiki, kuna umuhimu kwa kila mwananchi kufanya maombi kwa imani yake ili kunusuru hali hiyo.

Alisema wataalamu wanadai kuwa hali hiyo, imetokana na uharibifu wa mazingira unaofanywa na watu wenyewe kwa kukata miti ovyo na kunasababisha mvua kutokunyesha kwa wakati.

"Naweza kusema kuna mambo mawili, kwanza uharibifu wa mazingira unaweza kutusababisha tusipate mvua kwa wakati, lakini jambo lingine maovu yetu kwa kuwa maandiko yanasema ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina langu wataomba, watalia, Mungu atawasikia na ataiponya nchi," alisema.

Alisema ni vyema Watanzania wakamtafuta Mungu ili awakumbuke na mvua kwa kuwa mifugo na watu wanakufa kwa njaa kwa kukosekana kwa mvua kwa muda mrefu.

Aliwataka wananchi kuendelea kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa amekuwa kiongozi msikivu na ambaye anawajali watu wake, bila ya kujali itikadi za vyama vyao, pia ni kiongozi wa kuwatia moyo wachungaji.

Mchungaji wa kanisa hilo, Pendo kileo, alisema ni vyema wananchi wakawa kwenye mikono salama ya kumjua kwa kuwa ataruhusu vitu vyote alivyovitengeneza hapa duniani.

Kadhalika alitaka kuendeleza upendo na mshikamano kwa lengo la kuijenga nchi ili kupiga hatua kimaendeleo na kiuchumi.

# TAKUKURU yadhibiti wagonjwa hewa 313 wa VVU

**Na Boniface Gideon,** TANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Tanga imefanikiwa kudhibiti wagonjwa hewa 313 wa VVU waliokuwa wamesajiliwa na wataalamu wa afya kwenye mfumo wa usajili wa wagonjwa hao wilayani Muheza.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tanga, Zainabu Bakari, wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2022, huku lengo la wahudumu hao wa afya kufanya usajili hewa likiwa ni kujipatia kipato kupitia malipo ya shirika linalosaidia kutoa elimu ya afya nchini.

Alisema TAKUKURU kupitia vyanzo vya siri ilibaini kuwa watoa huduma za afya wanaohusika na kusajiliwa watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi, wanafanya udanganyifu kwa kuwaingiza majina hewa ili kuonesha takwimu za wanaoishi na VVU kuonekana zipo juu kwa maslahi yao binafsi.

Alibainisha kuwa katika ufuatiliaji wao, mkoa ulibaini kuwa wahudumu wa afya wanaohusika na kuwasajili na kuwafuatilia wagonjwa wanaoishi na VVU wamekuwa wakilipwa posho ya gharama ya usafiri kupitia akaunti za simu za mawasiliano Sh. 20,000 kwa siku kila wanapotoka kwenda kuwatembelea wagonjwa hao.

Alisema fedha hizo hulipwa na Shirika la Utafiti wa Dawa Afrika (AMREF Tanzania) kwa kazi ya kufuatilia kila mgonjwa kwa lengo la kuhakikisha hali yake kiafya inaimarika kwa maana ya kutumia dawa kwa wakati na huduma nyingine zinazostahili.

Aidha, alisema fedha hizo hulipwa moja kwa moja kwa mhudumu husika kupitia namba yake ya simu ya mkononi na ndiyo sababu watumishi wasio waadilifu huweka takwimu hewa kwa lengo la kujiongezea posho.

Alisema katika ufuatiliaji uliofanywa na TAKUKURU kwa baadhi ya zahanati ilibainika kuwa kuna wagonjwa ambao sio halisi kwa maana ya upatikanaji wake na hivyo kufanya udhibiti wa kuchukua hatua.

Alisema hatua walizoanza kuchukua ni kufikisha kikao cha pamoja kati yao na ofisi ya Mganga Mkuu wa wilaya na watendaji wake wote wanaohusika na kuwahudumia watu wanaoishi na VVU pamoja na AMREF

"Katika kikao hicho TAKUKURU iliwasilisha yaliyobainika katika ukaguzi wa kutembelea jumla ya zahanati saba kati ya 16 zilizoko katika Wilaya ya Muheza na kubaini tatizo hilo," alisema.

Pia, taasisi hiyo mkoani hapa ilimwagiza Mganga Mkuu wa wilaya ya Muheza kufanya uhakiki wa takwimu za wagonjwa wote wanaoishi na VVU na kutoa taarifa ya uhakiki.

Alisema baada ya agizo hilo ilibainika kuwapo wagonjwa hewa 313 na idadi hiyo iliondolewa kwenye mfumo.

Pia alisema wahusika katika usajili wa wagonjwa hao hewa wamepewa barua za kujieleza kwa kitendo cha hicho cha udanganyifu. Taasisi hiyo inaendelea kuwasihi watumishi wote wa umma kufanya kazi kwa mujibu wa kanuni, taratibu, sheria iliyoko katika utekelezaji wa majukumu yao.



Diwani wa Kata ya Mtindiro, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Mustafa Hatibu (kushoto), akimtwisha ndoo ya maji Asha Hassani mwanafunzi wa darasa la nne Shule ya Msingi Kibaoni, wakati akikagua mradi wa maji uliofadhiliwa na Taasisi ya Islamic Help, katika kata hiyo jana. Visima zaidi ya 10 vimechimbwa kwenye kata hiyo na wafadhili mbalimbali. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Wamshukuru Rais kwa kupatiwa mashine ya X-ray

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, wamemshukuru Rais wa Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia mashine ya X-ray yenye thamani ya Sh. milioni 160 kwenye Kituo cha Afya cha Longoi kilichoko wilayani humo.

Kituo cha Afya Longoi, ni kipya katika Wilaya ya Hai ambacho kimejengwa kwa Sh. milioni 600 na fedha hizo zilitolewa na serikali, awali halmashauri hiyo ilipokea Sh. milioni 400 kwa ajili ya kujenga majengo ya mwanzo na baadaye walipokea Sh. milioni 200 za kumalizia ujenzi.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani la halmashauri hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hai, Edmund Rutaraka, alisema mashine hiyo, itakwenda kuhudumia kata nne za wilaya hiyo, ikiwamo ya Weruweru, Rundugai, Mnadani na Masama Kusini kwa upande wa kwa Sadala ikiwa ni kilomita chache kwenda Longoi.

Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Dk. Etikija Msuya, alisema mashine hiyo, ni muhimu katika hospitali hiyo, kwa kuwa itasaidia kuyatambua magonjwa mbalimbali hasa yanayohusiana na mfumo wa upumuaji.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kutupatia mashine hii kwasababu itasaidia wananchi wote wanaoishi ukanda huu wa bondeni kwa kuwa huduma hii imesogea karibu na wananchi wa Masama Rundugai ambapo itanufaisha hadi kata za jirani."

# Wazazi wanaopokea posa kwa wanafunzi waliomaliza la 7, kidato cha 4 waonywa

**Na Dege Masoli,** KILINDI

OFISA Mtendaji wa Kata ya Songe, katika Tarafa ya Kwekivu, Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, Ramadhani Dhahabu, ametoa onyo kwa wazazi waliopokea posa na mahari kwa wanafunzi waliofanya mitihani ya kuhitimu darasa la saba na kidato cha nne mwaka huu, kabla ya matokeo kuwa watachukuliwa hatua za kisheria ikwamo kuburuzwa kortini.

Dhahabu, alitoa onyo hilo jana, kwenye mkutano wa hadhara wa Kijiji cha Kwamba, uliokuwa umelenga kusikiliza kero za wananchi na kutambulisha miradi iliyotekelezwa kwenye maeneo yao. Alisema kuna fununu ya kuwapo taarifa ya baadhi ya wazazi kupokea mahari kwa ajili ya watoto hao na kuwaonya wasithubutu watakumbana na mkono wa sheria.

"Kuna baadhi ya wazazi wameshakula mahari hata kabla ya matokeo kutoka ninasema hatutalivumilia kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amerahisisha mambo, sasa hivi elimu ni bure kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita kwa hiyo mzazi atakayemnyima mtoto kusoma hatakuwa salama kisheria," alisisitiza Dhahabu. Ofisa Elimu, Kata ya Songe, Bakari Mwanangoto, aliwataka wazazi kuhakikisha watoto wote, wanawaandikisha kuanza shule mwakani na kuwasimamia kwa kufuatilia mienendo yao shuleni ili kudhibiti utoro na kusaidia kuleta tija kama ilivyokusudiwa.

Ofisa Maendeleo Kata ya Songe, Fatuma Said, alisema tatizo la wazazi kutochukua nafasi yao ya malezi imesababisha kupunguza maadili katika j amii ikiwamo kufanya ukatili wa kijinsia kwa kukeketa wasichana.

Ofisa Mifugo Kata ya Songe, Joshua Mwenda, alitangaza kiama kwa wafugaji ambao hawatasajili mifugo yao, kuwekewa hereni kama utambulisho wake, watatozwa faini ya Shilingi milioni mbili. Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Songe, Hassan Mtambi, alisema mkutano huo ni wa kawaida na ulikuwa na dhamira ya kukutana na wananchi na kuwasikiliza matatizo yao na kupanga mipango ya maendeleo.

Diwani wa Kata ya Songe, Mohamed Makengwa, alielezea mafanikio ya uongozi wake, kipindi cha miaka miwili cha udiwani wake, kuwa ni pamoja kuhakikisha kumekuwapo na upatikanaji wa vyumba vya madarasa, zahanati, maji ukarabati wa miundombinu ya barabara na ongezeko la watumishi wa umma.

ama

ALHAMISI NOVEMBA 3, 2022

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 14

**Uharibifu wa vyanzo maji mabondeni, sasa yakaribisha ugumu kupatikana maji salama**



Ukurasa 15

Ilivyo rushwa ya ngono na sumu kisaikolojia iliyojaa ndani yake




Ukurasa 20

**Fedha za Uviko 19 zinavyogeuka msaada wa kuleta maji Bukoba**

KAZI YA MABINGWA NCHINI...

# Ugonjwa matumbo wazi kwa watoto na utaalamu wa kunusuru uhai wao

**Dk. Rajabu Mlaluko,** Mbeya

• Shida ya mzazi; sigara, pombe, dawa kulevya...

UGONJWA matumbo wazi au kitaalamu 'abdominal birth defects' huwapata watoto wadogo, ambao ukuta wa tumbo unabaki wazi, hata kufanya utumbo, ini au bandama unaonekana nje ya tumbo (abdominal cavity).

Kimsingi, kuna aina kuu mbili za tatizo hilo, kwanza ni pale viungo vya tumbo vinajitokeza nje kupitia uwazi kwenye ukuta wa tumbo, bila ya kufunikwa na kiwambo laini (membrane). Kitaalamu inaitwa 'gastroschisis.'

Pili, inatajwa kuwa penye viungo vya ndani ya tumbo kujitokeza nje na hufunikwa na kiwambo laini au kitaalamu 'membrane' au 'omphalocele'. Nayo, ni pale tatizo linajitokeza tumboni mwa mzazi kabla ya mtoto kuzaliwa.

Maana yake ni kwamba, mtoto anazaliwa akiwa na tatizo hilo, ikiwa ni ugonjwa nadra kutokea, japo katika sura ya pili inatajwa hatari kwa uhai wake. Tafiti zinaonyesha kuwa, kati ya watoto 10,000 wanaozaliwa, wanne ndio wanakutwa na hilo.

Pia, tafiti hizo huainisha kwamba hakuna sababu maalum inayosababisha mama kujifungua mtoto mwenye tatizo hilo, isipokuwa vichochezi maalum zinazomsababisha mjamzito kujifungua katika mazingira hayo.

Hapo kunatajwa umri mdogo chini ya miaka 20, uvutaji sigara, unywaji pombe, kuwa na historia ya kujifungua mtoto mwenye matumbo wazi, matumizi ya dawa za kulevya kukitajwa mifano ya aina za cocaine, bangi na 'methamphetamine', vilevile hali duni ya kimaisha.



Matabibu wa watoto wakiwa kazini.. **PICHA: YASMINE PROTACE**

**ANGALIZO LA MABINGWA**

Dk. Lazaro Mboma, bingwa katika Kitengo cha Upasuaji kwa Watoto kutoka Hospitali ya Rufani Kanda Mbeya, analifafanua kwa maelezo: "Tatizo hili kwa watoto wachanga, lilikuwa changamoto kubwa katika mazingira yetu.

"Kwani, katika mwaka mmoja uliopita, tulipokea wagonjwa 49 wenye tatizo hilo na watatu tu ndio walifanikiwa kupona kabisa, kulinganisha na miaka ya nyuma ambapo watoto karibu wote walikuwa wakipoteza maisha, kutokana na ukosefu wa vifaa na utaalamu.

"Kwa sasa, hali ya huduma zetu zimeimarika maradufu, kutokana na uwezeshwaji unaofanywa na timu ya madaktari bingwa wa upasuaji wa watoto kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, inayoongozwa na Dk. Zaituni Bokhary, bingwa mshauri wa upasuaji wa watoto.

Hapo, bingwa Dk. Lazaro Mboma anawashauri watoa huduma, akinena: "Mara wanapopata wagonjwa hawa wa matumbo wazi, basi wawafunike na karatasi za nailoni za aina yoyote ile na si kutumia vipande vya nguo au ngozi."

Anataja sababu za ushauri huo kitaalamu ni kuwalinda watoto dhidi ya upotevu wa maji na joto kwa njia ya mvuke, kwa kuwa matumbo yanakuwa wazi, akihimza wawahishwe hospitali zenye huduma kwa watoto wenye shida hizo.

Vilevile, bingwa mbobezi wa watoto kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Rehema Marando, analalamika kukosekana mifuko maalumu ya kuzuia matumbo yasipoteze maji na joto, pia kutokuwepo lishe maalumu inayopitia kwenye mishipa ya damu ya watoto hao.

Anaishauri serikali kupitia Wizara ya Afya, iongeze nguvu za upatikanaji mifuko hiyo maarufu 'silo bags" na lishe maalumu kwa watoto hao, kabla na baada ya kufanyiwa oparesheni hiyo.

"Wajawazito wote wafike kliniki mapema kwa ajili ya uchunguzi wa awali na kupata dawa zinazohitajika. Ikiwa watafika mapema na kuhudhuria kiliniki zao vizuri, basi itasaidia kugundua matatizo kama haya kwa kupitia vipimo kama 'ultrasound' na kadhalika," anaeleza.

Katika hoja hizo, mbobezi na mshauri kutoka hospitalini Muhimbili, ambaye pia ndiye ni msimamizi wa mradi wa ugawaji 'silo-bags' kwa ushirikiano na taasisi kutoka Ujerumani, anahitimisha kwa hoja zake:

"Tatizo lipo na hutokea kwa msimu, kwani kwa mwezi mmoja uliopita yaani mwezi wa tisa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, tulipokea watoto 11 na kati ya hao, ni wawili tu ndio walipoteza maisha.

"Tunaomba Wizara ya Afya isimamie utengenezaji wa 'silo-bags' nchini kwa kushirikiana na kampuni zinazotengeneza kondomu, ili kurahisisha upatikanaji wake, kuliko kusubiri hizi za sasa zinazotengenezwa nchini Afrika Kusini".

Anahitimisha kwa kauli: "Tunaiomba Wizara ya Afya, isaidie upatikanaji wa chakula maalumu kupitia mishipa ya damu (total parenteral nutrition) chenye virutubisho maalumu kwa watoto wachanga"

***• Mwandishi ni mtaalamu bingwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya. Anapatikana kwa; Simu, +255 753 93 86 28 na baruapepe; drrajabumlaluko@gmail.com***

MAZINGIRA

SHIDA YA MAJI KOTE... MORO NAKO?

# Uharibifu wa vyanzo maji mabondeni, sasa wakaribisha ugumu kupatikana

**Na Christina Haule,** Morogoro

KUNA mikakati inayotajwa mahsusi kutoka serikali mkoa Morogoro, ukiwataka wafugaji, wachimba madini na wakulima wanaotumia vyanzo vya maji kuendesha shughuli zao za kiuchumi, waache mara moja, huku wakivilinda vyanzo vilivyopo, hata wajinusuru na ukame.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Wakili Albert Msando, anayemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa, kwenye kikao cha Bodi ya Maji Bonde la Wami - Ruvu, kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji unaotishia kukauka kwenye mito mikubwa inayotiririsha maji ya kutumiwa na binadamu.

Wakili Msando anasema, wapo watu wanaendesha shughuli za kibinadamu kwenye kingo za mito na wengine mitoni, ambako kuna maji yanayotumiwa na watu milioni 11 kwenye mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam, jambo linalotajwa kuna hatari ya ukame.

Msando anauagiza uongozi wa Bonde la Maji, Wami Ruvu, kuendesha operesheni ya kuwaondoa wavamizi katika vyanzo vya maji na watakaokiuka sheria zilizopo, ikiwemo ya bondeni ndani ya mita 60 kutoka kilipo chanzo cha maji, hatua zinachukuliwa.

Anasema, kwa sasa wanashirikiana na Bonde la Wami Ruvu, kuangalia hatua stahiki za kuchukuliwa kuokoa hali hiyo na maji yanakopatikana, akiwataka wafugaji waache kulalamika wanapoondolewa maeneo hayo.

"Mkikamatwa kwa kuingiza ng'ombe kwenye vyanzo vya maji, mnatozwa faini ambazo wakati mwingine zinafika mpaka shilingi milioni nne kwa mfugaji mmoja. Sasa, hapo utakuwa umejenga mabirika mangapi kama una moyo wa kujenga mabirika ya kunyweshea, wakati birika moja mpaka linakamilika halizidi shilingi milioni kumi " anahoji Msando.

Anafafanua, taarifa zinaonyesha wafugaji kwenye maeneo yao sasa mkoani Morogoro, ni wavamizi na wamefuata maji na malisho, hivyo anawataka kurejea kwenye makazi yao wanakotokea.



Tukio la kampeni kupigania hifadhi ya maji Morogoro. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

> "Wavamizi kwenye vyanzo vya maji wanapaswa kuondolewa, elimu nayo izidi kutolewa kwa wananchi, maeneo tajwa yasivamiwe, sambamba na kurejesha uoto wa asili katika vyanzo vya maji.

### WANENAVYO WAHUSIKA

Mfugaji Timothy Olekoyesa, anaiomba serikali iwaruhusu kutumia vivuko vilivyotengwa kwenye mito iliyopo, wanyweshee mifugo yao kwa mujibu wa sheria ndogo za vijiji, kwa sababu kuna hatari wanaweza kupotezwa kwa wakati mmoja.

Pia, anaiomba serikali kuweka utaratibu wa kuwaelimisha wafugaji, kama wanavyofanyiwa wakulima kila mara, ili kuwawezesha kujua namna bora ya kufuga na kuhifadhi mifugo, kwa manufaa yao na taifa.

Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wilayani Morogoro, Eliah Madihi, anaiomba serikali iweke utaratibu bora wa kuondoa mifugo na kuacha kutumia nguvu.Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu, Elibariki Mmassy, anasema wamelazimika kusitisha vibali 12 vya watumiaji maji mkoani Morogoro, ili kupunguza matumizi ya maji na kukabiliana na ukame uliopo sasa, inayosababishwa na shughuli za kibinadamu na mabadiliko ya tabianchi.

Mmassy anasema, wamekuwa wakitoa barua zenye uamuzi huo tangu mwezi Mei mwaka huu, baada ya kubaini kutokuwepo mvua za kutosha za masika na vuli, ikiwamo maji na mvua isiyojitosheleza.

Sasa, Mmassy anawataka wadau wa maji kuzingatia vipaumbele vya kutoa vibali, ikiwemo kutunza mazingira, pia matumizi majumbani kulingana na upatikanaji maji, akisisitiza kupunguza matumizi ya maji kutasaidia kupambana na upungufu huo, akitaja mojawapo ni kupunguza matumizi majumbani.

"Mwaka huu haukuwa na mvua za utoshelevu na kufanya kupungua kwa kina cha maji kwenye mito mingi. Mpaka sasa kuna maji lita 2,580 kwenye mito, huku mililita 1870 zikiwa kwenye Mto Wami ambapo mahitaji ya maji kiujumla ni lita 9,000 na mahitaji ya majumbani ni lita 5,800 na kuna upungufu wa mililita 3200 za maji, " anafafanua Mmassy.

Mkurugenzi huyo anaendelea:"Miaka ya kawaida kwa tarehe kama hii, kunakuwa na ujazo wa mililita 14,000 kwenye mito, lakini kutokana na uharibifu unaofanywa na mabadiliko ya tabianchi na kutokuwepo mvua za kutosha za masika na vuli, kuna ukame katika mwezi huu wa Oktoba.

"Hali imekuwa tofauti na hali kama hii hutokea mwezi Novemba, mwishoni wakati mvua za masika zinataka kuanza kunyesha na kufanya kutokuwa na shida ya maji."

Pia, anafafanua bodi imejenga mabirika sita kwa gharama ya Sh. Mil. 60 kwa wafugaji, ili kuhifadhi maji na kufanya mifugo iendelee kuishi pasipo kuharibu vyanzo vya maji, kwa mabirika matano yamejengwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na moja wilayani Kilosa.

Mmassy anataja shughuli mbalimbali, zikiwemo umwagiliaji, matumizi ya maji viwandani na wavuvi, wamekuwa wakiharibu vyanzo vya maji na kufanya mito mikubwa minne kujaa michanga na tope, ikigharimu sasa uchimbaji mpya wa Sh. milioni 20.

Anaitaja mito hiyo ni; Mngazi, Mlali, Mpiji na Mgeta, akisema wanalazimika kuisafisha mito hiyo kwa awamu, ili kuipa uwezo wa kuhifadhi maji mara mvua zitakapoanza, hata kusaidia kukabiliana na ukame unaosogelea nchi sasa.

### HUDUMA SHERIA

Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Wizara ya Maji, Simon Nkanyemka, anawataka wadau wa maji kutambua umuhimu wa kuzingatia sheria za nchi, hata wakafanya shughuli za kibinadamu katika maeneo umbali mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji.

Anasema, wavamizi kwenye vyanzo vya maji wanapaswa kuondolewa, elimu nayo izidi kutolewa kwa wananchi, maeneo tajwa yasivamiwe, sambamba na kurejesha uoto wa asili katika vyanzo vya maji.

Nkanyemka anakinzana na hoja ya wanakijiji, akisema licha ya malalamiko ya wafugaji kuwapo sheria ndogo za vijiji zinazoruhusu kutumia vivuko kunywesha maji mifugo, anawatahadharisha mipaka ya sheria hizo haizidi za rasilimali maji za mwaka 2019 na ile ya mazingira mwaka 2004.

Kwa mujibu wa Nkanyemka, hadi sasa hakuna haki shughuli za kibinadamu kufanyika ndani ya mita 60 kutoka kilipo chanzo cha maji.

### BODI YA MAJI

Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu, Hafsa Mtasiwa, anasema wanawaangalia wananchi, wafugaji na wakulima wajipange kuona maji yakiwa mengi na wazidi kupata huduma ya maji kwa kuchimba visima au kwa kuweka mabwawa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Anthony Sanga, anazitaka bodi za maji za mabonde nchini, kuwa na mikakati mahsusi ya kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, ili kuzuia athari zake, katika vyanzo vya maji na kuleta ufanisi wa mabonde tisa ya maji yaliyopo nchini.

"Tumeona athari za mabadiliko ya tabianchi zilivyoathiri maeneo mbalimbali nchini mwaka huu hadi kusababisha upungufu wa maji kwenye vyanzo vingi vya maji.

INAENDELEA UK.15

AFYA

# Ilivyo rushwa ya ngono na sumu kisaikolojia iliyojaa ndani yake

**Na Yasmine Protace**

WATOTO wa kike, baadhi yao wamekuwa wakikumbana na matukio ya rushwa ya ngono. Kati yao, wapo wanaotoa taarifa, lakini kunashuhudiwa usugu wa matukio hayo kuendelea kutokea.

Hivi karibuni katika maadhimisho ya siku ya mtoto wa kike duniani, asasi ya Hance Obote, Ofisa Tathimini Ufuatiliaji Wanawake katika jitihada za kimaendeleo wanawake (WAJIKI), iliandaa maadhimisho hayo, ikisema wameamua kuanzisha mradi ambao wameupa jina la 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana.'

Malengo ya mradi huo ni kujenga uelewa mpana wa jamii juu ya masuala ya rushwa ya ngono na athari zake kwa watoto, hasa wa kike.




Baadhi ya wanafunzi wakiwa katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, ambapo WAJIKI waliandaa maadhimisho hayo, katika Shule ya Sekondari Makumbusho, Dar es Salaam. **PICHA: YASMINE PROTACE**

Katika kipindi cha mwaka 2015, mwezi Machi hadi Desemba mwaka huo, ukaanzishwa mradi wa kuwajengea, uelewa wa rushwa ya ngono wanawake katika kipindi cha uchaguzi.

Hance Obote, Ofisa wa asasi WAJIKI katika maadhimisho ya siku ya mtoto wa kike, yaliyofanyika Katika Shule ya Sekondari Makumbusho, Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau wa maendeleo kutoka ubalozi wa Uswizi, Kihowede, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Women Fund, Tanzania Trust Sema, Felm ,We AinoAid na Wajiki.

Anasema mwaka 2016, mwezi Juni hadi Septemba mwaka huu, yalianza matembezi ya nyumba kwa nyumba kwa kuwawezesha jamii kuvunja ukimya dhidi ya rushwa ya ngono na aina zote za ukatili wa kijinsia.

"Machi 2018 hadi Desemba, ilizaliwa kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa' ya ngono kwa wasichana na wanafunzi inawezekana ," anasema.

Anaongeza kuwa, mwaka 2019 wakawajengea uwezo madereva bodaboda, daladala na viongozi wao athari za rushwa ya ngono kwa wanafunzi, wasichana na wanawake wamebeba ajenda kampeni na kuchukua hatua ya kumlinda mtoto wa kike dhidi ya rushwa ya ngono na ukatili kijinsia.

Obote, anaongeza kuwa mradi huo ulifanyika katika Mansipaa ya Ilala, Kinondoni na Temeke na kuwa wanufaika wa mradi huo ni wasichana walioopo ndani na nje ya shule.

Anaongeza kuwa walengwa wengine wa mradi huo ni mashirika, makundi ya kijamii ,ambapo vinara wa kampeni walikuwa wanafunzi na vijana.

"Wanufaika wa moja kwa moja ni madereva ambao waliofikiwa Kinondoni walikuwa 1975, Ilala 1479, Temeke 851," anasema na kufafanua, shule zilizonufaika na mradi ni Kinondoni shule 20, Ilala kuna shule sita na Temeke shule nne.

> **Machi 2018 hadi Desemba, ilizaliwa kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa' ya ngono kwa wasichana na wanafunzi inawezekana.**

Mkuu wa Dawati la Takukuru, kutoka Kinondoni, Backbie Msumi, anasema wanaofanyiwa ukatili wanatakiwa kutoa taarifa ili wahusika wachukuliwe hatua.

Anaongeza kuwa, kila anayefanyiwa ukatili anatakiwa kutoa taarifa, ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria na anaendelea: "Tunapoona ukatili umefanywa haitakiwi kuyafumbia macho, tukiyafumbia macho matukio ya kikatili,tujue yataendelea kutokea."

Diwani wa Kata ya Makumbusho, Mohamed Ally Mohamed, anasema kuwa ukatili upo, hata katika Shule ya Sekondari Makumbusho, baadhi ya watoto wa kiume wamekuwa wakifanyiwa ukatili.

Anaongeza kuwa elimu iendelee kutolewa, ili kuendelea kupambana na rushwa ya ngono na anasema, katika kuadhimisha maadhimisho hayo wameona ni bora kuwashirikisha madereva wa bodaboda na daladala, kwa sababu wameona wanakuwa karibu sana na jamii.

Anashauri walimu na wazazi washirikiane kwa kuhakikisha watoto wanapata haki zao na anasema, watoto wanapoona wanafanyiwa matukio ya ukatili, waende kutoa taarifa katika madawati ya jinsia, ili wahusika wachukuliwe hatua.

## Uharibifu wa vyanzo maji mabondeni, sasa yakaribisha ugumu

**INATOKA UK.14**

"Ili kuepuka hali ya aina hii isijirudie, bodi zote za mabonde zifanye tathmini ya kina kuhusu changamoto zilizotokea na kuweka mikakati mahsusi, ili kukabiliana na athari zote zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

"Tuhakikishe mvua zinazonyesha zinakuwa na manufaa, kwa kujenga mabwawa kwa ajili ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadaye na hasa katika kipindi cha ukame," anaelekeza Mhandisi Sanga.

Pia, Mhandisi Sanga anazipongeza bodi hizo kwa kuongeza ufanisi kutoka asilimia 51 ya mwaka 2019/2020 hadi asilimia 75.2 kwa mwaka 2020/2021, akidokeza haja ya kuwa na msukumuo katika ukaguzi wa vibali vya maji vinavyotolewa kwa wateja wote kila mara.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya hewa Tanzania (TMA) iliyotolewa kama Dondoo muhimu za mvua za msimu wa mwezi Novemba 2022 hadi Aprili, 2023, kuanzia mwezi huu hadi ujao, kutakuwapo upungufu mkubwa wa unyevu wa udongo unaotarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi yanayopata mvua za msimu na kuathiri ukuaji mazao, hali kadhalika upatikanaji malisho ya mifugo.

Taarifa hiyo, inasema kina cha maji katika mito na mabwawa kinatarajiwa kupungua na kuathiri upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali kama vile umwagiliaji na uzalishaji wa nishati.

Mamlaka zinashauriwa kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa pamoja na kuweka miundombinu ya uvunaji maji sambamba na kuandaa na kutekeleza mipango mikakati ya kuhimiza kilimo himilivu.

Hivi karibuni Menejimenti ya Maafa Tanzania imesema ma Watanzania takriban 437,000 kutoka maeneo mbalimbali ya nchi wanahisiwa kukabiliwa na tishio la upungufu wa chakula.

Mkurugenzi Msaidizi kutoka Idara ya Uratibu wa Menejimenti ya Maafa iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Charles Msangi, anasema Watanzania hawana sababu ya kuhofu hali hiyo.

Ni hali inayotajwa inaendana na sura ya pili, kukibashiriwa takriban Watanzania 437,000 wanahisiwa kukabiliana na tishio kali la upungufu wa chakula, kwa mujibu wa shirika linalojihusisha na uangalizi wa usalama wa chakula nchini la Integrated Food Security (IPC).

Taarifa hiyo inasema kati ya halmashauri 14 ambazo IPC ilifanya tafiti ikijumuisha watu milioni 3.4, ni kwamba halmashauri nne za wilaya za Handeni, Longido, Mkinga, na Monduli, zimeshariotiwa kukabiliwa na tishio la upungufu wa chakula.

Taarifa ya Umoja wa Mataifa UN iliyotolewa Mei mwaka huu, inasema baa la njaa linanyemelea Afrika Mashariki, huku kukibashiriwa ukame kwa miaka mitano mfululizo.

Mashirika sita ya Umoja wa Mataifa na wadau wengine wa masuala ya kibinadamu, wameshatoa tahadhari ya baa la njaa kunyemelea Afrika Mashariki, baada ya miaka minne ya ukame mkali, huku ikitabiriwa uhaba wa mvua kwa miaka mingine mitano mfululizo.

Taarifa hiyo ya pamoja iliyotolewa mjini Nairobi Kenya na mashirika ya Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani WFP, la chakula na kilimo FAO, la kuhudumia Watoto UNICEF, la kuhudumia wakimbizi UNHCR, la utabiri wa hali ya hewa WMO na la kuratibu masuala ya kibinadamu na misaada ya dharura OSHA na washirika wengine kama UKaid imesema ukame uliokithiri na unaoendelea unaathiri misimu mingi ya mvua Somalia, Kenya, na maeneo ya wafugaji ya mashariki na Kusini mwa Ethiopia ambao haujawahi kutokea.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka mtandao wa justdiggit wa mwaka 2020 unasema ukame ni changamoto ya kidunia ambapo theluthi mbili ndani ya ardhi ya Afrika imeharibika.

Mpango wa Urejeshwaji wa Mazingira ya Msitu wa Afrika (AFR100) una lengo la kurudisha hekta milioni 113 za ardhi ndani ya Afrika kabla ya mwaka wa 2030 na kwamba hilo ni eneo kubwa kama Sweden, Finland na Norway pamoja na kwamba lengo ni kuharakisha urejeshwaji wa ardhi, kuongeza usalama wa chakula, kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na kupunguza umaskini.

Pia taarifa ya Umoja wa mataifa ya mwaka 2020 imeonyesha kwamba pembe ya Afrika inakabiliwa na hali mbaya ya ukame kuwahi kuonekana katika muda wa miaka 40, kutokana na ukosefu wa mvua kwa misimu kadhaa.

AFYA

# Simulizi za uhalisia mabinti Njombe wanavyoangukia janga ndoa utotoni

• Wazazi walioponza watoto waanika siri, mzizi wa tatizo



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mpechi, ambao wanaangukia katika kundi la wanaopaswa kutetewa nafsi zao, dhidi ya ndoa za utotoni. **PICHA: ELIZABETH JOHN**

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

LUCIA Mlowe mwenye miaka 21, anasema aliingia katika maisha ya ndoa katika umri miaka 16. Anaeleza, kipindi chote cha ndoa yake amekuwa akikiona kama ndoto, kwa sababu hakufahamu kilichoendelea.

Huyo ni miongoni mwa wasichana wanaotoka katika jamii zinazoruhusu ndoa za mapema, uamuzi unaopingana na Sheria ya Ndoa nchini, inayoweka utaratibu wa kuolewa binti mwenye umri chini ya miaka 18.

Pia, Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inamtambua mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18. Kadhalika, Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978, inamkataza mwanafunzi kubeba ujauzito.

Hata hivyo, umasikini na migogoro ya familia unatajwa, imekuwa chanzo kinachosukuma mabinti wengi kuingia katika ndoa za utotoni na hata kuhatarisha afya zao.

Hapo Lucia anasimulia: "Niliolewa nikiwa mtoto, sikuwa najua mume anatakiwa kufanyiwa nini, wala majukumu ya ndoa kiujumla. Kiukweli, nilikuwa ni mtoto hata sijui ilitokeaje."

Lucia, mzaliwa wa wilayani Ludewa, mkoa wa Njombe, anasema alilelewa na baba yake na mama wa kambo, baada ya mama yake kufariki.

"Nilimaliza darasa la saba, nikatakiwa kwenda sekondari, ndipo tatizo lilipoanza, kwa sababu mama yule hakutaka mimi nisome. Ugomvi wa mara kwa mara kati ya baba na mama, ulisababisha niolewe," anasimulia, huku akidokeza ndoto ya kuendelea na shule ilikonasa.

Anasimulia alichokikuta ni tofauti na matarajio kwenye ndoa, kwa sababu mwanaume alitumia umri wake mdogo kumnyanyasa kingono.

> "
> **Zinataka anayeoa awe ni kijana aliyekomaa miaka 18 na kuendelea, siyo sasa miaka 12 au 13.Huu ni umri mdogo atapata shida hata kwenye uzazi wake.**

"Maisha yalikuwa ni magumu, kwa sababu sikuwa na maamuzi ya kitu chochote,sikujua hata mume anatakiwa kufanyiwa nini," anasema.

Anasimulia hata madhila wakati wa kujifungua, alikuwa na magumu ikiwamo kupoteza damu nyingi na hata kuzimia siku mbili.

Ni simulizi kama hiyo inapatikana kwa Maria Mwalongo (23), aliyeolewa katika umri wa miaka 15, akisema zahama iliyoanzia katika maisha ya kumtegemea mume, huku akikosa fursa ya elimu.

"Umasikini umenifanya niingie kwenye tatizo la ndoa za mapema, kwa sababu nilitakiwa kuendelea na shule ya sekondari, lakini ilishindikana kwa sababu ya mtu wa kunihudumia shuleni hakuwepo kwa sababu baba alifariki," anasema.

Anaendelea:"Baada ya baba kufariki kila kitu kilibadilika, nilikaa nyumbani ndipo alitokea mwanaume na kutaka kunioa nilikataa,ila ndugu walinilazimisha hadi nikakubali."

Huku sasa akikemea ndoa za utotoni, anasimulia: "Madaktari waliniambia kutokana na umri wangu nisingeweza kujifungua kwa njia ya kawaida, kwa sababu nyonga zangu zilikua hazitanuki.'

"Maisha yanaharibika ukiwa mdogo unakuwa huna maamuzi,mwanaume anakupeleka tu, lakini ukiolewa na umri ulioko maana una uwezo wa kuhoji unapoona kuna jambo haliko sawa," anaeleza.

**WANAOSABABISHA**

Mzazi Vestina Lwiva, anaeleza huko nyuma ana simulizi kuhusu matendo anayoyajutia sasa, kwa kushirikiana na ndugu zake kumuozesha mdogo wake

"Muda umepita kidogo, mimi na ndugu zangu tulishiriki kumuozesha mdogo wangu ambaye alitoka tu kumaliza la saba, ilikuwa ni mbaya! Alibeba mimba akafariki kwa uzazi," anaeleza kwa masikitiko.

Anakiri changamoto iliyoko ni umasikini na kukosa elimu ya kutosha kuhusu ndoa za utotoni na namna zinavyogharimu maisha ya watoto.

Ni hoja inayoungwa mkono na Justine Sanga, anayelalamika jami kukosa uelewa sahihi kuhusu madhara ya ndoa za utotoni hadi sasa.

"Watoto wanaolewa wakiwa wadogo kwa siri. Jamii haijui madhara ambayo binti huyu anaweza kupata, elimu zaidi itolewe na sheria, pia isimamiwe." anashauri.

**WATAALAMU ELIMU**

Ofisa Elimu ya Msingi - Takwimu, Halmashauri ya mji Njombe, Augusta Wellah, anasema: "Kwa kweli kwa habari ya ndoa za utotoni kwetu halipo, ila masuala ya ulawiti,ubakaji huwa tunaendelea kutoa elimu toka watoto wadogo kabisa wa darasa la kwanza. Awali siwezi kusemea sana habari ya ndoa za utotoni.'.

Mwalimu Joyce Ngata, kutoka Idara ya Elimu Sekondari katika Halmashauri ya Mji Njombe, anabashiri huenda ndoa hizo zipo, lakini zinafanyika kwa siri, kwani kuna familia zinazomuona mtoto anapopevuka au kumaliza shule ya msingi, wanaamini amekuwa mtu mzima.

"Umasikini wakati mwingine unafanya wazazi wapokee mahari wakijua amemaliza shule sasa ni mtu mzima, sambamba na mabadiliko ya sheria lakini pia zisimamiwe kwa sababu mtoto anapoolewa anakwenda kubebeshwa mizigo mizito' 'anaeleza Joyce.

**VIONGOZI WA DINI**

Shekhe wa Wilaya ya Njombe, Shabani Dinga, anakemea kwa kauli kwamba, hakuna imani inayoruhusu msichana kuolewa akiwa na umri mdogo.

Anasema muda sahihi wa binti kuolewa, ni pale anapopevuka kimwili, lakini inaendana pamoja na kutimiziwa haki zake za msingi, ikiwamo malezi na elimu.

"Atapewa mafunzo yatakayohusu maisha yake ya baadaye, lakini wakati huo huo ataelimishwa masuala ya mahusiano. Lakini, anapofikisha miaka 18 atakuwa na nafasi ya kuolewa," anasema Sheikh Dinga.

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God, mkoani Njombe, Zephania Tweve, anaungana na mtangulizi wake wa kiimani, kwamba hata andiko lao linakemea ndoa za utotoni.

"Sisi viongozi wa dini na serikali tuendelee kupambana kwa sababu tukilegeza kwenye eneo hilo tutafanya watoto wengi waumie kwa kuwa, ndoa chini ya miaka 18 ni za utoto," anafafanua Mchungaji Tweve.

Katibu wa Baraza la Wazee wa Mila wa kabila la Kibena,Julius Msigwa, anasema mila na desturi za kabila lao haziruhusu ndoa za kijana wala msichana.

"Zinataka anayeoa awe ni kijana aliyekomaa miaka 18 na kuendelea,siyo sasa miaka 12 au 13.Huu ni umri mdogo atapata shida hata kwenye uzazi wake," anasema.

**USTAWI JAMII/SHERIA**

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Mji Njombe, Petro Mahanza, anasema sasa wamekuja na mbinu za kujengea uwezo, kamati za kupinga ukatili wa mama na mtoto kuanzia ngazi za mitaa na vijiji.

"Wajumbe wake ni wenyeviti wa vitongoji, watu wa dini, watu maarufu, watendaji na mwenyekiti kwa hiyo wale tunaamini kwamba wanaweza kutuibulia chochote kitakachokua kinaendelea, tofauti na kwenye ngazi ya jamii ili kuzuia ndoa hizo," anasema Mahanza.

Wakili wa Kujitegemea, Innocent Kibadu, anasema Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 na marejeo ya mwaka 2019, inamkataza mwanaume yeyote ambaye hajafikia miaka 18 au mwanamke wa umri haujafikia miaka 15, kuoa au kuolewa.

"Kifungu cha (13) Kifungu Kidogo cha (2), kinaruhusu ndoa kwa mtu mwenye umri wa miaka 14 katika mazingira ambayo mahakama kama itaona inafaa inaweza ikaruhusu," anasema.

Kwanini ndoa zaidi za utotoni? Mwanasheria huyo, anaendelea: "Maeneo hasa vijijini hawana elimu ya kutosha juu ya madhara ya ndoa za utotoni.Watoto wengi wanamaliza shule wakiwa na umri mdogo na wengine hawamudu kwenda elimu ya sekondari kwa hiyo wanabaki nyumbani. Hiki ndicho kinaleta kichocheo cha watoto kuoa au kuolewa."

INAENDELEA UK.17

MAZINGIRA

# Unaujua Mkutano COP 27, pia manufaa yake kwa Mtanzania?

• Wataaluma wazawa, waainisha kilio

**Na Jenifer Gilla**

ZIMEBAKI siku tatu, macho na masikio ya Watanzania yataelekezwa jijini Sharm El Sheikh nchini Misri, ambako kunategemewa kuanza kwa Mkutano wa 27 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabia nchi, maarufu Conference of Parties (COP27), kati ya Novemba 6 hadi 18.

Ni mkutano utakaoongozwa na kaulimbiu 'Utekelezaji' ukija katika kipindi chenye madhara makubwa ya mabadiliko ya tabia nchi yanayoendelea kuonekana barani Afrika, ikiwamo ukame, mvua kutotabirika, joto kuongezeka, mafuriko na magonjwa kama vile dengue na malaria.

Nchini Tanzania, kwa miaka takribani mitatu shughuli za kilimo zimeathirika, huku maeneo ya vijijini ambako ndiko kwenye wazalishaji wakubwa wa vyakula, nako wanalalamika njaa wakiomba serikali iwapelekee chakula.

Baadhi ya maeneo nchini, ikiwamo kijiji cha Sindeni katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, wanalazimika kununua unga kwa bei Sh.1800 baada ya kilimo kukataa kwa miaka mitatu, wakiwa sio haba katika kuzalisha mahindi ya sembe.

Mifugo nayo, inatajwa kufa kwa kukosa chakula na maji, hata juhudi za maendeleo sasa zinatuama.

Mkoani Dar es Salaam, kunakoongoza kwa wakazi kitaifa, linapitia changamoto ya mgawo mkali wa maji, kutokana na kupungua kina cha maji kutoka vyanzo vya Ruvu Chini na Ruvu Juu, hata kuuweka mji katika hatari ya magonjwa ya mlipuko.

Hivyo, baadhi ya ajenda zinazotegemewa kujadiliwa mkutanoni Misri ni upatikanaji fedha za kuzisaidia nchi masikini kukabiliana na athari hizo, kuwapo mfuko wa kusaidia nchi zinazoendelea pale zinapopatwa na majanga yatokanayo na athari za mabadiliko ya tabia nchi, kama vile mafuriko na uhaba wa chakula.

Pia, kunatajwa kutakuwapo majadiliano kuhusu uzalishaji wa gesi joto, kwamba mpaka sasa ni kiasi gani cha gesi hiyo inaenda angani. Pia pa kujiuliza, madhara yake yakoje na namna ya kupunguza kasi ya uzalishaji, ikizingatiwa kasi hiyo imeongezeka, ikilinganishwa na miaka 100 iliyopita.



Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Kilimo Kusini mwa Afrika, (SACAU) Dk. Sinare Yusuph. **PICHA ZOTE: MAKTABA**



Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Kisayansi linaloshughulika na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi, pia mtaaluma wa Mabadiliko ya Tabianchi, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Prof. Pius Yanda.

Ni majadiliano yanayokuja, baada ya tathmini za kisayansi za Jopo la Wataalamu wa Kimataifa Linaloshughulika na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi, chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa (IPCC) kuonyesha kuwa kwa sasa joto hilo ni nyuzi 1.09 na likifikia 1.5 hali zitakuwa kubwa huku na ikifika nyuzijoto 2, hali itakuwa mbaya zaidi.

**WANAZUONI DAR**

Mhadhiri wa Mabadiliko ya Tabia nchi, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Prof. Pius Yanda, anasema kuwa mkutano huo unafanyika Afrika, matarajio yakiwa utajikita zaidi kujadili namna ya kuzisaidia nchi za Afrika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Anasema, mfano Tanzania kupitia Makubaliano ya Paris ya Mwaka 2016, imeunda malengo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi (NDC). Ili kuifikia, kunahitajika Dola za kimarekani bilioni 19.23 ambazo ni ngumu kupatikana kwa nchi masikini.

"Nchi za Afrika zinatakiwa kutumia nafasi hii kuhakikisha kuwa zile Dola bilioni 100 zilizoahidiwa kutolewa na nchi zilizoendelea kusaidia nchi masikini kukabiliana na athari hizi zinapatikana, pia mfuko wa kusaidia majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi ( loss and damage) unafanya kazi na kuwafikia wa Afrika wote" anasema.

Prof. Yanda, Makamu Mwenyekiti wa (IPCC), anasema kutumike nafasi hiyo kuomba kuwezeshwa kiteknolojia, ili ichangie kupunguza uzalishaji gesi joto, akitoa mfano wa kukuza teknolojia ya kunyonya hewa ya kaboni kupitia mikoko na bahari.

"Ingawa mchango wa Afrika katika kuzalisha gesi joto ni asilimia 0.15 tu lakini ndio waathirika wakubwa kutokana na umasikini na teknolojia kuwa duni, lakini tuna shughuli zinazochangia kuharibu mazingira kama vile ukataji wa misitu kwa matumizi ya mkaa na makazi," anasema.

Matarajio yake anasema ni kuona malengo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanajadiliwa upya, ili kupunguza makali ya athari zake kwa sababu haya yaliyopo sasa yanaonekana kutozaa matunda .

Anashauri, pia nchi zinazoendelea zibanwe kuonyesha namna ya kupunguza uzalishaji mafuta na matumizi ya makaa ya mawe na gesi asilia, kwa sababu ndio vyanzo vikuu vya uzalishaji gesi joto.

"Baadhi ya nchi zilizoendelea ilifika mahali ziliacha kabisa kutumia makaa ya mawe, lakini baada ya mabadiliko ya uongozi yale matumizi yakaruhusiwa tena, sasa fikiria nchi kama hizo zinazalisha zaidi yetu lakini madhara makubwa yanazikuta nchi masikini," anasema.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Kilimo Kusini mwa Afrika, (SACAU) Dk. Sinare Yusuph, anaeleza nchi za Afrika, zitumie nafasi hiyo kuiambia dunia kilimo cha nchi masikini, kina mchango mdogo sana katika mabadiliko ya tabianchi, lakini kimeathirika kwa kiasi kikubwa.

Aidha, anazitaka nchi hizo kutumia nafasi hiyo kuhakikisa zinapewa msaada wa fedha na teknolojia kukabili majanga, fedha zinazohitajika ambazo zinahitaji kutolewa na nchi zilizoendelea kutokana na mchango wao mkubwa katika kusabisha mabadiliko ya tabia nchi.

"Tunahitaji teknolojia itakayomwezesha mkulima kule vijijini kuboresha upatikanaji wa chakula, kuongeza thamani ya mazao yake ili nchi iwe na chakula cha kutosha lakini pia aweze kuuza na kujiongezea kipato. Hii yote inahitaji uwezeshwaji fedha na teknolojia" alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utu na Mazingira (HUDEFO) Sarah Pima alisema anatarajia kuona mijadala ya kuziwezesha nchi masikini teknolojia ya kuteketeza taka ngumu kwa kuwa zinatoa gesi aina ya methane ambayo inachangia kutengeneza gesi joto.

Alisema pia anatarajia kuwapo mijadala ya namna ya kushirikisha watoto katika mapambano hayo,ili kuwapa elimu na kutengeneza vizazi vitakavyoendeleza mapambano hayo hapo baadaye.

**JAMII MTAANI**

Meneja Mradi wa Msichana kuchukua Hatua Dhidi ya Mabadiliko ya tabianchi kutoka Chama cha Maskauti wa Kike Tanzania (TGGA), Nyendo Kinyonga, anasema wanatarajia kuona majadiliano ya namna ya ushiriki wa wanawake dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Wanawake na wasichana ni waathirika wakuu wa athari za mabadiliko ya tabia nchi kwa sababu ndio wahudumiaji wa familia, wanahusika kutafuta maji, chakula na nishati ya kupikia," anasema.

Mfugaji Joshua Godliver, wa kijijini Sindeni, Handeni, Tanga anasema anatarajia mkutano huo utajadili namna utakavyomwezesha mfugaji kukabiliana na ukame unaosababisha mifugo kufa kwa kukosa maji na chakula.

"Tunahitaji viongozi wetu watakaporudi waje na suluhisho la kufa kwa mifugo, teknolojia ya kisasa itakayoniwezesha mimi kuendelea kufuga na sio kuniambia niuze mifugo yangu, kufuga ndio kitu pekee nilichojifunza tangu nikiwa mdogo na ninategemea kurithisha watoto wangu," anaeleza.

## Simulizi za uhalisia mabinti wanavyoangukia janga ndoa utotoni

**INATOKA UK.16**

Kwanini ndoa zaidi za utotoni? Mwanasheria huyo, anaendelea: "Maeneo hasa vijijini hawana elimu ya kutosha juu ya madhara ya ndoa za utotoni.Watoto wengi wanamaliza shule wakiwa na umri mdogo na wengine hawamudu kwenda elimu ya sekondari kwa hiyo wanabaki nyumbani. Hiki ndicho kinaleta kichocheo cha watoto kuoa au kuolewa."

Anaikosoa sheria ya ndoa kwamba inakinzana na sheria ya elimu. "Kwanini nasema inakinzana? Kwa sababu unakuta watoto wengi wenye umri wa miaka 14 hadi 18 na 20 bado wapo shuleni, kwa hiyo kuna mkinzano wa sheria."

Anafafanua kuwa Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 na marejeo, pia marekebisho ya mwaka 2002 na 2016, inakataza kuolewa au kuoa mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari, awe wakiume au wa kike, ikielekeza adhabu ya kifungo kirefu

**NENO LA MBUNGE**

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, anasema sheria ni zao la jamii na mchakato wa kutunga, ni lazima ushirikishe jamii.

"Sasa hivi serikali ipo kwenye mchakato wa kukusanya maoni kwa makundi mbalimbali ili kuweza kutatua hiyo changamoto ya sheria ya ndoa, hasa umri kama ambavyo mahakama imesema," anasema.

Ni mchakato, zao la msukumo wa kisheria kutoka kesi ya madai ya mwaka 2016, aliyofungua Rebecca Gyumi, katika Mahakama Kuu dhidi ya serikali ya kupinga kipengele cha Sheria ya Ndoa nchini, kuruhusu mtoto wa kike kuolewa katika umri usio rafiki kiafya.

**HALI HALISI NCHINI**

Wakati awamu ya kwanza ya Takwimu ya Idadi ya watu ikitolewa nchini wiki hii, Takwimu za Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya (TDHS) 2015-2016, zimeonyesha asilimia 36 ya mabinti wenye umri wa miaka 20 hadi 24 walikuwa wameolewa kabla hawajatimiza umri miaka 18.

Pia, Demografia ya Afya nchini ya Mwaka 2010, inanyooshea kidole mikoa yenye viwango vikubwa vya ndoa za utotoni ni Sinyanga (59%), Tabora(58%), Mara(55%) na Dodoma(51%).

Ripoti mpya ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), inaiorodhesha Tanzania ya 11 kati ya nchi zenye idadi kubwa zaidi ya ndoa za utotoni.

MAZINGIRA

EWURA YABAINI...

# Mabilioni lita za maji yanapotea, yaunda mwongozo wa kuwajibika

• Mamlaka kupoteza kienyeji 'sasa basi'




Tukio la kuzinduliwa huduma ya maji, eneo ambalo EWURA inasisitiza umakini maji yasipotee. **PICHA: MAKTABA**

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MIONGONI mwa vikwazo vilivyopo kwenye mamlaka za maji nchini, ni upotevu mkubwa wa maji, kusababisha kukosa mapato.

Ripoti za utendaji kazi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini 2018/19 hadi 2020/21, zilizotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA), zinaonyesha mita za ujazo milioni 411 za maji zimepotea kwa sababu mbalimbali, ikiwamo uchakavu wa miundombinu.

Maji hayo yanayopotea, ni sehemu ya mita za ujazo bilioni 1.1 zilizozalishwa na mamlaka 91 za maji, kati ya mwaka 2018/19 hadi 2020/21.

Kwa mujibu wa ripoti ya EWURA, mwaka 2020/21, upotevu wa maji katika mamlaka za miji mikuu ya wilaya na miji midogo ni asilimia 40 ya mita za ujazo milioni 87.3 za maji yaliyozalishwa, yenye thamani ya Sh.bilioni 417.7.

Pia, inabainisha upotevu huo katika mamlaka za miradi mikubwa ulikuwa asilimia 24.4 ulitokana na sehemu ya uzalishaji wa mita za ujazo milioni 72.88 za maji yenye thamani ya Sh.milioni 52.786.

Kwa upande wa mamlaka za miji mikuu ya mikoa, upotevu ulikuwa asilimia 38 ya mita za ujazo milioni 943.9 za maji yenye thamani ya Sh.bilioni 97.99, maji hayo yakipotea, wakati uzalishaji wake umeshatumia umeme, dawa na mishahara ya wataalamu, hivyo kusababisha mamlaka husika kuingia hasara kubwa.

> **Moja ya changamoto kubwa ya sekta ya maji ni kuendelea kuwa na viwango vikubwa vya maji yasiyolipiwa, ikilinganishwa na kiasi kinachokubalika cha asilimia zisizozidi 20.**

### MWONGOZO UDHIBITI

EWURA imeshachukua hatua mbalimbali za kuzibana mamlaka za maji zidhibiti upotevu huo wa maji, ikiwamo kuandaa mkakati wa kupunguza maji yasiyolipiwa wa mwaka 2021 ili kudhibiti hali hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Modestus Lumato, anasema wataalamu wa mamlaka za maji 31 kwenye mafunzo ya kuzijengea uwezo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira juu ya miongozo ya kiutendaji.

Anasema kwa kipindi cha miaka 11 sasa tangu kuanzishwa, EWURA imekuwa ikifuatilia utendaji wa mamlaka hizo na kuandaa taarifa za utendaji wa kila mwaka, ikiwa na taarifa za viashiria vya utendaji.

"Moja ya changamoto kubwa ya sekta ya maji ni kuendelea kuwa na viwango vikubwa vya maji yasiyolipiwa, ikilinganishwa na kiasi kinachokubalika cha asilimia zisizozidi 20."

"Kwa mara ya kwanza tumeandaa mwongozo utakaoziwezesha mamlaka za maji kuandaa mikakati yao ya kupunguza kiasi cha maji yasiyolipiwa," anasema.

Alieleza kuwa matarajio yao ni mamlaka hizo kuwa na mikakati bora ya kupunguza kiasi cha maji yasiyolipiwa na hivyo kuongeza ufanisi wao wa utendaji na kupunguza upotevu wa mapato.

Anaongeza "Mwongozo huu hauna adhabu kwa wasiotekeleza, unawezesha kupanga mikakati yao, baada ya mwaka mmoja tutaanza kufuatilia utekelezaji wao ili kuona mabadiliko, tunawasisitiza watumie miongozo hiyo ili kupunguza upotevu huo."

Mkurugenzi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira EWURA, Mhandisi Exaudi Fatael, anasema EWURA imeandaa mwongozo huo ili kuimarisha huduma na utendaji kazi wa mamlaka hizo.

### TEKNOLOJIA UDHIBITI

Wizara ya Maji mwezi Juni mwaka huu, ilishuhudia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) ikiingia mkataba wa thamani ya Sh. bilioni 1.4 na kampuni ya CityTaps ya Ufaransa, ikipanga kukabiliana na upotevu wa maji katika eneo la Mwisenge, Manispaa ya Musoma, mkoani Mara.

Utiaji saini wa mkataba huo ulifanyika katika Wizara ya Maji jijini Dodoma, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, anasema mkataba huo ni mwendelezo wa hatua za wizara kukabiliana na changamoto ya kupotea maji.

Anasema Mamlaka hiyo na Kampuni ya CityTaps ya Ufaransa waliandaa andiko la juu mkakati wa kupunguza kiwango cha upotevu wa maji kwa kutumia teknolojia mpya ya "Smart Meters" inayotumia mawimbi ya satelaiti kubaini mivujo ya maji ardhini.

"Anaongeza; "Natarajia ufanisi na matokeo mazuri katika utekelezaji wa mradi huu, ambao utadhibiti kiwango cha upotevu wa maji lakini pia kubaini sababu zinazosababisha upotevu wa maji na kuja na mkakati bora wa kukabiliana na changamoto hiyo katika maeneo mengine nchi nzima."

Meneja Biashara wa Kampuni ya CityTaps, Aurelie Guibert anasema pamoja na utekelezaji wa mradi huo watakuja na mkakati bora utakaokua suluhisho la upotevu wa maji nchini Tanzania.

Anasema, mradi ni wa majaribio na wa kwanza wa aina yake hapa Tanzania ambao utatekelezwa kwa muda wa miaka miwili na pindi utakapokamilika na kufanikiwa utatekelezwa kwenye Mamlaka za Maji za nchi nzima.

### HALI YA MAJI

Katika bajeti 2022/23, Waziri wa Maji Jumaa Aweso, anasema rasilimali za maji nchini zinakadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka, rasilimali za maji juu ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 105 na zilizopo ardhini mita za ujazo bilioni 21.

"Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali nchini yanakadiriwa kuwa ni takribani mita za ujazo bilioni 47 kwa mwaka sawa na asilimia 37.37 ya maji yaliyopo nchini," anasema.

Anasema mahitaji hayo ya maji yanatarajiwa kuongezeka hadi kufikia wastani wa mita za ujazo bilioni 80 kwa mwaka ifikapo mwaka 2035.

Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002, inalenga kuboresha huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini ili wapate huduma hiyo kwa umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye makazi yao, huku Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ikilenga kuboresha huduma za maji vijijini kufikia asilimia 85 ifikapo mwaka 2025.

Katika kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi waishio vijijini inafikia zaidi ya asilimia 85 ifikapo mwaka 2025, Serikali imeendelea kujenga, kukarabati, kupanua mitandao ya kusambaza maji pamoja na kuimarisha usimamizi wa huduma ya maji.

Hadi mwezi Aprili 2022, upatikanaji wa huduma ya maji vijijini umefikia wastani wa asilimia 74.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 72.3 mwezi Machi, 2021. Kiwango hicho kinatokana na kukamilika kwa ujenzi wa miradi mipya, ukarabati na upanuzi wa miradi 303 ambayo imeanza kutoa huduma kwa wananchi wapatao 1,467,107.

Kwa mijini, hadi mwezi Aprili, 2022 hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini ni wastani wa asilimia 86.5 ikilinganishwa na asilimia 86 ya mwezi Machi 2021.

Ongezeko hilo linatokana na kukamilika kwa ujenzi wa miradi 40 iliyohusisha ukarabati, upanuzi na ujenzi wa miradi mipya.

MAZINGIRA

# Ukame unavyowapa mtihani kusaka maji km. 10, wadai kukesha kisimani

• Tembo nao wahamia kwao 'kudowea'

**Na Maulid Mmbaga, aliyekuwa Mwanga**

KILIMAJARO ni kati ya mikoa nchini, inayokumbwa na tatizo ukame unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Waathirika hao kuna wilaya za Same na Mwanga, zinazoonekana kudhurika zaidi.

Bangalala, ni kati ya kata 34 zinazopatikana wilayani Same, ambako watoto na wanawake wanatajwa kuathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi, pale wanawake wanapotumia muda mrefu kutafuta maji na kuwaacha watoto bila ya uhakika wa chakula.

Nipashe ilizuru mahali hapo, kufika katika vyanzo vya maji, kukielezwa vitongoji vitatu katika kata hiyo. Kila kimoja kikikadiriwa kuwa na zaidi ya kaya 130, ikiwakuta kinamama wameketi kusubiri maji, katika nyuso za kukosa furaha.



Wanawake wakiwa wanasubiri maji katika kitongoji cha Makei. **PICHA ZOTE: MAULID MMBAGA**

### UHABA MAJI

Mama Upendo Kiango, anaiambia Nipashe kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi katika eneo lao umelazimisha watembee zaidi ya kilomita 10, kutafuta chemchem ambayo ni moja ya tegemeo lililobaki kwao.

Anatafsiri ukame ni hali inayosababisha vyanzo vya maji kukauka na kubakiwa na chemchem, pamoja na kisima kimoja pekee, vinavyohudumia wakazi wote, huku ikielezwa kiasi cha maji kinachotoka katika vyanzo husika hakikidhi mahitaji ya wakazi

"Tatizo la maji hapa kwetu limekuwa sugu kwa sababu ni la miaka mingi, tunatoka nyumbani saa 12:00 asubuhi tunatembea umbali mrefu kuja hapa kufuata maji, zaidi ya vitongoji vitatu vinategemea vyanzo viwili vya maji, watu ni wengi foleni na mahitaji ni makubwa kuliko kilichopo.

"Tuna watoto wadogo lakini tunalazimika kuwaacha wakati mwingine tunatumia zaidi ya masaa tisa mpaka 10 kurudi nyumbani kwa sababu maji yanayotoka ni madogo, dumu linaweza kuchukua hadi dakika 30 kujaa, ni tatizo pia kwa watoto tunaowaacha muda mrefu nyumbani," anaeleza Upendo.

"Kuna mwenzetu alikuwa anamuacha nyumbani mtoto wa miezi miwili na kutembea hadi huku kuja kutafuta maji, hali yake hairuhusu, lakini kutokana na shida iliyopo inambidi kufanya hivyo," anabainisha Upendo.

Issa Mashambo, anaunga mkono hoja, akisema chanzo hicho ni tegemezi kubwa kwao, hadi usiku watu wanakesha kusubiri maji pasipo kufanya shughuli za kuwaingizia kipato

"Katika eneo hili watu hawakauki kutokana na kwamba ni porini kumewekwa utaratibu wa kuwasha moto kwa ajili ya kujikinga baridi na wanyama wakali tukiwa tunasubiri maji nyakati za usiku.

> **Wake zetu wanatakiwa kuoga kila siku, lakini inawalazimu kumaliza zaidi ya siku mbili bila kuoga, kwa sababu maji hakuna, watoto wakati mwingine wanaenda shuleni na nguo chafu.**



Mwanakijiji, Upendo Kiango, akichota maji katika chemchem inayotegemewa na vitongoji vitatu katika Kata ya Bangalala, wilayani Same Mkoa Kilimanjaro.

"Wake zetu wanatakiwa kuoga kila siku, lakini inawalazimu kumaliza zaidi ya siku mbili bila kuoga, kwa sababu maji hakuna, watoto wakati mwingine wanaenda shuleni na nguo chafu," anasema Mashambo.

### MWENYEKITI KITONGOJI

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kirinjiko chini Nzia Mwarabu, anasema chanzo kimoja cha maji kisima kiko katika eneo lake, kimechimbwa kikiwa na kina cha mita 150, huku akisema uongozi wa eneo hilo uliachiwa jukumu la kuweka bomba na kwamba yaliyowekwa yana urefu mita 80, jambo linalosababisha maji kutoka kidogo.

Anaeleza kisima hicho kina zaidi ya miaka saba, lakini kutokana na bomba zilizowekwa fupi, zinasababisha mashine iliyowekwa kuvuta maji inaharibika kila mara na kuwa chanzo cha ugumu wa kupata maji kuongezeka, haya ikawalazimu kugeukia chemchem ya sasa.

"Tulishaita fundi kaja kupima, alituambia bomba zilizowekwa ni fupi ndiyo maana hazitoi maji inavyotakiwa, tumeshazitoa na tunasubiri siku watakapokuja kwa sababu hadi sasa hawajui kwamba tumeshalitambua hilo." anasema Mwarabu.

### TEMBO TATIZO

Ukame, zao la mabadiliko tabianchi, sasa yamesababisha baadhi yao kuhama kutoka hifadhini na kutembea maeneo mbalimbali hadi penye makazi ya watu na kusababisha uharibifu wa mazao na mali nyingine.

Saida Simba, mkazi wa Kitongoji cha Makei, anasema wanyama wamesababisha hofu kwa watoto wanaotembea wakati wa kwenda shule asubuhi na wakati mwingine hushindwa kutokana na kuwepo kwa tembo katika makazi hayo.

Pia, anataja imekuwa tatizo kwa wanawake waendao sokoni kutafuta riziki, kuna wakati mwingine wanalazimika kuchelewa kurejea nyumbani, wakisubiri tembo waondoke eneo wanakotakiwa kupita.

"Tatizo la wanyama hawa katika eneo hili limekuwa kubwa na la muda mrefu hadi watoto wa Chekechea wanakuambia 'wamewaona Tembo wakiwa wanaenda shule'. Hii inahatarisha usalama wao! Jana pia kuna 'wamama' walikuwa wanatoka sokoni, walishindwa kwenda nyumbani kwa sababu tembo walikuwa barabarani walikaa porini hadi saa mbili usiku wakisubiri waondoke ili warejee nyumbani," anasema Saida.

Charles Athumani, ni Katibu na Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kitongoji cha Makei, anasema zaidi ya miaka mitatu wanakabiliwa na njaa na wanapolima hawapati mazao kutokana na ukame, huku akilalamika hata kidogo wanachokipata, nacho kiko hatarini kuharibiwa na wanyama hao.

"Maliasili walisema watatoa elimu namna ya kuwafukuza, lakini hadi sasa hakuna chochote kilichofanyika. Hivyo, tunasisitiza watimize wajibu wao ili kuondokana na tatizo hili," anasema Athumani.

### JITIHADA SERIKALINI

Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo, anakiri tatizo kubwa la uhaba wa maji linalosababishwa na ukame, huku akibainisha mikakati inayofanywa na serikali kukabili changamoto hiyo, ni kutekelezwa Mradi wa Maji wa Same - Mwanga, ambao umefikia asilimia 90.

Anataja mradi mwingine ni uchimbaji visima, hasa katika ukanda wa tambarare kunakokabiliwa na tatizo kwa asilimia 40, akibainisha gharama, kwamba serikali imetoa Sh. milioni 500 kufanikisha utekelezaji huo.

Pia, Mpogolo anasema serikali imetoa Sh. bilioni moja kuwezesha miradi mbalimbali ya maji kukamilika, ili kutatua tatizo la maji katika maeneo ya ukanda huo. Hata hivyo, anakana dai kwa baadhi ya visima kuwekwa mabomba mafupi kama inavyodaiwa na baadhi ya wakazi.

"Visima vinapochimbwa ni lazima viwekwe bomba ambazo zinaendana na urefu wake, ndipo maji yapatikane. Hakiwezi kuwa na mita 150, halafu bomba zikawa na mita 80, jambo hilo haliwezekani na sio kweli.

Kuhusu makazi ya tembo, Mwenyekiti huyo wa Ulinzi na Usalama wilayani humo, anakiri uwepo wao, akieleza kwamba limekuwa tatizo kwa sababu wanawaharibia mazao yao.

Anasema halmashauri husika, zimeshafanya jitihada kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA), ikiwemo kuandaa kikosi kazi na kukipatia elimu watakayokwenda kuitoa kwa wananchi ambayo itawapa mbinu ya kuwafukuza wanyama hao pindi watakapowaona katika makazi yao.

MAZINGIRA

# Fedha za Uviko 19 zinavyogeuka msaada wa kuleta maji Bukoba




Tenki jipya la maji katika Halmashauri ya Bukoba. **PICHA ZOTE: LILIAN LUGAKINGIRA**

**Na Lilian Lugakingira,** Bukoba

UTEKELEZAJI miradi ya maji kwa fedha za Uviko 19, unatajwa umewasaidia wananchi kuondokana na adha ya maji, katika maeneo mbalimbali mkoani Kagera.

Miongoni mwa maeneo yaliyonufaika na fedha hizo yanatajwa kuwa ni kata ya Katoma, iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, yenye vijiji vitatu vya Irogelo, Kashenge na Rukindo.

Alicia James, mkazi wa Katoma, anasema hali ya upatikanaji maji kwa sasa ni nzuri, ikilinganishwa na siku za nyuma kabla ya kupelekewa mradi wa maji, maana walienda kuchota maji mtoni.

"Wakati mwingine tulirudi nyumbani usiku na kuna kipindi hasa cha kiangazi mito hukauka, ikitokea hali hii tunalazimika kwenda mbali zaidi katika vijiji vingine kufuata maji," anasema.

Mama huyo anatoa mfano, kwamba nyumbani anakoishi, kwenda mtoni, alitoka asubuhi na kuwasili mtoni saa moja asubuhi ukiwa ni mwendo mrefu, pia maji hayo waliyagombania na wanafunzi wanaoamka alfajiri kuyafuata.

Mkazi mwingine, Egbert Rweyemamu, kutoka kijijini Kashenge, anasema kwa sasa wamefarijika na wana amani, kutokana na mradi huo ujulikanao kama Kashenge - Irogelo, kuisaidia jamii wakiwamo kinamama, watoto, familia za wazee na kwenda mtoni na vijana wao.

> **Kwa hiyo, lazima jamii izingatie maelekezo na kutii sheria na miongozo yote inayotolewa, ili miradi iwe endelevu na vyanzo vya maji vilindwe.**



Kaimu Meneja wa RUWASA, mkoa Kagera, Mhandisi Patrice Jerome

"Mradi huu utawasaidia sana vijana, hasa wanaojishughulisha na shughuli za kilimo cha bustani za mboga na matunda, wapo wanaolima, lakini sio kwa ufanisi kutokana na kukosa maji ya kutosha ya kumwagilia bustani zao," anasema.

Rweyemamu anaeleza, kuwepo maji ya uhakika kunawaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo, pia itasaidia kukuza uchumi wa wananchi wa kata Katoma, maana muda waliokuwa wakiutumia kwenda mtoni watautumia katika shughuli za uzalishaji mali.

Mhandisi Patrice Jerome, Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mkoani Kagera, anasema miradi inayoendelea kutekelezwa kwa fedha za Uviko 19 katika mkoa iko saba.

Mhandisi Jerome anasema, miradi hiyo inatekelezwa katika wilaya sita zenye majimbo saba ya uchaguzi, ambayo ni Muleba Kusini, Muleba Kaskazini, Bukoba Vijijini, Nkenge, Ngara, Karagwe na Kyerwa.

"Miradi hii itagharimu zaidi ya shilingi bilioni 4.8, vitajengwa vituo vya maji 105, ambavyo kwa ujumla wake vinalenga kuwanufaisha wananchi 42,542. Ipo katika hatua mbalimbali na mingi ukiwamo wa kata Katoma (Kashenge -Irogelo) imekwishaanza kutoa maji" anasema.

Mhandisi Jerome anasema, miradi mitatu na utekelezaji wake umefikia asilimia 99, miwili asilimia 90 na iliyosalia, mmoja upo asilimia 86 na mwingine asilimia 75 na kwamba wanatarajia ifikapo mwanzoni mwa mwezi Novemba mwaka 2022, miradi yote iwe imekamilika kwa asilimia 100.

Anasema, katika kutekeleza miradi hiyo, walikumbana na baadhi ya matatizo, ikiwamo kiwanda kilichopewa kazi ya mabomba kutokamilisha kwa wakati na kusababisha kazi hiyo kuhamishiwa katika kiwanda kingine, hali iliyochangia ucheleweshaji miradi.

"Inaendelea kukamilishwa, pia makandarasi walikumbwa na matatizo ya mitaji ya fedha, ushauri wangu kwao wasiwe na tamaa, waombe miradi kulingana na mitaji yao, hii itawasadia kujenga majina yao na kupata fursa nyingine inapoletwa miradi mingine," anasema.

Kuhusu uendeshaji miradi, Mhandisi Jerome anasema kuwa itaendeshwa katika miradi mingine ya vijijini iliyopo chini ya RUWASA, inayosimamiwa na vyombo vya watoa huduma ngazi ya jamii ambavyo vimeundwa katika miradi hiyo saba.

Anasema, vyombo hivyo vitasimamia huduma hiyo kwa kuzingatia Sheria ya Maji Namba Tano ya mwaka 2009, ambayo ndiyo inaunda vyombo hivyo na imetoa kanuni za uendeshaji, ili miradi iweze kuendelea.

"Wito wangu kwa wananchi, watoe ushirikiano katika kulinda miundombinu ya maji iliyojengwa kupitia fedha za Uviko 19 kama ilivyo kwa miradi mingine, maana usalama wa miradi yote upo mikononi mwao.

"Kwa hiyo, lazima jamii izingatie maelekezo na kutii sheria na miongozo yote inayotolewa, ili miradi iwe endelevu na vyanzo vya maji vilindwe," anasema.

Aidha. Anafafanau kwamba ili miradi ya maji iweze kujiendesha, ni lazima huduma hiyo ilipiwe kwa viwango elekezi ambavyo vimetolewa na serikali kwa kuzingatia teknolojia ya mradi na kwamba, maji yanayosukumwa kwa umeme ndoo moja yenye ujazo wa lita 20, itanunuliwa kwa shilingi 40 na miradi ya mserereko ndoo moja ni shilingi 20.

Anatoa wito kwa wenye jukumu la kusimamia miradi hiyo kutoingiza siasa katika usimamizi, na kwamba Rais Samia Suluhu Hassan, akitahadharisha hakuwapatia miradi hiyo waitumie kupotosha umma, bali kuunga mkono jitihada zake, ili miradi hiyo inufaishe vizazi vya sasa na vijavyo.

Anataja mwongozo wa kiserili uliopo, unalenga kuongeza kasi ya usambazaji majisafi na salama, ili kutosheleza mahitaji kwa zaidi ya asilimia 85 vijijini na zaidi ya asilimia 95 kwa mijini kwa upande wa Tanzania Bara, ifikapo 2025.





# Mahakama yatupa shauri la watoto kupinga mama kusimamia mirathi

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kyela, imetupilia mbali shauri la madai ya kupinga mgawanyo wa mirathi lililofunguliwa na watoto watatu wa kambo wa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Marehemu John Mwakipesile, wakidai kutoridhishwa na mchakato wa kumpata msimamizi wa mirathi ya baba yao.

Watoto hao walifungua shauri hilo Septemba 9, mwaka huu, dhidi ya mke wa Marehemu, Bupe Mwakipesile ambaye aliteuliwa na familia kuwa msimamizi wa mirathi ya mumewe wakidai kuwa hawana imani naye.

Katika madai yao ya msingi watoto hao ambao ni Nsajigwa Mwakipesile, maarufu Bony, Jesca Mwakipesile na Hilda Mwakipesile, waliomba Mahakama ya Wilaya kupitia upya mchakato wa kumpata msimamizi wa mirathi ya baba yao na kwamba huyo aliyeteuliwa hawana imani naye.

Watoto hao waliwakilishwa na Wakili Aikande Lema, huku upande wa utetezi ukisimamiwa na Wakili Hashim Mziray, kutoka jijini Dar es Salaam.

Mahakama baada ya kusajili kesi hiyo ilipanga kuanza kuisikiliza jana, mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kyela, Andrew Njau kwa kupokea hoja za pande zote mbili.

Hata hivyo, walalamikaji pamoja na wakili wao, hawakufika mahakamani kusikiliza shauri hilo bila kutoa taarifa.

Wakili wa Utetezi Hashim Mzirai, akisoma kifungu cha 95 kifungu kidogo cha 33 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa wa Madai, aliiomba mahakama kuondoa shauri hilo mahakamani kwa madai kuwa kitendo cha walalamikaji pamoja na wakili wao kutofika mahakamani bila taarifa ni kuisumbua mahakama.

Aidha, Wakili Mziray aliiomba mahakama kuwataka walalamikaji kulipa gharama za uendeshaji wa kesi hiyo, kwa madai kuwa wamesababisha usumbufu na hasara kwa wateja wake.

Akitoa uamuzi wa mahakama, Hakimu Njau alikubaliana na hoja ya upande wa utetezi na kuridhia kuiondoa kesi hiyo mahakamani kwa kutumia kifungu cha 95 (33) bila uwapo wa walalamikaji.

Baada ya uamuzi huo, wakili wa utetezi Mziray aliishukuru mahakama kwa kuwatendea haki wateja wake akidai kuwa walalamikaji hawakuwa na hoja za msingi kwenye madai yao.

Alidai hata kama walalamikaji wangejitokeza mahakamani hapo alikuwa amejiandaa kwa hoja nzito za kisheria.

"Kimsingi kesi hii imeondolewa mahakamani, kwa sababu walalamikaji hawakutokea, lakini hata kama wangekuja tulijiandaa kwa hoja nzito za kisheria kukabiliana nao, maana hili suala halikuwa na umuhimu wa kuletwa mahakamani, lingeweza kutatuliwa hata kwenye ngazi ya familia, namshukuru hakimu kwa kutenda haki maana mahakamani sio mahali pa kutelekeza kesi," alidai Wakili Mziray.

Kwa upande wake, mtoto mkubwa wa marehemu, Sekela Mwakipesile aliishukuru mahakama kwa uamuzi huo akidai kuwa baada ya kufunguliwa kwa kesi hiyo mahakamani, mama yake alikuwa akifika mara kwa mara mahakamini kuhudhuria kesi hiyo, lakini walalamikaji hawakuhi kujitokeza.

Mwakipesile alifariki Mei, mwaka huu wilayani Kyela kwa ugonjwa wa shinikizo la damu na kuzikwa nyumbani kwao Kijiji cha Kapamisya, wilayani hapo.



Chifu Mkuu wa Kabila la Wasafwa mkoani Mbeya, Rocketi Mwashinga, akisisitiza umuhimu wa utunzaji wa vyanzo vya maji katika safu za Mlima Mbeya, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanaisumbua dunia kwa sasa, kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Ihombe wilayani Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Wananchi wasalimisha silaha 20 walizomiliki kinyume

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya silaha za moto 20 zilizokuwa zinamilikiwa na wananchi kinyume cha sheria mkoani hapo, zimesalimishwa kwenye vituo mbalimbali vya polisi na ofisi za serikali mkoani humo katika kipindi cha miezi miwili.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, aliyasema hayo jana alipozungumza na wandishi wa habari ofsini kwake kuhusu operesheni mbalimbali zilizofanywa na jeshi hilo.

Alisema wananchi hao wamesalimisha silaha hizo baada ya jeshi hilo kutoa miezi miwili kabla operesheni ya kuwasaka na kuwachukulia hatua haijaanza.

Kamanda Kuzaga alisema baadhi ya silaha zilizosalimishwa zimetengenezwa kienyeji na wananchi na baadhi zilikuwa zinatumika kwenye matukio ya uhalifu ikiwamo uwindaji haramu na ujambazi.

"Muda wa kusalimisha kwa hiyari umekwisha na hizi ndizo zilizosalimishwa, kwahiyo tutaanza operesheni muda sio mrefu wa kuwasaka wote wanaoendelea kuzimiliki ili tuwachukulie hatua za kisheria," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema wametumia mbinu mbalimbali za kuhamasisha wananchi kusalimisha silaha hizo na kwamba kazi hiyo ilikuwa ni utekelezaji wa agizo lililotolewa na serikali mwezi Septemba.

Katika hatua nyingine, Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo linamshikilia mtu mmoja aitwaye Mwinyiheri Kitalima (32) mkazi wa Magwalisi wilayani Mbarali kwa tuhuma za kukutwa na nyara za serikali ambazo ni meno mawili ya tembo.

Alisema meno aliyokutwa nayo kijana huyo yana uzito wa kilogramu 42 na kwamba alikuwa ameyahifadhi nyumbani kwake na kwamba operesheni za kuwasaka wengine wanaofanya vitendo hivyo zinaendelea.

Kamanda Kuzaga alisema mtuhumiwa huyo ameshafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria kwa kushirikiana na vyombo vingine.

# Wakazi Mbeya waanza kuonja machungu mgawo wa maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya wakazi wa Jiji la Mbeya wameanza kukabiliwa na mgawo wa maji kutokana na uzalishaji wa maji kutoka chanzo cha Mlima Mbeya kushuka kutoka lita 9,000 kwa siku hadi 3,000.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya UWSSA), imesema hali hiyo imesababishwa na uharibifu wa mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS), Mkoa wa Mbeya katika kijiji cha Ihombe wilayani Mbeya, Ofisa Uhusiano wa Mbeya UWWSA, John Nkana, alisema uzalishaji wa maji katika chanzo hicho umeshuka kwa zaidi ya asilimia 75 na kusababisha baadhi ya maeneo ya pembezoni mwa jiji la Mbeya kukosa maji.

Aliyataja baadhi ya maeneo ambayo yameathirika kwa kukosa au kupata maji kwa mgawo kuwa ni vijiji vya Idugumbi, Ihombe na Mamlaka ya Mji Mgogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya pamoja na maeneo ya Iwambi, Itende na Iziwa yaliyoko katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Nkana alisema upungufu huo wa maji kwa kiwango kikubwa unasababishwa na shughuli za kibinadamu zinazoendelea kufanyika kwenye vyanzo vya maji, hususan kilimo cha umwagiliaji kunachofanyika bila kuzingatia sheria.

"Tumefuatilia na kubaini kuwa kuna shughuli za kilimo zinafanyika kwenye vyanzo vya maji, watu wanachepusha maji kabla ya kufika kwenye banio letu, na kusababisha kiwango cha maji kinachoingia kwenye banio kuwa kidogo kulingana na matarajio yetu, hali hii ndiyo inasababisha maji yapatikane kwa mgawo katika baadhi ya maeneo yanayotegemea kupata maji kutoka kwenye chanzo hicho," alisema Nkana.

Ofisa Mhifadhi Mkuu wa TFS Wilaya ya Mbeya, Eunice Mbilinyi, alisema kumekuwapo na ukiukwaji mkubwa wa sheria za uhifadhi miongoni mwa wananchi wanaoingia bila kibali ndani ya hifadhi ya safu za Mlima Mbeya na kufanya shughuli za kibinadamu.

Alisema sheria hairuhusu mtu yeyote kuingia ndani ya hifadhi bila kibali, lakini baadhi ya watu wanapokamatwa wakiwa huko wanalalamika kuwa wanaonewa.

"Niwakumbushe tu kwamba sheria za uhifadhi zipo pale pale, haturuhusu mtu yeyote kuingia wala kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya misitu yetu," alisema Mbilinyi.

Wazee wa mila maarufu 'machifu', waliiomba serikali kuwashirikisha katika suala la kuhifadhi mazingira ili watumie nafasi zao kuwadhibiti watu wanaoingia ndani ya misitu na kufanya uharibifu.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alitoa siku tano kwa watu wote wanaofanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji vilivyo ndani ya hifadhi za TFS kuondoka mara moja kabla hatua kali hazijachukuliwa dhidi yao.

"Natoa maelekezo kwamba yeyote ambaye ana shamba lililo ndani ya hifadhi ya TFS ikiwa ameshalima, basi asipande, ikiwa ameshapanda basi asipalilie ili asipate hasara, kuanzia sasa natoa siku tano tu, wote walio huko waondoke kabla serikali haijawaondoa kwa nguvu," alisema Dk. Chuachua. Uharibifu wa mazingira pamoja na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamesababisha ukame wa muda mrefu vimechangia uwepo wa uhaba wa maji kwenye vyanzo vya maji vinavyohudumia Jiji la Mbeya na kupelekea wananchi kupata maji kwa mgawo.



# NBS yafafanua takwimu za sensa zilizotangazwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) imesema idadi ya watu 61,741,120 iliyotangazwa mwanzoni mwa wiki hii na Rais Samia Suluhu Hassan ni ya watu wote waliolala nchini usiku wa kuamkia siku ya sensa bila kujali utaifa wao.

Vilevile, ofisi hiyo imesema kwa sasa inaandaa chapisho ambalo litatolewa Machi 2023 likionyesha idadi kamili ya Watanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo juzi, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema uchambuzi wa kina unaendelea ili kubaini watu waliolala nchini na utaifa wao.

"Machi mwakani tutatoa chapisho lingine litakalokuwa linaeleza Watanzania ni wangapi katika idadi hii ya 61,741,120, litabainisha idadi ya watu kulingana na utaifa wao.

"Matokeo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan ni ya mwanzo, ikumbukwe kuwa dodoso la sensa lilikuwa na maswali 100, hivyo zitatolewa awamu kwa awamu na kwa namna tofauti," alisema.

Dk. Chuwa alisema kuwa matokeo ya mwanzo yatafuatiwa na taarifa nyingine za kijamii, kiuchumi, kidemografia na mazingira huku machapisho mengine yakiendelea kutolewa kadri muda unavyokwenda kulingana na ratiba ya utoaji wa matokeo ya sensa.

Alisema kwa sasa wanaendelea kuandaa chapisho ambalo litatoka Desemba mwaka huu likionyesha mgawanyo wa watu wote nchini kiumri kwa ngazi zote.

Alisema chapisho hilo litabainisha vijana wako wangapi kwa sera ya nchi ya vijana, idadi ya watoto na wazee.

"Hili ni chapisho ambalo lazima litoke Desemba mwaka huu na baada ya hili ndipo tutatoa chapisho ambalo linaelezea Watanzania wako wa ngapi," alisema.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi 2022 Zanzibar, Balozi Mohmed Haji Hamza, alisema katika uchambuzi wa matokeo ya mwanzo uwiano wa watu kijinsia kwa Tanzania Bara na visiwani ni wanaume 95 kwa kila wanawake 100 huku mikoa ya Manyara na Kusini Unguja ikionyesha kuwa na idadi kubwa ya wanaume kuliko wanawake.

Alisema hali hiyo kwa mikoa husika huenda imesababishwa na uhamaji wa wanawake kwenda mikoa mbalimbali kwa ajili ya kujitafutia kipato kwa ajili ya kumudu maisha yao.

"Kusini Unguja ambako shughuli kuu ni utalii, inawezekana ndiyo chanzo cha kuwa na wanaume wengi zaidi kuliko wanawake, haya ni mawazo ambayo yanahitaji kufanya utafiti wa kina utakaobainisha sababu kwa ajili ya kuweka mipango sahihi kwa wananchi wa maeneo husika," alifafanua.

Balozi Hamza alisema ongezeko la idadi ya watu nchini kutoka mwaka 2012 hadi 2022 ni wastani wa asilimia 3.2 kwa mwaka.

Alisema taarifa zinazosambazwa mitandaoni zinazoonyesha wastani wa ongezeko la idadi ya watu ni asilimia 3.7 zipuuzwe na sio sahihi.

"Kwa idadi hii ya watu ya 61,741,120 ya mwaka huu na matokeo ya sensa ya mwaka 2012, Tanzania ilikuwa na watu 44,928,923 hii ni dhahiri kuwa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, idadi ya watu imeongezeka kwa watu 16,812,197," alifafanua.

## NMB yatoa msaada kwa wenye ulemavu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BENKI ya NMB Kanda ya Kati imetoa msaada wa vitu mbalimbali kwa ajili ya watu wenye ulemavu zikiwamo kofia na mafuta kwa ajili ya watu wenye ualbino yatakayosaidia kuwalinda dhidi ya mionzi inayosababisha saratani ya ngozi.

Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, akikabidhi vitu hivyo kwa mwenyekiti wa shirika lisilo la kiserikali la Foundation for Disabilities Hope (FDH), alisema msaada huo ni sehemu ya kurudisha fadhila kwa jamii.

Alisema kuwa katika msaada huo, wametoa vitu muhimu kwa ajili ya watu wenye ulemavu vitakavyowasaidia kupunguza baadhi ya kero ambazo wanakumbana nazo kila siku.

"Kwenye msaada huu tunaokabidhi leo (juzi) tumetoa fimbo kwa ajili ya watu wasioona ambazo watazitumika kuwasaidia katika harakati zao mbalimbali za kila siku.

"Lakini tumetoa kofia kwa ajili ya watu wenye ualbino ili kuwakinga na jua kali la Mkoa wa Dodoma na kuwaondoa katika hatari ya kupata saratani ya ngozi, pia tumewapatia mafuta maalum kwa ajili ya ngozi yao," alisema Mlozi.

Mwenyekiti wa Shirika la FDH, Michael Salali, aliishukuru benki hiyo kwa msaada huo, akisema umetolewa wakati mwafaka.

Salali alisema watu wenye ulemavu wanakabiliwa na kero mbalimbali ambazo zinahitaji wadau kuwaunga mkono ili kuzimaliza.

"Tunashukuru sana NMB kwa kutukumbuka kwa msaada huu ambao utasaidia watu wenye ulemavu zikiwamo kofia na mafuta haya kwa ajili ya watu wenye ualbino ambao kutokana na jua kali la Mkoa wa Dodoma wapo hatarini kupata saratani ya ngozi," alipongeza.

Alitoa wito kwa wadau wengine kujitokeza kutoa misaada kama hiyo kwa watu wenye ulemavu ili kuwapunguzia shida zinazowakabili.

Dk. Peter Chota, Bingwa wa Magonjwa ya Ngozi, alisema msaada huo utawasaidia watu wenye ualbino kulinda ngozi zao kutokana na jua kali la Mkoa wa Dodoma.

"Changamoto kubwa kwa watu wenye ulemavu mkoani hapa ni jua kali. Kofia hizi pamoja na mafuta vitasaidia kulinda ngozi zao na saratani ya ngozi," alisema.




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Mind Garden, Sumaiya Mahmoud (kulia), akizungumza na kijana, Faridi Haruna, baada ya kumaliza kuwapa elimu kuhusu afya ya akili kwa vijana waliokuwa wakiishi katika kituo cha kulelea watoto yatima cha Ijango Zaidia Orphanage, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MV Mwanza kuanza kutoa huduma Julai

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesema Meli ya MV Mwanza inatarajia kukamilika ifikapo Mei 2023 kisha kuanza kutoa huduma kwa wananchi Julai mwakani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni za Meli (MSCL), Eric Hamissi, alibainisha hayo juzi jijini hapo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mwelekeo wa taasisi hiyo na utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu.

Alisema hadi sasa ujenzi wa meli hiyo umefikia hatua nzuri na mwezi huu itaingizwa katika maji kwa ajili ya ujenzi wa vitu vya ndani na kujaribu injini kama iko vizuri.

"Tunatarajia hadi kufikia Mei 5 mwakani, meli hiyo ikabidhiwe na ikifika Julai mwakani, ianze kutoa huduma. Meli hii ni kubwa kuliko meli zote zinazoelea katika maziwa makuu. "Kukamilika kwake italeta mapinduzi makubwa katika sekta ya usafirishaji wa njia ya maji kwa sababu itakwenda Uganda, Kisumu, Bukoba na maeneo mengine ambapo kutakuwa na biashara," alisema.

Alisema meli hiyo itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo na ina urefu wa mita 92.6 na upana mita 17 na ina ghorofa nne.

Hamissi alisema katika mwaka huu wa fedha, serikali imeipatia MSCL Sh. bilioni 111.8 kwa ajili ya kukarabati, kuendeleza na kujenga meli 11. Alisema fedha hizo zitakarabati meli tatu na kuanza ujenzi wa meli mpya nne, lengo likiwa kumaliza shida ya usafiri kwa njia ya maji.

Alisema katika mwaka huu wa fedha, serikali imetenga Sh. bilioni 53 kwa ajili ya kutekeleza miradi saba iliyoko Ziwa Tanganyika.

"Serikali imeona ni vyema kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika Ziwa Tanganyika, ikitoa Sh. bilioni 53.9 kwa ajili ya kujenga chelezo ya tani 5,000 itakayogharimu Sh. bilioni 12 kwa sababu zitajengwa meli kubwa za mizigo na kontena kubwa ambazo zitavushwa kupelekwa Zambia na DR Congo.

Pia alisema katika mwaka huu, watajenga meli mpya ambayo itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo ambayo itajengwa kwa miezi 24 na itagharimu Sh. bilioni 70.



# Jamii yatakiwa kujenga utamaduni kuchangia damu

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

KATIKA kuokoa maisha ya wagonjwa, jamii imetakiwa kuwa na utamaduni wa kuchangia damu ili kuokoa maisha ya watu hao.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation, Mariyam Mwinyi, mke wa Rais wa Zanzibar, wakati wa uzinduzi wa kambi ya matibabu ya macho, chumba maalum cha matibabu kwa viongozi mashuhuri katika Hospitali ya Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) Kibweni.

Akisoma hotuba yake, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema huduma ya damu ni muhimu kwa wagonjwa hasa wajawazito na uamuzi wa kikosi hicho ni wa kupongezwa kwa sasabu wanaunga mkono juhudi za serikali katika huduma za afya.

Alisema hatua ya kikosi hicho kuleta madaktari bingwa wa maradhi mbalimbali yakiwamo ya moyo itasaidia upatikanaji wa huduma ya matibabu kwa wananchi bila malipo. "Ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Dk. Hussein Ali Mwinyi, hospitali hii imepiga hatua upande wa huduma za afya kwa wananchi hali inayothibitisha uzalendo wa watendaji na viongozi wa kikosi hiki," alisema Mariam.

Aidha, aliwapongeza madaktari bingwa wa macho kutoka Shirika la Puma Vision la Ujerumani kwa kuiunga mkono serikali na hospitali hiyo kwa kutoa matibabu kwa wananchi bila ya malipo.Naye Mkuu wa KMKM, Komondoo Zan Hassan Msingiri, alisema kikosi hicho kinaendelea kuimarisha huduma kila mwaka ikiwamo kuimarisha majengo ya kutolea huduma, vifaa tiba na kuimarisha huduma za matibabu.

Alisema kikosi hicho kinaendelea kuwasiliana na madaktari kutoka nchi za India na Ujerumani kuisaidia Hospitali ya KMKM ili kutoa matibabu bora kwa wananchi.

Akisoma taarifa ya hospitali hiyo, Dk. Hussein Khamis Othman, alisema huduma za matibabu zimeongezeka zikiwamo za upasuaji, afya ya uzazi hali iliyoongeza idadi ya wagonjwa kutoka 7,600 mwaka 2020 hadi wagonjwa 9,000 mwaka 2021.

"Ubora wa huduma tunazotoa umeongeza wagonjwa hadi sasa hospitali inapokea wastani wa 200 hadi 320 kwa siku na kusababisha changamoto ya ufinyu wa maeneo ya kutolea huduma, vifaa tiba na watoa huduma wakiwamo madaktari," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Puma Vision anayeongoza timu ya madakari wa macho kutoka Ujerumani, Dk. Frank Klemn, alisema wataendelea kushirikiana na KMKM kutoa matibabu ya maradhi mbalimbali ili kuwasaidia wananchi kupata huduma bora.



Baadhi ya watalii wakiwa kwenye bwawa la kuogelea katika hoteli yenye mandhari nzuri ya Michamvi, Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kamisheni Ardhi yaridhishwa ushiriki wananchi Jambiani

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHENI ya Ardhi Zanzibar kupitia kitengo cha utambuzi wa ardhi imeeleza kuridhishwa na ushiriki wa wananchi wa kijiji cha Jambiani Kibigija katika zoezi la uhakiki wa majina maeneo ambayo yamefanyiwa utambuzi.

Akizungumza jana wakati wa uondoaji wa bango la kuhakiki majina (public display), Jambiani Mkoa wa Kusini Unguja, Mratibu utambuzi wa ardhi kutoka Kamisheni hiyo, Kauthar Kamal Basha, alisema hatua hiyo inaonesha wananchi kutambua umuhimu wa zoezi hilo litakalowawezesha kupata hati ya haki ya matumizi na umiliki wa ardhi. Alisema hatua hiyo pia ni miongoni mwa utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Zanzibar aliyetaka taasisi hiyo kuhakiki na kutambua maeneo yote ya Zanzibar na kuyapatia hati kwa lengo la kumaliza migogoro ya ardhi.

"Kwa sasa tupo katika zoezi la uondoshaji wa bango ambalo tuliliweka kwa muda wa miezi mitatu ili wananchi waweze kuhakiki majina yao kwa shehia ya Jambiani ambapo wameonekana kutekeleza agizo hilo," alisema.

Aidha, alisema baada ya uondoshaji wa bango la majina hatua inayofuata ni utengenezaji wa hati kwa maeneo yote yaliyotambuliwa.

Kwa upande wake Sheha wa shehia ya Jambiani Kibigija, Sinatama Makame Haji, alieleza kuridhishwa na uhakiki uliofanywa kwa kuweka hadharani bango la uhakiki wa majina yao na kila mwananchi kuwa na uhakika jambo ambalo litaepusha uzoroteshaji wa kiutendaji.

"Naipongeza serikali kuendeleza mpango huu ambao utaondoa malalamiko yanayoweza kujitokeza hasa katika umiliki halali wa eneo pamoja na usahihi wa jina la mmiliki," alisema Sheha huyo.

Baadhi ya wananchi wa shehia hiyo waliipongeza serikali na uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa kuendesha zoezi hilo kwa uwazi na kujiridhisha uhalali wa maeneo yao na usahihi wa majina yao.

Uondoaji wa bango la uhakiki umetokana na Kamisheni hiyo kufanya utambuzi katika maeneo mbalimbali ya Unguja yakiwamo ya Meya katika wilaya Mjini na Jambiani Kibigija, wilaya ya Kusini Unguja, majina hayo yalikaa kwa siku 90 na hatua inayofuata ni utengenezaji wa hati za umiliki wa ardhi na maeneo yaliyotambuliwa.

# AAFP yatoa ushauri Serikali ya Muungano kuhusu mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wakulima (AAFP), kimeishauri Serikali ya Muungano kuzingatia maelezo yaliotolewa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuhusu ugumu wa kukosa mikopo toka taasisi za fedha kimataifa.

Kimesema endapo kasoro hiyo na nyingine hazipatiwa ufumbuzi wa mapema na dawa ya kudumu Muungano utatikisika.

Hayo yameelezwa jana Mjini Zanzibar na Mwenyekiti wa AAFP, Said Soud Said wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema njia pekee bora ili mambo yaende sawa ni kufanyika marekebisho changamoto zinazolalamikiwa kwa muda mrefu na upande mmoja wa Muungano.

Soud alisema njia muafaka ni kusikiliza maoni ya wananchi yanayotolewa kwa miaka kadhaa kabla Rais Samia Suluhu Hasssan, hajashika madaraka ikiwamo kusuasua utekelezaji wa matakwa yalioainishwa katika ripoti ya pamoja ya Kamisheni ya Fedha ya Muungano (JFC).

Alisema siku zote kutibu mapema jeraha ni juhudi za kukinusuru kidonda kisigeuke na kuwa saratani isiyotibika haraka na kumsababishia mgonjwa kupoteza maisha kwa uzembe wa kuficha maradhi.

"Madai ya Rais Dk. Mwinyi kuhusu SMZ kushindwa kukopa taasisi za fedha za kimataifa yasipuuzwe. Lazima kipengele hicho kirekebishwe kabla mambo hayajaenda arijojo. Njia pekee ni kutekeleza matakwa ya kamisheni ya pamoja ya fedha ili kuupa ustawi Muungano," alisema Soud.

Alisema licha ya AAFP kuunga mkono muundo wa serikali mbili, lakini bila kushughukiliwa malalamiko ya msingi katika uso wa Muungano changamoto zake zitaendelea kujitokeza na hazitamalizika.

"Ni kweli Zanzibar haiwezi kukopa kwenye taasisi za fedha za kimataifa kwa kuwa si nchi dola. Dola ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Basi hata kipengele cha kukopa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Zanzibar na watu wake kuwe na vizingiti?" Alihoji.

Hivi karibuni Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi alisikika akisema wakati alipokutana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stegomena Tax, na kuelezea ugumu wa SMZ kushindwa kukopa katika taasisi za kimataifa kwa kuwa si dola.

Aidha, AAFP kimeishauri Serikali ya Tanzania kuitambua hadhi ya Zanzibar na nafasi yake kama nchi mshirika iliyounda Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kuzaliwa Taifa la Tanzania Aprili 26, 1964.

"Kuungana kwa Zanzibar na Tanganyika ndiko kulikosababisha lipatikane taifa jipya la Tanzania lenye kukaribia miaka 60. Katika Muungano huo hakuna mdogo wala mkubwa. Wanachama wote wana haki sawa. Lazima kila upande ufaidike na matunda ya Muungano," alisisitiza.

Hata hivyo, alisema hakuna sababu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kukwepa ukweli huo badala yake kinachotakiwa kufanyika ni kuondoa kasoro zote bila kukwepa ukweli wa madai ya wananchi wa Zanzibar na kufikia utatuzi wa kasoro za msingi.

# Maofisa ustawi wafundwa kukabili ukatili kwa watoto

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

MAOFISA ustawi wa jamii mkoani hapo wameanza kupokea mafunzo kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto wa shule za msingi, sekondari na wa mitaani.

Mafunzo hayo yanayofadhiliwa na Shirika la Plan International yanajumuisha maofisa ustawi wa jamii, maofisa maendeleo ya jamii, ofisa elimu na maofisa dawati la jinsia yakiwa na lengo la kuwanusuru watoto dhidi ya vitendo vya kikatili ndani na nje ya shule.

Akifungua mafunzo hayo juzi, Kaimu Katibu Tawala, Utawala na Rasilimali watu Mkoa wa Mwanza, Daniel Machunda, alisema kuwa serikali imeunda kamati 1,106 zenye wajumbe 27,650 za Mpango kazi wa taifa wa mkakati wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) zikiwa na lengo la kutekeleza shughuli za ulinzi wa mtoto.

Alisema mkoa unafanya jitihada kutekeleza mpango kazi wa MTAKUWWA na kuielimisha jamii kufahamu umuhimu wa kushiriki kwenye shughuli za maendeleo yakiwamo masuala ya jinsia.

"Leo tumepata fursa ya kuongeza uelewa wa namna bora ya kushughulika na watoto nichukue fursa hii kuwashukuru Plan International kwa jinsia walivyoshirikiana na serikali kuanzia ngazi ya wizara na mkoa na wadau wengine kuzidi kuwekeza katika masuala ya watoto kwani yana matatizo mengi yanayotakiwa kuchukuliwa hatua mapema," alisema Machunda.

Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu (Idara ya Maendeleo ya Mtoto), ambaye ni mwezeshaji wa mafunzo hayo, Aurelia Msanga, alisema kupitia usimamizi mzuri wa sera, wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wana jukumu la kuhakikisha wanamlinda mtoto dhidi ya vitendo vya ukatili.

Tayari tumeandaa miongozo miwili ambayo ni uanzishwaji wa dawati pamoja na ulinzi na usalama wa mtoto ndani na nje ya shule ambayo yataanzishwa kwa ajili ya kushughulikia na kuzuia vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

"Madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto ni majukwaa yanayoanzishwa katika shule za msingi na sekondari pengine mtoto anaweza kuwa amekutana na ukatili nyumbani ama popote akakosa sehemu ya kufikisha hizo taarifa kwa hiyo kupitia haya mabaraza mtoto anaweza kufikisha hizo taarifa," alisema. Aliongeza kuwa kuanzishwa kwa madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto ndani na nje ya shule kutapunguza vitendo vya ukatili kwa kuwa wamegundua watoto wengi wanafanyiwa vitendo vya ukatili ndani na nje ya shule, lakini wanakosa sehemu husika ya kwenda kupeleka matatizo yao kupitia hayo madawati watoto watafundishwa namna ya kupeleka taarifa. Naye mshiriki wa mafunzo hayo Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Kayenze Ilemela, Matula Mgeta, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kupambana na kupunguza vitendo vya ukatili ambavyo vinaendelea kwenye maeneo ya shule na mitaani na jukumu la serikali ni kuendelea kuyasimamia mabaraza yatakayoundwa.

Alisema wanapokea matukio mengi katika maeneo yao ikiwamo kutowapeleka watoto shule, wa kike kupata mimba, vipigo na vitisho hasa kwenye maeneo ya familia. Aidha, Ofisa Maendeleo Mwandamizi Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Ilemela, Sara Nthangu, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa sababu ni miongozo ya serikali, yanaongeza weledi na uwezo wa wataalamu kuweza kutoa huduma stahiki kwa watoto.




Makamu Mkuu wa Chuo cha Mtakatifu Augustine (SAUT), Balozi Prof. Costa Mahalu (kulia), akipokea mkataba wa makubaliano ya program ya mafunzo kwa vitendo kutoka kwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Generation Empower, Joshua Naiman, jijini Mwanza juzi, unaolenga kuwajengea uwezo wanachuo 5,000 kwa mwaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waiomba serikali kusitisha usafirishaji mazao nje

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya wakazi wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kusitisha utoaji wa vibali vya kusafirisha mazao ya chakula nje ya nchi kutokana na hofu ya taifa kukabiliwa na baa la njaa.

Walibainisha hayo juzi kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na gazeti hili kuwa wamepokea kwa mshtuko taarifa ya uchache wa mvua katika msimu huu wa kilimo huku wakitambua uliopita mazao hayakupatikana ya kutosha.

Samwel Wilson, mkazi wa Busoka Manispaa ya Kahama, alisema, vyakula vichache ni matokeo ya kupanda kwa gharama za maisha, hivyo kuwa na mashaka zaidi endapo taifa litaendelea kutoa chakula nje na kusababisha upungufu wa chakula hicho nchini.

Alisema, gharama za vyakula sokoni zimekuwa zikiongezeka kila siku na wasiokuwa na uwezo kulazimika kupata mlo mmoja kwa siku na kulalamika kuwa kuruhusu chakula kuuzwa nje kutaleta athari baadaye. Naye Johari Mbaraka, Mkazi wa Kata ya Majengo alisema, upo umuhimu wa serikali kudhibiti vibali vya kusafirisha mazao nje ya nchi kwa mustakabali wa wananchi wake kwa kuwa wataalamu wa hali ya hewa tayari wametoa tahadhari ya uwapo wa mvua chache msimu huu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliwataka wananchi kuandaa mashamba yao mapema ili kuwahi kiwango cha mvua kitakachotokea kutokana na tahadhari iliyotolewa na wataalamu wa hali ya hewa ya kuwapo mvua chache katika msimu huu. Aliwataka kuandaa mazao yenye uwezo wa kustahimili hali ya ukame yatakayosaidia kukabiliana na baa la njaa ambalo kwa sasa limeanza kutishia taifa kulingana na hali ya upatikanaji wa mvua ikiwa finyu huku bidhaa zikizidi kupanda bei.

# Madiwani waishukia TANESCO umeme kukatika ovyo

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MADIWANI wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, wamemjia juu Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Shinyanga, Mhandisi Grace Ntungi, kuhusu kukatika nishati hiyo mara kwa mara.

Madiwani hao walifikia hatua hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha kawaida cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha (2022/2023), wakati taasisi za serikali zilipokuwa zikiwasilisha taarifa zao za utekelezaji wa miradi kwenye baraza hilo.

Diwani wa Viti Maalum, Zuhura Waziri, alisema tatizo la kukatika kwa umeme katika Manispaa ya Shinyanga limekuwa kero, pamoja na kushusha heshima ya viongozi kwa wananchi kuwa wameshindwa kuwajibika kutatua tatizo hilo.

"Naiomba serikali iangalie utaratibu kuwapo na shirika mbadala ambalo litaisaidia TANESCO utoaji wa huduma bora kwa wananchi, kama ilivyo kwenye maji ambapo iliongezwa RUWASA na barabara ikawekwa TARURA," alisema Waziri.

Naye Reuben Kitinya, Diwani wa Kizumbi, aliliomba shirika hilo kutoa taarifa maalum endapo ukatikaji wa umeme ni sehemu ya mgawo wafahamu mapema.

Aidha, Diwani wa Viti Maalum, Pica Chogelo, aliwasilisha kilio kwa TANESCO, kuwa kati ya kata zote 17 za Manispaa ya Shinyanga, Mwamalili ni pekee isiyokuwa na huduma ya umeme na kuomba watekelezewe ili wananchi wapate huduma hiyo na kuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo.

Kwa upande wake, Meneja wa TANESCO mkoani Shinyanga, alifafanua suala la kukatika kwa umeme linatokana na hitilafu ya miundombinu ya uzalishaji na usambazaji umeme, pamoja na matengenezo ya dharura na kinga yanayofanyika mara kwa mara.

Alisema shirika hilo linaendelea na juhudi mbalimbali za matengenezo ili kuhakikisha hali ya kawaida inarejea na umeme usikatike tena, huku akiahidi suala la ukosefu wa huduma hiyo Kata ya Mwamalili kulifanyia kazi ili wapate wa REA.

## HABARI KIMATAIFA

# Burkina Faso yadaiwa kuingia vitani

**OUAGADOUGOU,** Burkina Faso

WAZIRI wa Ulinzi wa Burkina Faso, Kanali Kassoum Coulibaly, amesema mapambano wanayoendelea nayo dhidi ya wanajihadi ambao wanasababisha maafa makubwa katika nchi yake tangu mwaka 2015 ni vita vya kuiokoa Burkina Faso.

Aidha, kiongozi huyo wa ulinzi alitoa wito kwa wananchi wa taifa hilo kutetea nchi yao kwa kwenda kwenye uwanja wa vita.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika hafla ya kusherehekea kumbukumbu ya miaka 62 ya kuundwa kwa jeshi la kitaifa la Burkina Faso, ambapo mada ilikuwa "Vikosi vya jeshi la kitaifa na raia kwa ushirikiano kwa ajili ya kurejesha maeneo yanayokaliwa na wanajihadi kwenye himaya ya serikali".

"Ikiwa kwa muda mrefu mapambano dhidi ya ugaidi yameonekana kama vita jukumu pekee la vikosi vya ulinzi na usalama, ni wakati wa kubadilisha mtazamo huu ili kufanya kuwashirikisha raia kwa vikosi vyenye nguvu zaidi vinavyopambana," alisema na kuongeza:

"Kila raia lazima atambue kuwa hii ni vita ambayo hatima yetu ya pamoja iko hatarini kwa bahati mbaya, nikimaanisha, kuishi kwa taifa letu, na kujitolea ili kupigana kwa kiasi kikubwa dhidi ya makundi ya kigaidi yenye silaha," alisema Coulibaly.

Ilielezwa kuwa wiki iliyopita, makao makuu ya jeshi la nchi hiyo yalizindua utaratibu wa kuajiri watu 50,000 wanaojitolea kwa ajili ya ulinzi wa nchi (VDP) na wasaidizi wa kiraia, ambao lazima waje kuimarisha safu za jeshi katika muktadha wa mapambano dhidi ya ugaidi. **RFI**



Kombora la Korea Kaskazini likifyatuka. **PICHA: DW**

# Zelensky ataka ulinzi usafirishaji nafaka

**KYIV,** Ukraine

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky ametoa wito kwa ulimwengu kujiweka tayari kujibu jarabio lolote la Russia la kuvuruga usafirishaji wa nafaka ya nchi hiyo.

Zelensky alitoa wito huo siku kadhaa baada ya Moscow kutangaza kujitoa kutoka kwenye mkataba uliouruhusu kusafirishwa tena kwa bidhaa za Ukraine.

Katika ujumbe wa video alioutoa usiku wa kuamkia Jumatano, Zelensky alisema hadi sasa meli zinazobeba shehena ya nafaka na bidhaa nyingine bado zinaingia na kutoka katika bandari za Ukraine lakini usalama wa muda mrefu wa njia ya bahari zinakopita unahitajika.

Alisema Russia ni lazima ifahamishwe kwamba dunia haitokaa kimya iwapo itathubutu kuvuruga usafirishaji wa nafaka na bidhaa za Ukraine zinazotegemewa na mamia kwa mamilioni ya watu duniani.

Aidha, inaelezwa kuwa Russia ilitangaza kusitisha ushiriki wake kwenye mkataba wa kusafirisha nafaka za Ukraine mwishoni mwa juma lililopita baada ya kuituhumu Kyiv kuzishambulia meli zake zinazopiga doria kwenye Bahari Nyeusi. **DW**


WATUMISHI HOUSING Investments

## TANGAZO KWA UMMA

**(Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Gazeti la Serikali Na. 15 la Mwaka 1997.)**

Watumishi Housing Investments (WHI) inatoa taarifa kwa umma kuwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, imeidhinisha Waraka wa Matarajio na Mkataba wa Udhamini wa kuendesha Mfuko wa Faida, yaani Faida Fund. Faida Fund ni mfuko wa uwekezaji wa pamoja unaoendeshwa na Watumishi Housing Investment ambaye ni Meneja wa Mfuko na Benki ya CRDB ambaye ni Mdhamini wa Mfuko. WHI ni Kampuni ya Serikali ya uendelezaji milki na usimamizi wa uwekezaji iliyo chini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Faida Fund inatoa fursa kwa wananchi kuwekeza katika bidhaa kwenye masoko ya fedha ikiwa ni pamoja na Hatifungani za Serikali, Hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa. Mfuko unaruhusu ushiriki wa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, ukijumuisha watu binafsi, taasisi na kampuni. Kiwango cha chini cha kuwekeza ni shilingi 10,000 na hakuna na kiwango cha juu cha ukomo wa uwekezaji. Kiwango cha chini cha nyongeza ya uwekezaji ni shilingi 5,000. Uwekezaji unafanyika kwa kujaza fomu ya maombi na kuweka fedha katika akaunti ya Mfuko kupitia matawi ya Benki ya CRDB au au wakala wa Soko la Hisa (Stockbrokers). Wawekezaji pia wanaweza kuwekeza kwa njia ya kielektoniki: www.whi.go.tz, au kwa simu kupitia USSD Code *152*00# au kwa Wekeza WHI App ambayo inaweza kupakuliwa kutoka AppStore au PlayStore. Maelezo ya kina yamewekwa katika Fomu ya Maombi.

Kipindi cha mauzo ya awali kimefunguliwa rasmi tarehe 1 Novemba 2022 na kinatarajiwa kufungwa tarehe 31 Desemba 2022. Baada ya kipindi cha mauzo ya awali, vipande vya uwekezaji vitaendelea kuuzwa kwa kufuata mwenendo wa Soko.

Wananchi wote wanaotarajia kuwekeza katika Mfuko wa Faida wanashauriwa kuwasiliana na wakala wa Soko la Hisa, meneja wa benki, wanasheria, wahasibu au wataalamu wa masuala ya uwekezaji kwa ushauri kabla ya kufanya uwekezaji.

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu, Watumishi Housing Investments 4th Floor, Golden Jubilee Towers,**
**Ohio, Street Dar es Salaam,**
**S. L. P. 5119 Dar es Salaam, Simu: +255 22 292211,**
**Barua pepe: info@whi.go.tz, Tovuti: www.whi.go.tz**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ...........TANGA

Kituo cha MJINI TANGA...........Mkoa...TANGA

Usimamizi wa Mirathi Na................212/2022

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: JUMAA HATIBU PEMBE

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: HUSSEIN JUMAA PEMBE

## TANGAZO

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo tarehe 10 mwezi 11 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leo Tarehe ....28... mwezi ...10...mwaka 2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI TANGA

---

FORM 58

IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 997 OF 2022

In the Matter of the Estate of the Late RUSTICA MICHAEL MASOTA
and

In the Matter of Application for Letters of Administration
by
MICHAEL GELASIUS MASOTA

## GENERAL CITATION

(Rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 01 day of 12, 2022.

Dated at DAR ES SALAAM this 01 day November, 2022.

Senior Resident Magistrate

---

NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

M/MWANZO MWANZA MJINI- SHAURI LA MADAI Na. 345/2021
ZAKARIA PAULO ____________MDAI
DHIDI YA
HAMIS MOHAMED SAID ____________MDAIWA

MM/ ILEMELA- SHAURI LA MADAI NO. 50/2022
ROSEMARY RWECHUNGURA ______________MDAI
DHIDI YA
MSAFIRI MASIGE __________MDAIWA

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA **MAHAKAMA YA MWANZO MWANZA MJINI -NA MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA - MWANZA ,** TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI PIKIPIKI MOJA YENYE USAJILI Na. MC 422 CRN AINA YA KINGLION. NA PIKIPIKI SAN LG NA. MC 914 ACD. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ZILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | PIKIPIKI 1 USAJIRI NA. MC 422 CRNAINA YA KINGLION | YADI YA NYADHI INVESTMENT CO.LTD BUSWELU - MWANZA | 17/11/2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | PIKIPIKI SAN LG NA. MC 914 ACD | YADI YA NYADHI INVESTMENT CO.LTD BUSWELU - MWANZA | 17/11/2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI KWA MALI INAYOHAMISHIKA/ISIYOHAMISHIKA.
2. MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0768-588155**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE

Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM

Usimamizi wa Mirathi Na. 2105/2022

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SHABANI FELI MBENEKA

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ELIZABETH BENJAMIN MBANO

## TANGAZO

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 05 Mwezi wa 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 31 Mwezi wa 10 Mwaka 2022.

HAKIMU

---

SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999

KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI

BARUA YA TOLEO YENYE L.O NO. S.66676,

MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: ALI KIBWANA
SLP 110,
KOROGWE.

ARDHI: KIWANJA NAMBA 3 KITALU 'F' NEW KOROGWE,

HALMASHAURI YA MJI KOROGWE.

MWOMBAJI: ALFA ALLY
SLP 110
KOROGWE.

Taarifa imetolewa kwamba BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iliyotajwa hapo juu, imepotea na inakusudiwa kutoa nakala halisi ya barua ya kumiliki ardhi iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja, tangu taarifa ilipotangazwa katika gazeti. BARUA HALISI YA TOLEO ikipatikana irudishwe kwa Mkurugenzi wa Halmashsuri ya Mji KOROGWE WA SLP 615 KOROGWE.

Nyambega D. Kichele,
AFISA ARDHI MTEULE,
HALMASHAURI YA MJI KOROGWE

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DAR ES SALAAM

SHAURI LA MADAI NA. 23 YA MWAKA 2022
AHAZI TERU MWAMGOGWA.........................................MDAI

DHIDI YA

BEST SELL BUREAU
DE CHANGE LIMITED......................................MDAIWA WA KWANZA
GEOFREY WILLIAM MRAMIA...................................MDAIWA WA PILI

**Kwa:**
1. BEST SELL BUREAU DE CHANGE
2. GEOFREY WILLIAM MRAMIA

## KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la madai kwa njia ya uwakilishi (Representative) dhidi ya wadaiwa tajwa ambalo maelekezo yake yameelezwa katika nakala za hati ya madai, hivyo basi kwa mujibu wa Amri ya 1 kanuni ya 8 ya sharia ya Mwenendo wa Mashauri ya madai sura ya 33 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2019, mtu yeyote mwenye maslahi na shauri hili anatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii, binafsi au kupitia wakili au mwakilishi wake ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 23/11/2022 saa tatu (3:00) kamili asubuhi mbele ya J.D.LUAMBANO, NAIBU WAKILI kujibu au kuonesha maslahi yake katika shauri husika. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo vinathibitisha maslahi yako katika shauri hili.

**ANGALIZO:**
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa umepokea wito huu, basi shauri litasikilizwa na kutolewa maamuzi bila wewe mwenyewe kuwepo.
HATI hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya mahakama leo hii tarehe 27 Mwezi 10 2022

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM

---

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**VICKY JIM JENGO** anatangaza kupotelewa na passport yenye No. **TAE270441** iliyotelewa 03 January, 2020 na kuisha 02 January, 2030. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa polisi: **DOD/DOD/RB/427625/2022.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**PETER EDWARD** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma ; cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S1373-0113** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MBELEI SECONDARY SCHOOL mwaka 2010 na CHETI CHA UALIMU GRADE A chenye usajili namba: **E0583-0276** kilichotolewa na CHUO CHA UALIMU SAHARE TANGA mwaka 2013. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **DAR/GOG/RB/78297/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAKIKA OMARI RASHIDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **CS19203697** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SHULE YA SEKONDARI MNACHO mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **LIN/RUA/RB/420021/2022**


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Killy amalizana rasmi na Konde Music

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Killy, ametangaza kumalizana rasmi na Lebo ya Konde Music Worldwide na sasa yupo huru na tayari amepata usimamizi mpya.

Nyota huyo ambaye alikuwa chini ya lebo hiyo inayomilikiwa na Harmonize, amedokeza kwamba tayari ametengeneza ngoma mpya chini ya usimamizi wake mpya.

"Mungu ndiye mkuu wa nyakati zote Walahhi. Huru rasmi sasa hivi. Alhamdulillah. Oya, wanangu jitayarisheni kwa kibao kipya," aliandika kwenye Instagram yake.

"Video mpya za muziki, usimamizi mpya, fedha mpya, kila kitu kipya. Lakini pia msisahau kujisajili kwenye YouTube Channel yangu inayojulikana kama "OfficialKilly". Tuondokeni wanangu muda wetu huu!!"

Aidha, Killy tayari amefuta picha na video zote kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Usimamizi wa Lebo ya Bongo ya Konde Music Worldwide, ulitangaza kuondoka kwa Killy na mwenzake Cheed mapema mwezi uliopita.

Bosi wa lebo hiyo, Harmonize aliweka wazi walifikia makubaliano ya kutengana na wasanii hao wawili.

Killy na Cheed walijiunga na Konde Music Worldwide mwaka wa 2020 baada ya kutoka kwenye Lebo ya Ali Kiba ya Kings Music Records.





# WANANE WAHOJIWA KIFO CHA MTOTO WA DAVIDO

**LAGOS,** Nigeria

WAFANYAKAZI nane wanahojiwa na polisi baada ya kifo cha mtoto wa kike wa mwanamuziki wa Nigeria, Davido, Ifeanyi, kilichotokea Jumatatu.

Kwa mujibu wa Msejaji wa Jeshi la Polisi wa Jiji la Lagos nchini Nigeria, Benjamin Hundeyin, wafanyakazi hao wanahojiwa kutokana na kufa maji kwa mtoto huyo.

Ifeanyi ambaye alifikisha miaka mitatu Oktoba 20, mwaka huu, alizama na kufariki kwenye bwawa la kuogelea nyumbani kwa mwimbaji huyo, Banana Island.

Hundeyin aliwaambia waandishi wa habari kuwa wafanyakazi hao nane wa ndani walichukuliwa kwa mahojiano juzi. Alisema baada ya uchunguzi, watakaobainika kutokuwa na hatia katika tukio hilo wataachiwa huku watakaobainika kuwa na hatia watabaki polisi kwa uchunguzi zaidi.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Nigeria, mpishi na mlezi wa Ifeanyi walikuwa jikoni na wakasahau kumuangalia mtoto huyo na kujikuta wakianza kumtafuta bila mafanikio.

Iliwachukua zaidi ya dakika 20 mpishi na mlenzi wa mtoto huyo kumtafuta hadi mlinzi alipomwona akielea kwenye bwawa.

Wakati tukio hilo linatokea, Davido na mpenzi wake ambaye ni mama wa mtoto huyo, Chioma walikuwa wamelala kutokana na uchovu wakiwa wametoka safari.

Kutokana na Davido kuwa kama mtu aliyechanganyikiwa baada ya kifo cha mtoto wake huyo, polisi imewapiga marufuku marafiki na wafanyakazi kumtembelea kwani yupo kwenye usimamizi maalum.

# Vanessa atarajia mtoto wa pili

**Na Mwandishi Wetu**

MUIMBAJI wa muziki wa Bongo Fleva ambaye kwa sasa anaishi nchini Marekani, Vanessa Mdee, anatarajia mtoto wa pili.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Vanessa amefichukua kwamba yeye na mpenzi wake, Rotimi wanatarajia mtoto wa pili wa kike. Tayari wapenzi hao Vanessa na mpenzi wake huyo kutoka nchini Marekani mwenye asili ya Nigeria, wana mtoto mmoja waliyempa jina la Seven.

"Tayari nina ujauzito nakaribia kupata mtoto wa pili ambaye ni wa kike," aliandika Vanessa.

Vanessa aliondoka nchini Tanzania baada ya kutangaza kuachana na muziki wa Bongo Fleva miaka miwili iliyopita.



# PHIRI, LUSAJO WAINGIA MBIO YA KIATU CHA LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Simba, Moses Phiri amefikisha jumla ya mabao matano sawa na Reliants Lusajo wa Namungo ambapo wote hao sasa wanaliongoza kundi la wachezaji waliofunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

**Bao alilofunga Jumapili iliyopita dhidi ya Mtibwa, limemfanya Phiri kufikisha idadi hiyo, huku timu yake ikiwa imecheza mechi nane tu, Namungo ikiwa na Lusajo yenyewe ikicheza mechi tisa.**

Phiri amebainisha kuwa mbali na kwamba anacheza kwa ajili ya kuipatia Simba matokeo, lakini amejiingiza kwenye kinyang'anyiro cha kusaka Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu msimu huu, akisema anakitaka kwa udi na uvumba.

Mbali na Mtibwa Sugar, mabao yake mengine ameyafunga kwenye mechi dhidi ya Geita Gold, Kagera Sugar, KMC na Dodoma Jiji, na hakufanikiwa kufunga kwenye mechi tatu dhidi ya Yanga, Azam na Tanzania Prisons.

Kwa upande wa Lusajo, alifunga mabao mawili kwenye mechi dhidi ya Mtibwa Sugar, moja dhidi ya Ihefu, Ruvu Shooting na Coastal Union, huku akishindwa kufunga katika mechi tano, dhidi ya KMC, Kagera Sugar, Prisons, Geita Gold na Polisi Tanzania.

Wachezaji wanaofuatia, wenye mabao manne kila mmoja ni Sixtus Sabilo wa Mbeya City, Matheo Antony wa Mbeya City na Feisal Salum wa Yanga.

Straika wa Yanga, Fiston Mayele yupo katika kundi la wachezaji wenye mabao matatu kila mmoja, wengine ni Augustine Okrah wa Simba, Charles Ilamfya wa Mtibwa Sugar, Hassan Maudid wa Mbeya City, Abdulkassim Suleiman wa Ruvu Shooting, Nickson Kibabage wa Mtibwa Sugar na Amza Moubarack wa Coastal Union.

## NAIMBA...




Msanii wa Nyimbo za Injili nchini, Rose Muhando (kulia), akiimba mbele katika mkutano na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana wakati akitangaza kushiriki tamasha linaloandaliwa na Msama Promotions la kuliombea taifa amani pamoja na kumwombea, Rais Samia Suluhu Hassan kwa uongozi bora, litakalofanyika jijini Mwanza baadaye mwezi huu. Kushoto ni Mratibu wa Tamasha hilo, Emmanuel Mabisa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Precision Air yatia mkono Kombe la FA*

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka nchini (TFF), limeingia mkataba wa mwaka mmoja wenye thamani ya Sh. milioni 108 na Shirika la Ndege la Precision Air kwa ajili ya kudhamini Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania, maarufu FA Cup kwa msimu wa 2022/23.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema wameingia mkataba kwa mara ya kwanza na Precision Air kwa kutoa tiketi za ndege kuweza kufikisha watendaji kufika katika vituo husika.

Alisema mkataba huo hautakuwa wa fedha, bali watapokea tiketi zenye thamani ya mkataba huo kwa kuwezesha watendaji wa shirikisho hilo na wahusika wa mchezo kufika kwa haraka katika vituo husika.

"Udhamini huu utasaidia sana na kurahisisha safari za watendaji kufika sehemu husika na utakuwa kwa ajili ya Kombe la FA na Ligi ya Mkoa (RCL), tumeanza na Precision Air na milango iko wazi kwa wengine wanaotaka kuingia kusaidia soka la Tanzania," alisema Karia.

Alisema wameanza na FA na wanatarajia baadaye kuingia katika udhamini wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ajili ya kuendeleza soka nchini.

Naye Mkurugenzi wa Precision Air, Patrick Mwanri, alisema wamedhamini FA ikiwa ni kuendelea kuunga mkono sera ya serikali ya kusaidia michezo hasa katika soka.

"Tumeamua kuwekeza katika soka tukianza na kudhamini tiketi za ndege zenye thamani ya Sh. milioni 108 ambazo ni kwa ajili ya kuwezesha watendaji kufika kwa haraka kituoni," alisema Mwanri.

Alisema watafanya tathmini baada ya mkataba huo na kisha kuangalia namna ya kuendelea kutoa mchango wao katika ligi zingine ikiwamo Ligi Kuu.

Michuano ya Kombe la FA kwa msimu huu wa 2022/23, inatarajiwa kuanza rasmi Jumamosi wiki hii kwa mechi kadhaa za hatua za awali, ikiwa ni safari ya kuanza kusaka timu itakayoiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika.

## JWTZ Gofu Lugalo kushindana Malawi

**Na Meja Selemani Semunyu**

WACHEZAJI 12 wa Klabu ya Gofu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ya Lugalo wakiongozwa na Mkuu wa Majeshi Mstaafu, Jenerali George Waitara, wameondoka jana jijini Dar es Salaam kuelekea Lilongwe nchini Malawi kushiriki mashindano ya siku nne ya mchezo huo, imeelezwa.

Akizungumza wakati wa maandalizi ya safari hiyo juzi, Mkurugenzi wa Michezo na Utamaduni wa JWTZ, Kanali Martin Msumali, alisema lengo la mashindano hayo ni kudumisha ushirikiano na Malawi na pia kuchangia fedha kwa ajili ya Maveterani wa Vita wa Malawi ambao walipigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

Kwa upande wa Balozi na Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Ulinzi, Job Masima, ambaye ni miongoni mwa waliokwenda katika mashindano hayo alisema amejisikia furaha kupata nafasi hiyo muhimu kwa ushirikiano.

"Ni nafasi nzuri kushiriki mashindano hayo, ninalishukuru Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kukubali mwaliko huu, nina amini safari hii itakuwa na manufaa pande zote mbili," alisema Masima.

## TFB yasaka filamu bora 2022 mikoani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BODI ya Filamu Tanzania (TFB), imeanza usajili wa kazi za sanaa za maigizo nchini kwa ajili ya kuziingiza katika shindano na kupata filamu bora ya mwaka 2022 ambapo zoezi hilo linafanyika kupitia mikoa yote ya Tanzania kwa kusajili kazi mbalimbali zilizochezwa na wasanii.

Shindano hilo linatarajiwa kufanyika Desemba 17, mwaka huu jijini Arusha kwa kushindanisha zaidi ya kazi 1,000 ambazo zitawasilishwa na wasanii ukilinganisha na shindano lililofanyika mwaka jana kwa kushindanisha kazi 600.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Filamu nchini, Emmanuel Ndumukwa, wakati wa ukusanyaji wa kazi za sanaa akiwa wilayani Kahama na kufafanua kuwa, lengo ni kuzitambulisha kazi zinazofanywa na wasanii wa mikoani ili kukuza soko lao.

Alisema moja ya kigezo wanachokizingatia katika filamu zinazowasilishwa ni ubora wa kazi, picha, mazingira ya kuigizia na hadithi yenyewe, huku akikumbusha kwamba katika mashindano ya mwaka jana Filamu ya Janga kutoka Mbeya ndiyo iliibuka mshindi kwa kuzishinda kazi nyingine.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**BELLINGHAM DAU KUBWA**

KLABU ya Borussia Dortmund huenda ikahitaji dau la rekodi ya pauni milioni 130 ili kumuuza kinda wa England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, anayezivutia Manchester United, Chelsea na Liverpool. ***(Sun)***

**DE GEA KUPUNGUZA MSHAHARA**

GOLIKIPA wa Hispania, David de Gea, 31, yuko tayari kupunguza mshahara wake wa pauni 375,000 kwa wiki katika Klabu ya Manchester United ili kuongeza muda wake wa kukaa Old Trafford. ***(Athletic, via Sun)***

**RABIOT ATAKIWA CHELSEA**

CHELSEA wanapewa nafasi kubwa ya kumsajili kiungo wa kati wa Juventus na Ufaransa, Adrien Rabiot, 27, katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Fichajes)***

**EVERTON NAYO KWA BROJA**

KLABU za Everton na Newcastle United zinamfuatilia mshambuliaji wa Chelsea na Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 21. ***(CBS Sports)***

**EMERY MKATABA MREFU**

KOCHA Unai Emery ametia saini mkataba wa angalau miaka minne na nusu, mkataba mrefu zaidi wa ukocha katika historia ya Aston Villa, huku akijiandaa kuanza kazi yake rasmi wiki hii. ***(Telegraph)***

**TROSSARD AWANIWA CHELSEA**

KLABU ya Chelsea imetoa ofa ya dau la pauni milioni 30 kumnunua mshambuliaji wa Brighton na Ubelgiji, Leandro Trossard, 27. ***(FourFourTwo)***

**ARTETA KUMBADILI XAVI**

BARCELONA wanamtazama kocha wa Arsenal, Mikel Arteta mwenye umri wa miaka 40, kama mbadala wa kocha Xavi Hernandez mwenye miaka 42. ***(Sport)***

**ARSENAL, CHELSEA KWA ZAHA**

MATUMAINI ya Arsenal na Chelsea kumsajili fowadi wa Ivory Coast, Wilfried Zaha yameongezeka, kwani mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, bado hajakubali kuongezewa mkataba katika klabu ya Crystal Palace licha ya kuombwa kuongezewa mpya kwa maneno. ***(Mail)***

**KROSS HAJAAMUA MADRID**

KIUNGOA wa kati wa Ujerumani, Toni Kroos, 32, bado hajaamua kama atastaafu au kuongeza mkataba wake Real Madrid msimu ujao. ***(ESPN)***

**SCHUURS KUMRITHI VAN DIJK**

MLINZI wa Torino, Perr Schuurs, 22, yuko kwenye orodha fupi ya Liverpool kama mrithi wa muda mrefu wa beki wa kati wa Uholanzi, Virgil van Dijk, 31. ***(Tuttomercato)***

**SHELVEY KUFUNGWA**

KIUNGO wa kati wa Newcastle United, Jonjo Shelvey, 30, anatazamiwa kuongezwa mkataba wa mwaka mmoja wenye thamani ya zaidi ya pauni milioni 3. ***(Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA: HALAAND ATAKUWA FITI WIKIENDI

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ana matumaini Erling Haaland atarejea kutoka kwenye jeraha wikendi hii na anatumai pia Kalvin Phillips na Kyle Walker watakuwa fiti kabla ya Kombe la Dunia.

**Haaland, ambaye amefunga mabao 17 katika mechi 11 za Ligi Kuu England msimu huu, alikosa mechi ya ushindi wa wikendi dhidi ya Leicester City kutokana na tatizo la kifundo cha mguu.**

Mshambuliaji huyo alipata jeraha wakati City wakitoka suluhu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya klabu yake ya zamani, Borussia Dortmund wiki iliyopita, huku akishindwa kuendelea wakati wa mapumziko.

Guardiola alithibitisha Jumamosi kwamba Haaland pia atakosekana kwenye mchezo wa leo Jumatano dhidi ya Sevilla kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku wao wakiwa tayari wamefuzu.

Lakini anaonekana kuwa na matumaini kuhusu matarajio ya Haaland kurejea kwa wakati wakimenyana na Fulham kwenye Uwanja wa Etihad Jumamosi.

Guardiola amesema; "Anajisikia vizuri ukilinganisha na Jumamosi, Jumapili, Jumatatu, kila siku anajisikia vizuri, lakini bado si asilimia 100 hatutaki kuchukua hatari maana tunatumaini kuwa tunaye na ana jisikia vizuri."


> Anajisikia vizuri ukilinganisha na Jumamosi, Jumapili, Jumatatu, kila siku anajisikia...

Mchezaji mwenzake aliyesajiliwa kabla ya msimu mpya, Phillips amekosekana kwa muda mrefu baada ya kuumia bega katika mchezo wa kirafiki dhidi ya Barcelona Agosti mwaka huu.

Kiungo huyo wa zamani wa Leeds United ambaye amecheza dakika moja pekee ya soka ya Ligi Kuu msimu huu aliishia kuhitaji upasuaji na amekuwa nje tangu katikati ya Septemba mwaka huu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,046,4
MECHI KALI
REAL SOCIEDAD
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 3.06
X | 3.30
2 | 2.27
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DEPAY AGEUKA LULU JUVE, ROMA



**ROME,** Italia

MIAMBA ya Italia, AS Roma imejitosa kwenye mbio za farasi wawili na Juventus katika kinyang'anyiro cha kuwania saini ya mshambuliaji wa Barcelona, Memphis Depay.

Mshambuliaji huyo wa Uholanzi alijiunga na timu hiyo ya Hispania msimu wa majira ya joto mwaka 2021 kwa uhamisho wa bure baada ya mkataba wake na Lyon kumalizika.

Alifunga mara 13 katika mechi 38 alizoichezea Barcelona msimu uliopita, lakini sasa pale Nou Camp amejikuta akiwa nyuma ya wachezaji wengine washambuliaji kama vile Ousmane Dembele, Ferran Torres na Ansu Fati.

Depay alikuwa akihusishwa na kuhamia Juventus wakati wa majira ya joto, huku miamba hao wa Katalunya wakitaka kumsogeza katika harakati zao za kusajili wachezaji wao wa majira ya joto kabla ya kampeni mpya.

Roma ya Kocha Jose Mourinho sasa imejiunga na wapinzani wao wa Serie A katika mbio za kumsaka Depay.

Kutokana na mwanzo mbaya wa Juventus msimu huu, ambao umewafanya watoke nje ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kushika nafasi ya saba kwenye Ligi ya Italia, timu hiyo ya Max Allegri bado ina nia ya kuongeza wachezaji kwenye kikosi chao.



## Messi atabiriwa kung'ara Marekani

**NEWYORK,** Marekani

GOLIKIPA wa zamani wa Klabu ya Aston Villa na Timu ya Taifa ya Marekani, Brad Friedel, anaamini nyota wa PSG, Lionel Messi, atang'ara zaidi ya Pele akihamia Ligi Kuu ya Marekani.

Ikumbukwe gwiji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Pele ndiye mchezaji aliyewahi kutikisa zaidi alipohamia nchini Marekani katika Klabu ya New York Cosmos mwaka 1975.

Lakini golikipa huyo wa zamani wa Aston Villa amesema anaamini Messi atavunja rekodi hiyo.

Watu wengi wanaamini Messi atamalizia soka nchini Marekani na inaaminika klabu inayomilikiwa na David Beckham, Inter Miami ilifanya jaribio la kumsajili nyota huyo kutoka Klabu ya PSG, lakini ikashindikana.

Beckham ambaye alijiunga na Klabu ya Los Angeles Galaxy mwaka 2007, aliwavutia mastaa wengi wa kizazi chake kama Thierry Henry, Andrea Pirlo, Kaka, Frank Lampard, pamoja Steven Gerrard kucheza kwenye ligi hiyo.

Inaaminika Messi kabla ya kustaafu soka atakwenda kushiriki Ligi Kuu ya Marekani na Brad anaamini litakuwa jambo kubwa na lenye mapokezi makubwa zaidi kuliko Pele, ambaye alikuwa na mapokezi makubwa zaidi kwenye historia ya ligi hiyo.

## HABARI MICHEZO


433,814/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/11/22 | 18:00 | Blackpool vs Luton Town | 2.83 | 3.23 | 2.48 |
| 02. 05/11/22 | 18:00 | QPR vs West Bromwich | 2.44 | 3.29 | 2.84 |
| 03. 05/11/22 | 18:00 | Nottingham vs Brentford | 2.73 | 3.28 | 2.54 |
| 04. 05/11/22 | 19:00 | AC Ajaccio vs Strasbourg | 2.73 | 3.08 | 2.63 |
| 05. 05/11/22 | 20:00 | Galatasaray vs Besiktas | 2.43 | 3.33 | 2.83 |
| 06. 05/11/22 | 20:30 | Everton vs Leicester | 2.33 | 3.27 | 3.03 |
| 07. 05/11/22 | 21:00 | PAU FC vs Amiens | 2.79 | 3.14 | 2.64 |
| 08. 05/11/22 | 21:00 | Bastia vs Paris FC | 2.49 | 3.11 | 3.01 |
| 09. 05/11/22 | 21:00 | Dijon vs Guingamp | 2.50 | 3.16 | 2.96 |
| 10. 05/11/22 | 22:30 | Arminia Bielefeld vs Kaiserslautern | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 11. 06/11/22 | 14:30 | Bologna vs Torino | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 12. 06/11/22 | 15:00 | Chelsea vs Arsenal | 2.63 | 3.28 | 2.63 |
| 13. 06/11/22 | 15:30 | KAA Gent vs Brugge | 2.54 | 3.59 | 2.54 |
| 14. 06/11/22 | 15:30 | Eintracht Braunschweig vs Greuther Furth | 2.54 | 3.28 | 2.73 |
| 15. 06/11/22 | 17:00 | Clermont Foot vs Montpellier | 2.31 | 3.52 | 2.83 |
| 16. 06/11/22 | 19:05 | Lille vs Rennes | 2.48 | 3.48 | 2.63 |
| 17. 06/11/22 | 19:30 | Tottenham vs Liverpool | 2.88 | 3.53 | 2.30 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 03/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2959 | Hangzhou NG vs Shenzhen | 1.66 | 3.95 | 4.70 |
| 14:30 | 1902 | Chengdu Qianbao vs Hebei Zhongji | 1.04 | 9.72 | 28.19 |
| 14:30 | 2636 | Wuhan Three Towns FC vs Guangzhou RF | 1.21 | 6.45 | 8.40 |
| 15:00 | 1955 | Ararat Armenia vs Van Yerevan | 1.50 | 3.75 | 6.03 |
| 16:00 | 2277 | Espoir FC vs APR FC | 8.20 | 4.10 | 1.41 |
| 16:05 | 2690 | Dhofar Salalah vs Sohar Club | 1.99 | 2.98 | 3.81 |
| 16:30 | 1206 | Bunyodkor vs Surkhon Termez | 1.71 | 3.32 | 4.69 |
| 16:30 | 1377 | Nasaf Qarshi vs Dinamo Samarqand | 1.09 | 7.60 | 19.47 |
| 16:30 | 2790 | Lokomotiv Tashkent vs Navbahor Namangan | 3.95 | 3.05 | 2.05 |
| 16:30 | 5082 | Olympique de Beja vs Avenir Rjich | 2.18 | 2.67 | 3.74 |
| 17:00 | 4327 | FC Goa vs Jamshedpur | 2.52 | 3.45 | 2.42 |
| 17:00 | 4737 | Shabab Al Ordun vs AL Salt | 2.02 | 3.12 | 3.51 |
| 17:00 | 4833 | Shirak Gyumri vs Alashkert Martuni | 5.82 | 3.74 | 1.51 |
| 18:30 | 1538 | Rigas Futbola Skola vs Fiorentina | 8.17 | 5.18 | 1.33 |
| 18:30 | 5597 | Basaksehir vs Hearts | 1.29 | 5.59 | 8.78 |
| 18:50 | 1849 | AL Qadsia vs AL Tadamon | 1.39 | 4.28 | 6.81 |
| 20:00 | 3091 | Sandnes Ulf vs Kongsvinger IL | 1.94 | 3.63 | 3.53 |
| 20:45 | 1379 | AZ Alkmaar vs SC Dnipro 1 | 1.35 | 5.19 | 7.39 |
| 20:45 | 1397 | Pyunik Yerevan vs FC Basel | 4.00 | 3.70 | 1.82 |
| 20:45 | 1508 | Olympiakos vs Nantes | 3.10 | 3.40 | 2.21 |
| 20:45 | 1581 | Zalgiris vs Slovan Bratislava | 3.06 | 3.36 | 2.25 |
| 20:45 | 2052 | KAA Gent vs Molde | 1.98 | 3.56 | 3.51 |
| 20:45 | 2256 | Apollon Limassol vs FC Vaduz | 1.65 | 3.90 | 4.80 |
| 20:45 | 2855 | Trabzonspor vs Ferencvaros TC | 1.54 | 4.21 | 5.41 |
| 20:45 | 3104 | Karabakh vs SC Freiburg | 1.98 | 3.59 | 3.50 |
| 20:45 | 4589 | Real Sociedad vs Manchester Utd | 3.06 | 3.30 | 2.27 |
| 20:45 | 4647 | CFR Cluj vs KF Ballkani | 1.47 | 4.56 | 6.28 |
| 20:45 | 4953 | Monaco vs Red Star Belgrade | 1.63 | 4.10 | 4.70 |
| 20:45 | 5172 | Djurgardens IF vs Shamrock Rovers | 1.41 | 4.70 | 6.79 |
| 20:45 | 5742 | Feyenoord vs Lazio | 2.21 | 3.50 | 3.00 |
| 20:45 | 5770 | Slavia Prague vs Sivasspor | 1.39 | 4.86 | 7.49 |
| 20:45 | 5973 | Midtjylland vs Sturm Graz | 1.92 | 3.55 | 3.75 |
| 20:45 | 5993 | Sheriff Tiraspol vs Omonia Nicosia | 1.93 | 3.56 | 3.71 |
| 21:00 | 1528 | Sporting Gijon vs Albacete Balompie | 2.26 | 3.02 | 3.27 |
| 21:00 | 1614 | FC Cartagena vs Malaga | 1.76 | 3.37 | 4.66 |
| 23:00 | 1002 | Granada vs Levante | 2.48 | 2.98 | 2.93 |
| 23:00 | 1081 | Rennes vs AEK Larnaca | 1.17 | 7.03 | 13.05 |
| 23:00 | 1238 | Hapoel Beer Sheva vs Austria Vienna | 1.67 | 3.80 | 4.80 |
| 23:00 | 1513 | Sporting Braga vs Malmo | 1.29 | 5.43 | 9.24 |
| 23:00 | 1721 | Arsenal vs FC Zurich | 1.19 | 6.82 | 12.24 |
| 23:00 | 2091 | Lech Poznan vs Villarreal | 2.96 | 3.36 | 2.30 |
| 23:00 | 2340 | Roma vs Ludogorets Razgrad | 1.32 | 5.22 | 8.44 |
| 23:00 | 2436 | Silkeborg vs Anderlecht | 2.43 | 3.40 | 2.75 |
| 23:00 | 2547 | Dynamo Kiev vs Fenerbahce | 3.85 | 3.70 | 1.85 |
| 23:00 | 3405 | Partizan vs Slovacko | 1.64 | 3.95 | 4.81 |
| 23:00 | 3892 | Union Saint Gilloise vs Union Berlin | 3.79 | 3.54 | 1.91 |
| 23:00 | 4002 | Betis vs HJK Helsinki | 1.23 | 5.97 | 10.94 |
| 23:00 | 5226 | Bodo Glimt vs PSV Eindhoven | 3.15 | 3.75 | 2.06 |
| 23:00 | 5611 | FC Koln vs Nice | 2.01 | 3.50 | 3.50 |
| 23:00 | 5916 | Steaua Bucuresti vs West Ham | 5.81 | 4.31 | 1.50 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MABONDIA TANZANIA WAAHIDI USHINDI USIKU WA DOME BOXING

**Na Mwandishi Wetu**

MABONDIA wa Tanzania wametamba kuibuka washindi dhidi ya wapinzani wao kutoka nje ya nchi katika usiku wa Super Dome Boxing uliopangwa kufanyika kesho katika ukumbi mpya wa kisasa wa Super Dome Arena jijini Dar es Salaam.

**Mapambano hayo yameandaliwa kwa ushirikiano wa kampuni yenye uzoefu mkubwa wa kuandaa ngumi za kulipwa duniani, Global Boxing Stars kwa ushirikiano na Kampuni ya Tanzania, LP Sport chini ya udhamini wa Azam TV kupitia usiku wa vitasa.**

Akizungumza jana, bondia Nasibu Ramadhani amesema kuwa amejiandaa kumchapa mpinzani wake kutoka Afrika Kusini, Toto Helebe katika uzito wa feather.

Ramadhan alisema anajua kuwa mpinzani wake amekuja kusaka ushindi, lakini 'amepotea' njia kwani amedhamiria kumchapa mapema zaidi.

"Nimejiandaa vilivyo, nawaomba Watanzania waje kwa wingi kunipa sapoti katika pambano hili, ninaahidi sitowaangusha," alisema Ramadhani.

Mbali ya Ramadhani, bondia mwingine, Shaaban Jongo ametamba kumchapa mpinzani wake kutoka Uganda, Musa Ntege, katika pambano la uzito wa cruiser wa Afrika (ABU) kwa nchi za Afrika Mashariki. Endapo Jongo atashinda pambano hilo, atapata fursa ya kuwania ubingwa wa Afrika dhidi ya bondia Olanweragu Doradola na kuingizwa katika viwango vya WBC.

Kwa upande wa bondia Salehe Kassim, ameahidi ushindi dhidi ya Mghana Patrick Aryee katika pambano la uzito wa super feather.

Watanzania wengine, Fadhili Majiha amesema amejiandaa kutoa kipigo kwa mpinzani wake kutoka Ghana, Manyo Plange huku Mohamed Pesa akiahidi kumchapa Tope Tajdeen wa Nigeria katika pambano la uzito wa featherweight. Naye Hamis Palasungulu ametamba kumchapa Solomon Adebayo wa Nigeria katika pambano la uzito wa juu.

Mapambano mengine ya siku hiyo yatakuwa kati ya bondia Paul Kamatha dhidi ya Lemi Madeje wakati Sarafina Julius Bella akizipiga na Sara Alex katika uzito wa fly kwa upande wa wanawake.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa LP Sport, Levis Paul, amesema maandalizi ya mapambano hayo yamekamilika na wanatarajia kuwa na msisimko mkubwa zaidi.



Bondia Nasibu Ramadhani wa Tanzania (Katikati), akisisitiza jambo wakati wa utambulisho wa mabondia watakaopambana kesho kwenye usiku wa Dome Boxing. Kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa LP Sport, Levis Paul na kushoto ni Mtangazaji maarufu wa Ngumi za Kulipwa, Wasiwasi Mwabulambo wa Azam TV. **MPIGAPICHA WETU**

## Simba yazitaka 18 za Novemba

INATOKA UKURASA 32

matibabu wakati Jimmyson akitarajiwa kuwa nje kwa muda zaidi.

Mgunda alisema anajua mapambano kati yao na watani zao ni makubwa, lakini kitu cha msingi yeye anaangalia zaidi mechi zao kuhakikisha wanacheza vizuri na kupata ushindi mwisho wa msimu ndio atajua timu gani imekuwa bingwa.

Jumapili iliyopita Simba ilitoa dozi nzito ya mabao 5-0 kwa Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, kipigo ambacho ni kikubwa zaidi kuwahi kutolewa tangu kuanza kwa msimu huu wa Ligi Kuu Bara.

## *Yanga yajiweka pagumu*

INATOKA UKURASA 32

matunda.

Yanga itakuwa na kibarua kingine kigumu zaidi Jumatano ijayo ugenini nchini Tunisia, kwenye Uwanja wa Olympique Rades Hamadi Agrebi na mshindi wa mchezo huo atatinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

### WAGOMA KUINGIA VYUMBANI

Uongozi wa Club African uligomea wachezaji wake kuingia kwenye chumba cha kubadilishia nguo kwa kile kilichoonekana kama ni hofu tu ya kukutana na hujuma ya wenyeji wao, Yanga, hivyo kulazimika kutumia ukumbi maalum ambao unatumika kwa ajili ya mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi.

Baada ya kutokea sintofahamu hiyo, viongozi wa timu hiyo waliamua kutumia ukumbi huo kwa ajili ya wachezaji wao kubadilisha nguo pamoja na kupeana mawaidha machache kabla ya mechi hiyo.

Licha ya mechi kuchezwa mchana na siku ya kazi, lakini mashabiki wa Yanga walijitokeza kwa kiasi kwa ajili ya kuisapoti timu yao katika mchezo huo uliokuwa muhimu kwao kupata ushindi wa nyumbani.

# Michezo



Alhamisi Novemba 3, 2022

Nipashe

'Halaand atakuwa fiti wikiendi' UKURASA 29

# Yanga SC yajiweka pagumu CAF

●●● Sasa yalazimika kushinda Tunisia, Club Africain yailazimisha sare ikigoma kuingia...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MABINGWA wa Tanzania Bara Yanga jana walijiweka katika wakati mgumu wa kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kushindwa kuutumia vema uwanja wa nyumbani, Benjamin Mkapa, kutokana na kulazimishwa suluhu dhidi ya Club Africain ya Tunisia.

**Kama Yanga ingekuwa makini ingeweza kupata angalau ushindi wa bao moja, lakini wachezaji wake licha ya kuutawala kwa asilimia kubwa mchezo huo, ilishindwa kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kuwa na kazi rahisi kwenye mechi ya marudiano jijini Tunisi Jumatano ijayo.**

Dakika ya sita tu, Tuisila Kisinda alitanguliziwa mpira na Kibwana Shomari, lakini wakati wenzake wakisubiri krosi wauweke mpira ndani ya wavu, ulimzidi mbio na kutoka nje.

Kona fupi ilipigwa na Stephane Aziz Ki na kumkuta Khalid Aucho na kupiga krosi iliyowapita mabeki wawili wa Club Africain kabla ya kutua kwenye kichwa cha Yanick Bangala, lakini mpira uliishia kwa kupaa juu ya lango.

Club African karibuni kipindi chote cha mchezo ilionekana kukaa nyuma ya mpira na kuwaacha Yanga wakitengeneza mashambulizi, ilifanikiwa kufanya shambulizi la kwanza na la pekee kipindi cha kwanza dakika ya 20 kupitia kwa Abdenoour Belhoucini, lakini shuti lake liliendа nje ya lango.

Feisal Salum kama kawaida yake, akiwa nje kidogo ya lango alijitengenezea nafasi ya kupiga shuti kali, lakini lilitoka juu kidogo na pembeni mwa lango la wageni wao.

Yanga ilikosa bao lingine dakika ya 28, kichwa cha Fiston Mayele aliyewahadaa mabeki wa Club Africain, kilitua mikononi mwa kipa Mouez Hassan.

Nafasi nzuri zaidi ya Yanga kuweka mpira ndani ya wavu ilikuwa dakika ya 45, wakati Aziz Ki alipopiga krosi iliyowababatiza mabeki wa Club Africain na mpira ukatua kwa Mayele ambaye alibabaika kabla ya kipa kuuwahi miguuni mwake.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, ambapo wawakilishi wa Tanzania Yanga, waliwatoa Bernard Morrison, Kisinda na Djuma Shaaban, nafasi zao zikichukuliwa na Farid Mussa, Jesus Moloko na Heritier Makambo.

Kuingia kwa Makambo kulimaanisha kuwa Yanga ilikuwa na mastraika wawili uwanjani ambao walikuwa wakisaka mabao kwa ajili ya ushindi wa nyumbani, lakini hilo halikutokea.

Kuchelewa kupiga krosi kwa Morrison kabla hajatolewa, kuliwakosesha Yanga bao, ambapo mpira ulioporwa na Fei Toto alimpelekea mchezaji huyo ambaye aliambaa nao peke yake kwenye wingi ya kulia, huku wenzake wakiwa wamefika golini wakisubiri atie majalo, lakini 'aliupaka rangi' mpira kabla haujafagiliwa na mabeki wa timu pinzani.

Kipa Mouez alifanya kazi ya ziada dakika ya 70, aliporuka juu kwenye kona ya juu ya maungio ya lango na kupangua shuti kali lililopigwa na Mayele.

Kuingia kwa mastraika wawili Youssef Snana na Hamdi Labidi, pia beki wa kulia Hamza Agrebi kuliwafanya wageni hao kuanza kwenda mbele na kufanya mashambulizi makali dakika ya 86 na 87.

Shuti la Snana liliishia mikononi mwa Djigui Diara, huku akifanya kazi nyingine ya ziada alipopangua shuti kali la mbali kutoka kwa Labidi na kuwa kona ambayo haikuzaa

INAENDELEA UK. 31

KOKOTA...



Mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, akikokota mpira dhidi ya beki wa timu ya Club Africain, Ahmed Khalil, kwenye mechi ya mchujo ya mkondo wa kwanza ya kuwania kushiriki hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa sare tasa. **MPIGAPICHA WETU**

## Simba yazitaka 18 za Novemba

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Simba kinajipanga kuzoa pointi zote 18 katika michezo yake sita ya Ligi Kuu kitakachocheza mwezi huu wa Novemba, lengo likiwa kutafuta nafasi ya kurejea kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

Katika michezo hiyo sita, Simba itaanza kucheza dhidi ya Singida Big Stars katika Uwanja wa Liti mkoani Singida Novemba 9 kabla ya siku tatu baadaye kurejea Dar es Salaam katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Ihefu FC.

Novemba 16, Simba itashuka tena katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kuialika Namungo FC na siku tatu baadaye itakuwa ugenini kuvaana na Ruvu Shooting kabla ya Novemba 23 kuifuata Mbeya City katika Dimba la Sokoine jijini Mbeya.

Mchezo wa mwisho mwezi huu kwa Simba, utakuwa dhidi ya Polisi Tanzania ugenini utakaopigwa Novemba 27, ambao utakamilisha hesabu zao hizo.

Kwa sasa Simba ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 17 katika michezo nane, wakizidiwa alama tatu na watani wao wa jadi, Yanga walioko kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema malengo yao ni kuhakikisha wanafanya vizuri katika kila mechi ili kufikia kile kinachotarajiwa na Wanasimba.

Alisema anajua hakuna mechi rahisi kwao na ushindani umekuwa mkubwa kwenye ligi, hivyo yeye na wachezaji wake wanalazimika kupambana bila kuchoka ili kufikia kile ambacho wamekikusudia.

"Hakuna mechi rahisi, tunatakiwa kujipanga vizuri katika mechi zote tutakazocheza mwezi huu [Novemba] ili kutimiza lengo letu, kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kutimiza wajibu wake, naamini tukifanya hivyo uhakika wa ubingwa msimu huu ni mkubwa," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema anafurahi kurudi kwa baadhi ya wachezaji wake muhimu waliokuwa majeruhi akiwamo mchezaji mwandamizi, Shomari Kapombe ambao kwa namna fulani wameongeza ubora kutokana na uzoefu waliokuwa wao.

Alisema leo timu inaendelea na programu mbalimbali za kiufundi ili kuboresha viwango vya wachezaji kuelekea michezo hiyo.

"Kuhusu hali ya majeruhi ndani ya kikosi, mpaka sasa ni mlinzi wa kulia tu, Israel Mwenda na Jimmyson Mwanuke ndio bado wanaendelea kupata matibabu," alisema.

Alisema Mwenda anatarajia kurudi uwanjani hivi karibuni kutokana na kuendelea vizuri na

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002